# VIONGOZI WA WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO



**Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana (Mb.)**
**WAZIRI**



**Mhe. Hamisi Mwinjuma (Mb.)**
**NAIBU WAZIRI**



**Bw. Saidi Yakubu**
**KATIBU MKUU**



**Bw. Nicholas Mkapa**
**NAIBU KATIBU MKUU**

# YALIYOMO

ORODHA YA VIFUPISHO ............................................ iv

1.0 UTANGULIZI ........................................................ 1

2.0 DIRA, DHIMA, MAJUKUMU, MISINGI YA MWELEKEO, VIPAUMBELE VYA WIZARA NA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA ....... 12

3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU KWA KIPINDI CHA MWAKA 2022/23 ............................................................ 15

4.0 CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA NA HATUA ZILIZOCHUKULIWA KUKABILIANA NAZO ............................................................... 131

5.0 MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24 ............................................... 136

5.1 SEKTA YA UTAMADUNI ................................. 136

5.1.1I DARA YA MAENDELEO YA UTAMADUNI. 136

5.1.2 BARAZA LA KISWAHILI LA TAIFA (BAKITA) ............................................................ 138

5.1.3 MFUKO WA UTAMADUNI NA SANAA TANZANIA ........................................................ 139

5.2 SEKTA YA SANAA ............................................ 140

5.2.1 IDARA YA MAENDELEO YA SANAA........... 140

5.2.2 BODI YA FILAMU TANZANIA ....................... 141

5.2.3 BARAZA LA SANAA LA TAIFA (BASATA) .. 142

5.2.4 OFISI YA HAKIMILIKI TANZANIA (COSOTA) ......................................................... 143

5.2.5 TAASISI YA SANAA NA UTAMADUNI BAGAMOYO (TaSUBa) .................................. 143
5.3 SEKTA YA MICHEZO .................................. 144
5.3.1 IDARA YA MAENDELEO YA MICHEZO..... 144
5.3.2 BARAZA LA MICHEZO LA TAIFA (BMT) ... 145
5.4 MIRADI YA MAENDELEO .............................. 146
5.5 KUIMARISHA UTENDAJI WA WIZARA NA RASILIMALI WATU .......................................... 153

6.0 MAKADIRIO YA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24 ............................................. 154
6.1 MAPATO ........................................................ 154
6.2 MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO .................................................. 155

7.0 MAOMBI YA FEDHA KWA AJILI YA KUTEKELEZA MPANGO WA MWAKA 2022/23 ........................................................ 155

8.0 MWISHO NA SHUKURANI............................ 156

VIAMBATISHO ........................................................ 160

KIAMBATISHO NA.1 ............................................ 160
VITUO VILIYOTAMBULIWA NA BAKITA VYA KUFUNDISHA KISWAHILI KWA WAGENI................ 160

KIAMBATISHO NA. 2 ........................................... 164
MADUHULI YANAYOTARAJIWA KUKUSANYWA NA WIZARA NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA 2023/24 ..................................................................... 164

KIAMBATISHO NA.3 ........ 166
MGAWANYO WA BAJETI YA WIZARA YA MWAKA 2023/24 KWA IDARA NA VITENGO, TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA NA MIRADI YA MAENDELEO ........ 166

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| AAG | All African Games |
| ACCES | Africa Conference for Collaboration, Exchange and Showcase |
| ADPA | African Diamond Producers Association |
| AFPP | African Flight Procedure Programme |
| AFRIMMA | African Music Magazine Awards |
| AICC | Arusha International Conference Center |
| AMIS | Artist Management Information System |
| ARIPO | African Regional Intellectual Property Organization |
| AT | Athletics Tanzania |
| AU | African Union |
| BAKITA | Baraza la Kiswahili la Taifa |
| BASATA | Baraza la Sanaa la Taifa |
| BCDA | Bureau Congolais du Droit d'Auteur (BCDA) |
| BET | Black Entertainment Televison |
| BMT | Baraza la Michezo la Taifa |
| BRELA | Business Regulations and Licensing Agency |
| BSS | Bongo Star Search |
| CAC | Chamwino Arts Center |
| CAF | Confederation of African |

| | |
|---|---|
| | Football |
| CAPASSO | Composers Authors and Publishers Association |
| CCTV | Closed Circuit Television |
| CHANETA | Chama cha Netiboli Tanzania |
| CHANEZA | Chama cha Netiboli Zanzibar |
| CISAC | Confederation Internationale des Societes d'Auteurs et Composteurs |
| CMOs | Copyright Management Organizations |
| COSOL | Copyright Society of Liberia |
| COSOTA | Copyright Society of Tanzania (Ofisi ya Hakimiliki Tanzania) |
| DEV | Development |
| DRFA | Dar es Salaam Football Association |
| eGA | e - Government Authority |
| FEASSSA | Federation of East Africa Secondary School Sports Associations |
| FIFA | Federation Internationale de Football Association |
| GePG | Government electronic Payment Gateway |
| IDCA | International Deaf Cultural Arts |
| IFACCA | International Federation of Arts Council and Cultural Agencies |
| IFRRO | International Federation of Reproduction Rights |

| | |
|---|---|
| | Organizations |
| IFPI | International Federation of the Phonographic Industry |
| IOMMa | Indian Ocean Music Market |
| KKKT | Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania |
| JAMAFEST | Jumuiya ya Afrika Mashariki Festival |
| JICA | Japan International Cooperation Agency |
| JNICC | Julius Nyerere International Conference Center |
| KISUVITA | Kituo cha Sanaa na Utamaduni kwa Viziwi Tanzania |
| MMDI | Miss & Mr. Deaf International |
| NACP | National AIDS Control Programme |
| NACTVET | National Council for Technical and Vocational Eduction and Training |
| NBC | National Bank of Commerce |
| NBS | National Bureau of Statistics |
| NCAA | Ngorongoro Conservation Area Authority |
| NEEC | National Economic Empowerment Council |
| NMB | National Microfinance Bank |
| OAU | Organisation of African Union (Umoja wa Nchi Huru za Afrika) |
| OBFT | Open Boxing Federation of |

| | |
|---|---|
| | Tanzania |
| OC | Other Charges (Matumizi Mengineyo) |
| OR – TAMISEMI | Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| PAP | Pan African Parliament |
| PE | Personal Emoluments |
| PSSSF | Public Service Social Security Fund |
| RECs | Regional Economic Communities |
| RT | Riadha Tanzania |
| SADC | Southern African Development Community |
| SHIMISEMITA | Shirikisho la Michezo la Serikali za Mitaa Tanzania |
| SHIMIWI | Shirikisho la Michezo la Wizara na Idara za Serikali |
| SHIMMUTA | Shirikisho la Michezo la Mashirika ya Umma, Taasisi na Kampuni Binafsi Tanzania |
| TaBSA | Tanzania Baseball Association |
| TANAPA | Tanzania National Park |
| TaSUBa | Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo |
| TAFF | Tanzania Film Federation |
| TBA | Tanzania Building Agency |
| TBC | Tanzania Broadcasting Corporation |
| TCA | Tanzania Cricket Association |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |

| | |
|---|---|
| TanTrade | Tanzania Trade Development Authority |
| TCRA | Tanzania Communication Regulatory Authority |
| TCTA | Tanzania Correction Training Academy |
| TFB | Tanzania Film Board |
| TFF | Tanzania Football Federation |
| TGU | Tanzania Golf Union |
| THA | Tanzania Handball Association |
| THT | Tanzania House of Talent |
| TMA | Tanzania Music Award |
| ToT | Training of Trainers |
| TPA | Tanzania Port Authority |
| TRA | Tanzania Revenue Authority |
| TRU | Tanzania Rugby Association |
| TTA | Tanzania Tennis Association |
| TTTA | Tanzania Table Tennis Associaton |
| UAE | United Arab Emirates |
| UKIMWI | Ukosefu wa Kinga Mwilini |
| UMISSETA | Umoja wa Michezo ya Shule za Sekondari Tanzania |
| UMSOTA | Umoja wa Maveterani wa Soka Tanzania |
| UMITASHUMTA | Umoja wa Michezo na Taaluma kwa Shule za Msingi Tanzania |
| UNESCO | United Nations, Educational, Scientific and Cultural |
| UVIKO-19 | Ugonjwa wa Virusi vya |

| | |
|---|---|
| | Korona 2019 |
| VHS | Video Home System |
| VVU | Virusi vya UKIMWI |
| WCF | Workers Compensation Fund |
| WIPO | World Intellectual Property Organization |
| WIPOCOS | World Intellectual Property Organization Collective Societies |

**HOTUBA YA MHE. BALOZI DKT. PINDI HAZARA CHANA (MB.), WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO, AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA 2023/24**

## 1.0 UTANGULIZI

**1.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo katika Bunge lako Tukufu, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo (Fungu 96) kwa Mwaka wa Fedha 2023/24.

**2.** ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kutupatia uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana tena hapa Bungeni, na kuendelea kuijalia nchi yetu amani, utulivu, mshikamano na upendo.

**3.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu

Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo. Wizara hii ni muhimu kwa nchi yetu, ambayo kwa maneno mengine naweza kusema ni Wizara yenye nguvu shawishi (***soft power***) ya nchi, kwa maana ya kuwa inawaleta wananchi wenye itikadi tofauti pamoja, inaimarisha mshikamano na ushirikiano, inaleta furaha miongoni mwa wananchi, inadumisha amani na inajenga na kuimarisha afya za wananchi. Pia, inatoa ajira nyingi kupitia michezo na sanaa. Aidha, chambilecho wahenga, chanda chema huvikwa pete, naomba kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya kwa maendeleo ya nchi yetu. Pia, nimpongeze kwa mafanikio makubwa yaliyopatikana ndani ya kipindi cha miaka miwili (2) ya Serikali ya Awamu ya Sita katika sekta zetu ambayo yametokana na uongozi wake ulio mahiri, wenye weledi, umakini na upeo mkubwa unaoendelea kulishamirisha Taifa letu ndani na nje ya nchi. Sisi na wadau wetu wote wa sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo tunamuahidi kuendelea kumpa ushirikiano, kuchapa kazi kwa bidii na kwa weledi ili kuendana na fikra, maono, na falsafa yake ya "Kazi Iendelee". Aidha, nitumie fursa hii

kumuombea kiongozi wetu kwa Mwenyezi Mungu, awe na afya njema, Mungu aendelee kumpa hekima na busara katika kuiongoza nchi yetu.

**4.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa namna alivyo mstari wa mbele kwa kuwa kichocheo cha ukuaji wa Sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo ambapo hivi karibuni tumeshuhudia akiridhia Kocha wa Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu kulipwa mshahara na Serikali. Aidha, ikiwa ni sehemu ya uhamasishaji wake katika michezo, Mheshimiwa Rais alinunua tiketi 2,000 wakati wa mchezo wa Timu ya Taifa (Taifa Stars) dhidi ya Timu ya Taifa ya Uganda (The Cranes) uliofanyika katika Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam tarehe 28 Machi, 2023. Pia, amehamasisha Timu zetu za Yanga na Simba ambazo zimeshiriki mashindano ya kimataifa ngazi ya Afrika kwa kuwazawadia kila goli lililofungwa katika mashindano hayo Shilingi Milioni Tano (Sh. 5,000,000) katika hatua ya makundi. Hamasa hiyo iliendelea kwa timu hizo zilipofika hatua ya robo na nusu fainali kwa kutoa zawadi ya Shilingi Milioni Kumi (Sh. 10,000,000) kwa kila goli lililofungwa.

**5. *Mheshimiwa Spika,*** katika hatua ya fainali tumeshuhudia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiongeza dau kwa kuzawadia kila goli Shilingi Milioni Ishirini (Sh. 20,000,000). Aidha, ameweza kununua tiketi 5,000 zenye thamani ya Shilingi Milioni Ishirini na Tano (Sh. 25,000,000) kwa ajili ya mashabiki kuingia kuishangilia Timu ya Yanga katika mchezo uliofanyika tarehe 28 Mei, 2023 katika Uwanja wa Benjamin Mkapa dhidi ya USM Algiers. Pia ametoa usafiri wa ndege wa kuipeleka Timu ya Yanga na baadhi ya mashabiki wake nchini Algeria. Mchango wa Mheshimiwa Rais ndiyo chachu ya mafanikio ya timu za Simba na Yanga katika mashindano haya na kuiwezeshakufikia fainali kwa Timu ya Yanga na kama ambavyo Waswahili husema mwana hutazama uchogo wa mamaye, timu zinamwahidi kuendelea kuongeza jitihada. Hakika huyu ndiye mwanamichezo wa kweli na wa vitendo siyo wa maneno tu. Mheshimiwa Rais amekuwa akituunga mkono katika matukio na shughuli mbalimbali za Sekta zetu, ikiwemo Tamasha la Kimataifa la Michezo la Wanawake (*Tanzanite International Women Sports Festival*) na Mashindano ya Riadha kwa Wanawake ya *Ladies First*. Tunampongeza na kumshukuru sana.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** halikadhalika, ninawapongeza sana Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa katika kumsaidia Mheshimiwa Rais kutekeleza majukumu yake kwa hakika kinga na kinga ndipo moto uwakapo. Viongozi hawa wamekuwa wadau mahiri katika sekta zetu ambapo wameshirikiana nasi kuzindua au kufunga matukio mbalimbali ya Utamaduni, Sanaa na Michezo na kutupatia maelekezo pamoja na ushauri uliosaidia kuboresha sekta hizi. Ninawashukuru na kuwapongeza sana. Aidha, nizidi kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa Hotuba ya Bajeti yake iliyotoa utekelezaji wa malengo ya Serikali katika mwaka 2022/23 na mwelekeo wa shughuli za Serikali kwa mwaka 2023/24. Wizara yangu inaahidi kutekeleza maelekezo yote yaliyotolewa.

**7. *Mheshimiwa Spika,*** kipekee naomba nikupongeze wewe Mheshimiwa Spika kwa kuliongoza kwa busara na weledi Bunge la 11 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Maelekezo na miongozo yako imekuwa msingi wa ufanisi mkubwa wa Bunge katika kuisimamia Serikali kutekeleza vema majukumu yake. Vilevile, ninampongeza Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb.), Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kukusaidia na kukushauri vema katika majukumu yako ya kuliongoza Bunge. Nawapongeza sana Wenyeviti wa Bunge, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Mb.), Mheshimiwa Daniel Baran Sillo (Mb.) na Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile (Mb.) kwa kusimamia vema na kwa ustadi mkubwa mijadala ya kibajeti katika Bunge lako Tukufu.

**8. *Mheshimiwa Spika***, kivuli cha mvumo huwafunika walio mbali, Wizara hii ni kubwa na muhimu kama nilivyosema hapo awali kwani ni Wizara yenye nguvu shawishi (*soft power*) ya kukusanya na kugusa maisha ya Watanzania wengi wapenda michezo na burudani, hivyo, kila mtu katika nchi hii anaguswa na Wizara hii kupitia sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo. Naomba kumhakikishia Mheshimiwa Rais

utendaji ulio bora na uliotukuka katika utekelezaji wa majukumu aliyonikabidhi.

**9.** ***Mheshimiwa Spika,*** ukiona zinduna na ambari iko nyuma yake, naishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Prof. Kitila Alexander Mkumbo, Mbunge wa jimbo la Ubungo, Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko (Mbunge wa Viti Maalum), Makamu Mwenyekiti wa Kamati na Wajumbe wote wa Kamati kwa maelekezo, ushauri, michango na maoni yao kwa Wizara yangu ambayo yametusaidia sana katika kuboresha utendaji kazi. Maelekezo yao yamesaidia kwa kiwango kikubwa katika uwasilishaji wa hotuba hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Wizara itaendelea kuzingatia ushauri, maoni, mapendekezo na maelekezo yanayotolewa na Kamati kwa maendeleo ya Sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka wa fedha 2023/24.

**10.** ***Mheshimiwa Spika,*** papo kwa papo kamba hukata jiwe mafanikio yaliyopatikana katika kipindi chote hiki ni kutokana na ushirikiano mzuri miongoni mwa wadau wa

Wizara wakiwemo viongozi na watumishi wa Wizara. Natambua mchango mkubwa wa viongozi wenzangu wa Wizara wakati wa kufanikisha utekelezaji wa majukumu na mageuzi makubwa tunayoendelea nayo wizarani na katika sekta zetu. Nianze kwa kumshukuru kwa dhati kabisa Mheshimiwa Hamis Mwinjuma (Mb.), kwa lakabu "Mwana-FA", Naibu Waziri makini wa Wizara yangu kwa msaada mkubwa anaonipa katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Aidha, nimshukuru Bw. Saidi Yakubu, Katibu Mkuu anayehakikisha mambo yanakwenda na mageuzi yanatokea; Bw. Nicholas Mkapa, Naibu Katibu Mkuu mwenye jukumu la kuhakikisha ufanikishaji na kusonga mbele katika mageuzi makubwa ya tasnia za Utamaduni, Sanaa na Michezo; Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi, Wakuu wa Vitengo na Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara wanaofanya kazi kwa bidii na wanahakikisha mambo yanatokea na mipango inatekelezwa kama ilivyopangwa na Waswahili tunaamini ya kuwa kofi halilii kwa kiganja kimoja na kwa hakika ushirikiano wao umefanikisha.

**11.** ***Mheshimiwa Spika,*** mkono mmoja hauchinji ng'ombe niwashukuru kwa dhati watumishi wote wa Wizara na Taasisi zake kwa

kutekeleza kikamilifu majukumu yao kwa kujituma, hatimaye kuleta tija na ufanisi kwa Wizara. Aidha, napenda kuwashukuru Washirika wa Maendeleo na wadau wengine wakiwemo mashirikisho, vyama, vilabu na kila mdau mmojammoja kwa nafasi zake katika sekta ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa kuhakikisha Sekta hizi zinakua na zinaleta furaha kwa wananchi na kufikia malengo yaliyokusudiwa kwa mujibu wa Sera.

**12.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwenda tezi na omo marejeo ni ngamani, ninawashukuru wapiga kura wangu wanawake wa Mkoa wa Njombe kwa kuniamini na kuendelea kunipa ushirikiano mkubwa wakati wa utekelezaji wa majukumu yangu; na wakati wa kukabiliana na changamoto mbalimbali katika Mkoa wetu kwa lengo la kuwaletea maendeleo wanawake wa Mkoa wa Njombe. Ninawaahidi utumishi uliotukuka pamoja na ushirikiano wa dhati katika kipindi chote nitakachokuwa nikiwawakilisha katika Bunge hili Tukufu. Naomba waendelee kuniamini kwani mwana hasahau mkono uliomlea.

**13.** ***Mheshimiwa Spika,*** ni masikitiko yetu kwamba katika Bunge lako Tukufu lilipatwa na

msiba wa mpendwa wetu Mheshimiwa Mussa Hassan Mussa aliyekuwa Mbunge mwenzetu akiwawakilisha wananchi wa jimbo la Amani Zanzibar. Kwa niaba yangu binafsi, Wizara na wadau wetu wote, ninatoa pole kwako Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, familia ya marehemu, ndugu, jamaa na marafiki na wananchi wote wa jimbo la Amani Zanzibar na Tanzania kwa ujumla wake. Tunamuombea kwa Mwenyezi Mungu aipokee na kuilaza roho ya marehemu mahali pema peponi. Amina.

**14.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Aprili, 2023 Taifa letu pia limepoteza wadau mahiri na wa kutegemewa katika sekta zetu, wakiwemo wanamichezo, wanautamaduni na wasanii mbalimbali. Nitumie fursa hii kutoa pole kwa familia za marehemu wote, ndugu, jamaa, marafiki na kwa Watanzania wote kwa ujumla kwa kuwapoteza wapendwa wao "Tunaomba Mwenyezi Mungu azipokee roho za marehemu wote na kuzilaza mahali pema peponi". Amina.

**15.** ***Mheshimiwa Spika,*** hotuba hii imeandaliwa kwa kuzingatia maudhui ya Hotuba

ya Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2022/23 na Mwelekeo wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2023/24 aliyoiwasilisha hapa Bungeni tarehe 5 Aprili, 2023. Aidha, hotuba hii imezingatia Maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipohutubia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 22 Aprili, 2021; Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26); Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (2020 - 2025); Mpango Mkakati wa Wizara (2021/22 - 2025/26); na Sera, Sheria na Miongozo mbalimbali ya Sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo; na maelekezo mbalimbali ya viongozi wakuu wa Serikali.

**16.** ***Mheshimiwa Spika,*** hotuba yangu imegawanyika katika sehemu nane: Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi; Sehemu ya Pili ni Dira, Dhima, Majukumu, Misingi ya Mwelekeo, na Vipaumbele vya Wizara; Sehemu ya Tatu inaelezea Mapitio ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa kipindi cha Mwaka 2022/23 na

Sehemu ya Nne inabainisha changamoto zilizojitokeza na hatua zilizochukuliwa ili kuzipatia ufumbuzi. Aidha, Sehemu ya Tano ni Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2023/24; Sehemu ya Sita ni Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka 2023/24; Sehemu ya Saba ni Maombi ya Fedha kwa ajili ya kutekeleza Mpango wa Mwaka 2023/24; na mwisho, Sehemu ya Nane ni shukurani kwa wadau mbalimbali wa Wizara.

## 2.0 DIRA, DHIMA, MAJUKUMU, MISINGI YA MWELEKEO, VIPAUMBELE VYA WIZARA NA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA

**17.** ***Mheshimiwa Spika,*** dira ya Wizara ni ''***kuwa Wizara inayohakikisha ushiriki wa ushindani katika Utamaduni, Sanaa na Michezo kimataifa unaolenga maendeleo ya Taifa''*** na dhima ni ***''kukuza, kuwezesha na kuendeleza utambulisho wa Taifa kupitia maadili ya kiutamaduni, Sanaa na Michezo kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa Taifa''***.

**18.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kufikia Dira ya Wizara, majukumu ya Wizara ni pamoja na

kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria, Mipango, Miradi na Programu mbalimbali katika Sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo; kuendeleza shughuli za Utamaduni, Sanaa na Michezo na kusimamia shughuli za filamu na michezo ya kuigiza. Majukumu mengine ni kuimarisha utendaji na Rasilimali Watu Wizarani na kusimamia utendaji wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ambazo ni Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), Bodi ya Filamu Tanzania (TFB), Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa), Ofisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA), na Baraza la Michezo la Taifa (BMT). Vilevile, Wizara inaratibu na kusimamia Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya, Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika na Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania.

**19.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza na kuimarisha utendaji kazi, Wizara inaongozwa na misingi mitano ya kimkakati na kimageuzi ambayo ni Kuwafikia Wadau *(Outreach Programmes)*; Mageuzi ya Taasisi *(Institutional Reforms)*; Utawala Bora *(Good Governance)*; Uendelezaji wa Miundombinu *(Infrastructure Development)*; na Utafutaji wa Rasilimali

*(Resources Mobilization).*

**20.** ***Mheshimiwa Spika,*** chini ya misingi hiyo, katika mwaka 2023/24 Wizara imejipanga kutekeleza maeneo mbalimbali ya kipaumbele. Maeneo hayo ni pamoja na kukarabati, kuboresha, kujenga na kutunza miundombinu ya Utamaduni, Sanaa na Michezo; kukamilisha kutunga na kuhuisha Sera, Sheria, mikakati, miongozo na kanuni mbalimbali katika kuimarisha usimamizi na utekelezaji katika sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo; kuimarisha, kuziwezesha na kufanikisha ushiriki wa Timu za Taifa katika mashindano mbalimbali ya Kimataifa; kuweka na kuboresha mazingira wezeshi na kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi katika kukuza na kuendeleza sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo; na kuratibu, kuendesha na kusimamia matamasha, shughuli na matukio makubwa ya Utamaduni, Sanaa na Michezo.

**21.** ***Mheshimiwa Spika,*** maeneo mengine ni kuziimarisha na kuziongezea uwezo taasisi zilizo chini ya Wizara ili ziweze kusimamia na kutekeleza majukumu ya Sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo; kuimarisha ushirikiano na

Wizara nyingine katika utendaji kazi hususan zile zinazohusika na masuala ya Kazi na Ajira, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Elimu, Afya, Maliasili na Utalii, Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; na kuimarisha ushirikiano na wadau mbalimbali wakiwemo Sekta Binafsi katika maendeleo kwa kufadhili na kusukuma mbele gurudumu la Sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo.

## 3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU KWA KIPINDI CHA MWAKA 2022/23

## 3.1 MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA

### 3.1.1 Ukusanyaji wa Maduhuli

**22.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2022/23 Wizara ilikadiria kukusanya Shilingi Milioni Mia Tisa (Sh. 900,000,000) kutoka kwenye vyanzo viwili ambavyo ni mapato yatokanayo na viwanja vya Benjamin Mkapa na Uhuru pamoja na Ada za mafunzo na mitihani kutoka Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya. Vyanzo vyote vinatoka Idara ya Maendeleo ya Michezo. Hadi kufika mwezi Aprili, 2023 Shilingi

Milioni Mia Sita Themanini na Nane, Mia Nane Thelathini na Tisa Elfu, Mia Tano na Tisa (Sh. 688,839,509) sawa na asilimia 76.5 ya lengo zilikuwa zimekusanywa. Miongoni mwa sababu za kutofikia lengo ni pamoja na kutokamilika kwa miundombinu ya kumbi zilizopo uwanja wa Benjamin Mkapa ikiwemo vifaa; mwamko mdogo wa mashabiki kushabikia timu zilizopo nje ya kituo cha Dar es Salaam; na kutokuwasilishwa kwa wakati madai ya kodi ya pango katika eneo changamani la michezo Dar es Salaam.

**23.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Wizara inaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuongeza makusanyo ya mapato ikiwemo kufanya ukarabati mkubwa wa miundombinu katika uwanja, ili kuwezesha kuvutia mashabiki wengi zaidi; kuongeza hamasa katika michezo ikiwemo zawadi mbalimbali kwa washindi ili kuhamasisha matokeo mazuri yatakayochochea ushabiki na hatimaye mapato; na ufuatiliaji wa karibu wa madai ya pango kwa mujibu wa mikataba ya upangaji.

**24.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Taasisi zilizo chini ya Wizara, kiasi kilichokadiriwa kukusanywa ni Shilingi Bilioni

Tano, Milioni Mia Tatu Tisini na Sita, Mia Nne Hamsini na Tano Elfu (Shilingi 5,396,455,000) ambapo shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Tisa Tisini na Nane, Mia Tatu Kumi na Tano Elfu, Mia Sita Kumi na Moja (Shilingi 2,998,315,611) sawa na asilimia 55.5 ya lengo zilikuwa zimekusanywa hadi kufikia mwezi Aprili, 2023. Miongoni mwa sababu zilizochangia kutofikiwa malengo ni kutokana na wadau wengi wa filamu kufanya kazi zao bila ya kufuata utaratibu wa kisheria ikiwemo kukosa vibali na kuingiza filamu sokoni kabla ya kuhakikiwa; na kuchelewa kukusanywa na kugawanywa kwa mirabaha ya kazi za wabunifu. Fauka ya hayo, kwa upande wa vyuo, moja ya sababu ni wanavyuo kutokulipa ada kwa wakati kutokana na changamoto mbalimbali.

Wizara kupitia Taasisi inaendelea kutoa elimu kwa wadau na kufanya kampeni mbalimbali ili kuweza kukabiliana na changamoto hizo. Kampeni hizo ni pamoja na kuhamasisha usajili na kufuata taratibu za uzalishaji na usambazaji wa kazi za sanaa; kuongeza kasi ya kuibua vyanzo vipya vya mapato kwa taasisi; utekelezaji wa mabadiliko ya Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Na. 7 ya mwaka 1999; na kuhamasisha wanavyuo kulipa ada kwa wakati.

### 3.1.2 Bajeti ya Matumizi ya Wizara na Mtiririko wa Fedha

**25.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2022/23, Wizara iliidhinishiwa bajeti yenye jumla ya Shilingi Bilioni Thelathini na Tano, Milioni Mia Nne Ishirini na Tano, Mia Tisa Tisini na Moja Elfu (Sh. 35,425,991,000) ambapo kati ya hizo Mishahara ilikuwa Shilingi Bilioni Nane, Milioni Mia Mbili na Moja, Mia Nane Themanini na Mbili Elfu (Sh. 8,201,882,000), Matumizi Mengineyo (OC) shilingi Bilioni Kumi na Moja, Milioni Mia Tatu Tisini na Mbili, Mia Tisa Arobaini na Tisa Elfu (Sh. 11,392,949,000) na Miradi ya Maendeleo (DEV) Shilingi Bilioni Kumi na Tano, Milioni Mia Nane Thelathini na Moja, Mia Moja Sitini Elfu (Sh. 15,831,160,000).

**26.** ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 Wizara ilipokea jumla ya Shilingi Bilioni Ishirini na Nane, Milioni Mia Moja Sitini na Moja, Mia Tisa Thelathini na Nne Elfu, Mia Saba Sabini na Moja (Sh. 28,161,934,771) sawa na asilimia 79.5 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha zilizopokelewa, Shilingi Bilioni Tisa, Milioni Mia Tano Sitini na Moja, Mia Tatu Themanini Elfu, Mia Tisa Tisini na Tisa (Sh. 9,561,380,999)

ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo ya Wizara na Taasisi sawa na asilimia 83.9 ya bajeti ya Matumizi Mengineyo; Shilingi Bilioni Sita, Milioni Mia Saba Sabini na Mbili, Mia Tatu Tisini Elfu, na Themanini na Moja (Sh. 6,772,390,081) ni Mishahara ya Wizara na Taasisi sawa na asilimia 82.5 ya bajeti ya Mishahara; na Shilingi Bilioni Kumi na Moja, Milioni Mia Nane Ishirini na Nane, Mia Moja Sitini na Tatu Elfu, Mia Sita Tisini (Sh. 11,828,163,690) ni Miradi ya Maendeleo ambayo sawa na asilimia 74.7 ya bajeti ya Miradi ya Maendeleo.

## 3.2 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA MWAKA 2022/23

### 3.2.1 SEKTA YA UTAMADUNI

#### 3.2.1.1 IDARA YA MAENDELEO YA UTAMADUNI

**27.** ***Mheshimiwa Spika,*** sekta ya utamaduni ina majukumu ya kuhifadhi na kuendeleza urithi wa utamaduni, lugha na maadili ya Taifa; kuendeleza utambulisho wa Taifa; kuhimiza na kukuza utaifa kwa vijana na wananchi kwa ujumla; kukuza lugha ya Kiswahili ambayo ni lugha ya Taifa kupitia Baraza la

Kiswahili la Taifa (BAKITA); kufanya tafiti katika uga wa sekta ya utamaduni hususan lugha za kijamii ambazo ni kibebeo cha urithi wa utamaduni wetu na kuratibu na kusimamia shughuli za Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika na Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania. Katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2022 hadi Aprili, 2023 Sekta hii imetekeleza majukumu ambayo yamefafanuliwa kama ifuatavyo:

**28.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa wananchi wetu wanaendelea kunufaika na utamaduni wao, Wizara iliratibu Tamasha kubwa la Kitaifa la Utamaduni lililofanyika kuanzia tarehe 1 hadi 3 Julai, 2022 Jijini Dar es Salaam. Tamasha hilo lilitoa fursa kwa wananchi wetu kufanya matembezi ya kiutamaduni, mashindano ya ngoma za asili, maonesho ya vyakula vya asili, maonesho ya kazi za mikono za kiutamaduni na ubunifu pamoja na kuuza kazi hizo. Jumla ya vikundi 24 vya ngoma za asili kutoka mikoa ya Tanzania Bara na vikundi viwili (2) kutoka mikoa miwili (2) ya Zanzibar vilishiriki katika Tamasha hilo. Vilevile, Maafisa Utamaduni, Machifu na Viongozi wa Kimila walishiriki katika Tamasha hilo. Aidha, Serikali iliadhimisha Siku ya Uanuai

wa Utamaduni Duniani tarehe 21 Mei, 2023 kwa kuendesha Kongamano lililohusisha wanafunzi wa Vyuo Vikuu na vya Kati vya Mkoa wa Dodoma. Kongamano hilo lilifanyika katika Chuo Kikuu cha Dodoma ambapo mada zilizowasilishwa zilijikita katika Utamaduni na Maadili ya Mtanzania.

**29.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Michezo, Sanaa na Utamaduni ya Jamhuri ya Afrika Kusini iliratibu Tamasha la Msimu wa Utamaduni wa Tanzania na Afrika Kusini lililofanyika katika mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma na Morogoro kuanzia tarehe 18 Novemba 2022 hadi 4 Desemba 2022. Tamasha hilo lilikuwa na lengo la kuimarisha ushirikiano wa kiutamaduni baina ya Tanzania na Afrika Kusini. Aidha, Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Kushirikiana na Wizara ya Michezo, Sanaa na Utamaduni ya Jamhuri ya Afrika Kusini inaendelea na maandalizi ya Tamasha la Utamaduni wa Mtanzania linalotarajiwa kufanyika nchini Afrika Kusini mwaka 2023. Lengo la Tamasha hilo ni kutangaza kazi za Sanaa, Utamaduni, ubunifu kimataifa na asili ya Mtanzania na utamaduni wake.

**30.** ***Mheshimiwa Spika,*** umuhimu wa lugha ya Kiswahili umekuwa ukiongezeka siku hadi siku. Kutokana na hilo, ni ukweli usiopingika kuwa, kwa sasa mawanda ya matumizi na maendeleo ya lugha adhimu na aushi ya Kiswahili yamekuwa makubwa kitaifa na kimataifa. Hii imesababisha Kiswahili kuwa lugha ya mawasiliano mapana katika nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati. Aidha, Kiswahili imekuwa Lugha rasmi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na ni Lugha rasmi na ya Kazi ya Umoja wa Afrika (AU). Kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya lugha hii, Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) limepitisha tarehe 7 Julai ya kila mwaka kuwa Siku ya Kiswahili Duniani, ambayo kwa mara ya kwanza ilisherehekewa tarehe 7 Julai, 2022.




*Mkutano Mkuu wa 41 wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO), umepitisha Julai 7 ya kila mwaka kuwa Siku ya Kiswahili Duniani.*

**31.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Mei, 2023, Wizara iliendelea kuratibu na kushiriki katika matamasha mbalimbali yaliyoandaliwa na Wadau wa Utamaduni yakiwemo; Tamasha la Kwanza la Utalii la Jumuiya ya Afrika Mashariki lililofanyika Jijini Arusha tarehe 9 - 16 Oktoba, 2022; Tamasha la Utamaduni la Jamii za Watu wa Mwanza tarehe 4 - 8 Septemba, 2022 katika viwanja vya Kisesa Magu Jijini Mwanza; Tamasha la 12 la Muziki wa Cigogo lililofanyika tarehe 23 - 25 Julai, 2022 Wilayani Chamwino - Dodoma chini ya usimamizi wa Kituo cha Sanaa cha Chamwino "Chamwino Arts Center (CAC)" ambapo wadau wa Utamaduni na Sanaa zaidi ya

600 walishiriki katika Tamasha hilo; Tamasha la Utamaduni baina ya Tanzania na India kuhusu Mapokezi ya Balozi wa Amani Duniani na Kiongozi wa Kiroho Mheshimiwa Gurudev Sri Sri Ravi Shankar lililofanyika tarehe 24 Agosti, 2022 katika Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Julius Nyerere Jijini Dar es Salaam; na Tamasha la Utamaduni kutoka Mkoa wa Mbeya lijulikanalo kwa jina la Tulia Traditional Dance lililofanyika kuanzia tarehe 22 - 24 Septemba, 2022 Jijini Mbeya. Matamasha haya hutoa fursa na nafasi kwa wananchi wetu katika maeneo mbalimbali nchini kuusherehekea na kuudumisha utamaduni wao. Hali hii huonesha uhai wa utamaduni wa Mtanzania.




*Tamasha la 12 la Muziki wa Cigogo lililofanyika tarehe 23 - 25 Julai, 2022 Wilayani Chamwino - Dodoma chini ya usimamizi wa Kituo cha Sanaa cha Chamwino "Chamwino Arts Center (CAC)"*




*Tamasha la Utamaduni baina ya Tanzania na India la Mapokezi ya Balozi wa Amani Duniani na Kiongozi wa Kiroho Mheshimiwa Gurudev Sri Sri Ravi Shankar lililofanyika katika Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Mwl. Julius Nyerere Jijini Dar es Salaam tarehe 24 Agosti, 2022.*

**32.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa tunaendelea kudumisha utamaduni na utambulisho wa Taifa la Tanzania, Wizara iliunda Kamati ya Kitaifa ya upatikanaji wa Vazi la Taifa. Katika kipindi cha mwezi Julai mpaka Aprili, 2023, Kamati hiyo imekamilisha mapendekezo ya awali ya upatikanaji wa vazi hilo. Hatua inayoendelea kwa sasa ni kukusanya maoni ya wadau na wananchi kwa ujumla kuhusu vazi la utambulisho wa Taifa.

### 3.2.1.2 BARAZA LA KISWAHILI LA TAIFA (BAKITA)

**33.** ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu ya Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) ni pamoja na kuendeleza, kustawisha na kuimarisha lugha ya Kiswahili nchini na kufuatilia maendeleo yake nje ya nchi; kuhimiza matumizi ya lugha ya Kiswahili katika shughuli za Serikali na umma; kuratibu utafiti wa Kiswahili kwa kushirikiana na wadau na kuhimiza matumizi fasaha na sanifu ya lugha ya Kiswahili na kuzuia upotoshaji wake. Katika kipindi hiki mafanikio lufufu yamepatikana kama ifuatavyo:

**34.** ***Mheshimiwa Spika,*** BAKITA iliandaa maadhimisho ya kwanza ya Siku ya Kiswahili

duniani yaliyofanyika tarehe 4 - 7 mwezi Julai, 2022 Jijini Dar es Salaam. Maadhimisho hayo yalifana na yalihudhuriwa na jumla ya washiriki 1,514 wakiwamo wageni kutoka nchi za Ujerumani, China, Uingereza, Urusi, Misri, Uganda, Ghana, Afrika Kusini, Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo, Kenya na Burundi. Mafanikio ya maadhimisho hayo ni pamoja na kusainiwa kwa Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano kati ya Tanzania na Afrika Kusini katika Elimu ya Msingi na Ufundishaji wa Kiswahili. Vilevile, katika maadhimisho hayo *Mkakati wa Taifa wa Kubidhaisha Kiswahili* ulizinduliwa rasmi na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango tarehe 07 Julai, 2022. Aidha, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/23, Baraza liliandaa *Mwongozo wa Maadhimisho ya Kiswahili Duniani* ambao ulisambazwa katika Balozi za Tanzania na kutumiwa na Balozi hizo katika kuadhimisha Siku hiyo. Hali kadhalika, Baraza lilituma mwakilishi katika ubalozi wa Ujerumani kushirikiana nao katika kuadhimisha Siku ya Kiswahili Duniani.




*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Mpango akizindua Mkakati wa Taifa wa Kubidhaisha Kiswahili ndani na nje ya nchi wa mwaka 2022-2032 wakati wa kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Kiswahili Duniani iliyofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Mwl. Julius Nyerere Jijini Dar es salaam tarehe 7 Julai 2022.*

**35.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa lugha ya Kiswahili inazidi kukua na kuendelea, mwezi Agosti, 2022 BAKITA kwa kushirikiana na wachapishaji liliandaa na kugawa Vitabu 1,640 vyenye thamani ya shilingi milioni 50 kwa ubalozi wa Tanzania nchini Ujerumani na nchi zinazohudumiwa na ubalozi huo zikiwemo nchi za Polandi, Uswizi, Bulgaria, Hungary, Romania, Jamhuri ya Cheki, Jamhuri ya Slovakia na Holly See ambavyo vinakusudiwa kutumika katika vituo na vyuo vikuu

vinavyofundisha Kiswahili. Pia, vitabu hivi viligawiwa kwa Klabu ya Kiswahili inayofahamika kama **Kijiwe cha Kiswahili** nchini Ujerumani ambacho kimetambuliwa na BAKITA kama kituo rasmi cha kufundisha na kuendeleza Kiswahili nchini humo. Aidha, katika kutekeleza azma ya Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kukuza Kiswahili kimataifa, BAKITA limeandaa na kusambaza vitabu vya ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili katika nchi mbalimbali duniani. Pia, BAKITA liligawa vitabu kwa balozi 50 za Tanzania nje ya nchi ambapo kila ubalozi ulipewa vitabu 32 na vitabu vyote kwa ujumla wake viligharimu shilingi milioni 30. Vilevile, Baraza lilitembelea na kufanya mazungumzo ya uraghibishi na kushajiisha nia ya mmiliki wa *Good Hope Junior School* nchini Zimbabwe ya kutaka kuanzisha somo la Kiswahili na liliwakabidhi vitabu 50 vya kufundisha na kujifunzia Kiswahili ukiwamo *Mwongozo wa Taifa wa Ufundishaji wa Kiswahili kwa Wageni.*




*Balozi wa Tanzania nchini Ujerumani Dkt. Abdallah Possi (kulia) akikabidhi cheti cha utambuzi wa Klabu ya Kijiwe cha Kiswahili nchini Ujerumani mwezi Novemba, 2023.*

**36.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha hakuna nchi inayoachwa nyuma kwenye harakati za kitaifa za kukisambaza Kiswahili, BAKITA limeendesha darasa la kwanza la Kiswahili kwa walimu 49 nchini Malawi mwezi Novemba, 2022 na walimu 38 nchini Burundi mwezi Desemba, 2022. Mafunzo haya yamejenga hamasa kubwa na kusababisha walimu wa Kiswahili katika nchi

hizo kuhitaji mwendelezo wa mafunzo hayo. Kutokana na vuguvugu hilo, walimu wa Burundi wameanza harakati za kuundwa kwa baraza litakalosimamia maendeleo ya Kiswahili nchini humo kutokana na hamasa waliyoipata. Aidha, BAKITA lilishirikiana na ubalozi wa Nigeria kufanikisha darasa la Kiswahili la Waandishi wa Habari 27 wa *Voice of Nigeria (VON)* mwishomi mwa mwezi Mei, 2023. Pia, Shirika hili limeanzisha ushirikiano wa kubadilishana wataalamu na Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC).




*Uongozi wa Chuo Kikuu cha Hebron nchini Malawi na baadhi ya wanafunzi wa Kiswahili wakiwa katika picha ya pamoja na Walimu wa Baraza la Kiswahili la Taifa Bi. Wema Msigwa (wa nne kutoka kushoto - waliokaa) na Onni Sigalla (wa tatu kutoka kulia - waliokaa) wakati wa Mafunzo ya Kiswahili kwa Wageni yaliyoendeshwa na BAKITA.*

**37.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Mei, 2023, BAKITA liliandaa na kurusha hewani jumla ya vipindi 891 kupitia redio na televisheni za Redio One, TBC-Taifa, TBC1, Clouds Fm, Kiss FM, U-FM, WAPO Redio, MVIWATA FM na Idhaa ya Kiswahili ya Redio ya Umoja wa Mataifa. Vipindi hivi vililenga kuelimisha jamii kuzingatia matumizi fasaha na sanifu ya Kiswahili. Aidha, BAKITA liliandaa makala 49 zilizochapishwa katika gazeti la HabariLeo toleo la kila siku ya Ijumaa. Vilevile, BAKITA lilitoa jarida la mtandaoni mara 7. Jarida hili linajulikana kama Lugha ya Taifa na linatoka mara moja kwa mwezi. Fauka ya hayo, Baraza lilirusha maudhui mbalimbali yanayohusu sarufi na fasihi ya Kiswahili kupitia akaunti zake za mitandao ya kijamii ikiwemo; Twitter, Facebook, Instagram na channeli ya Youtube. (Facebook- bakitatz, Istagram - bakita_tz na Twitter– bakita_tz, Youtube – Kiswahili TV). Maudhui haya yamefanya BAKITA liwe na takribani wafuasi 64,000 wa akaunti zake kwa ajili ya kujifunza lugha na kujenga ulumbi wa lugha.

*Baadhi ya Nembo za Vyombo vya Habari vilivyotumika kurusha hewani Vipindi vya kuelimisha jamii kuzingatia matumizi fasaha na sanifu ya Kiswahili.*

**38.** ***Mheshimiwa Spika,*** ufundishaji wa Lugha ya Kiswahili kwa wageni ni sehemu ya utekelezaji wa *Mkakati wa Taifa wa Kubidhaisha Kiswahili*. Katika kipindi hiki, BAKITA lilitoa mafunzo kwa diaspora 42 katika nchi za Falme za Kiarabu za Abu Dhabi na Dubai, diaspora 14 katika nchi ya Italia, diaspora 28 katika nchi ya Uholanzi, diaspora 23 katika nchi ya Zimbabwe na diaspora kumi (10) nchini Nigeria. Mafunzo haya pia yanaendelea nchini Rwanda kuanzia tarehe 5 – 9 mwezi Juni, 2023 kwa wanafunzi 324 na mpango wa BAKITA ni kufikia balozi zote. Malengo ya mafunzo hayo ni kufanya diaspora wawe na uwezo wa kufundisha Kiswahili kama lugha ya kigeni kupitia vituo vilivyoanzishwa na balozi za Tanzania katika kutekeleza agizo la Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.)

na pia kufungua vituo kwa kuiga mfano wa Watanzania watatu wanaoishi nchini Zimbabwe waliofungua kituo cha Kiswahili na Utamaduni katika jimbo la Bulawayo. Fauka ya hayo, BAKITA lilitoa mafunzo ndani ya nchi kwa walimu 288 sawa na ongezeko la asilimia 476 ya lengo la kufundisha walimu 50 wa kufundisha wageni. Ongezeko hilo limetokana na mbinu iliyobuniwa na BAKITA ya kutoa mafunzo hayo kwa wanafunzi wanaohitimu vyuo vikuu na lilianza kwa kuendesha kozi hiyo kwa wanafunzi 200 wa Chuo Kikuu cha Dodoma na waliobaki 88 ni wale waliofundishwa kupitia kituo cha Makao Makuu cha Ofisi za BAKITA. Utaratibu huo utaendelezwa kwa vyuo vyote vinavyotoa shahada za Kiswahili nchini. Manufaa ya mafunzo haya ni kujenga uwezo wa nchi wa kuteka soko la Kiswahili ndani na nje ya nchi na kubaini wahitimu wa Kiswahili kwa kila mwaka kupitia vyuo vikuu nchini.



*Moja ya darasa la mafunzo ya kuimarisha stadi za kufundisha Kiswahili kwa wageni kwa wahitimu wa Chuo Kikuu cha Dodoma yaliyofanyika mwezi Julai, 2022.*

**39.** ***Mheshimiwa Spika,*** hali kadhalika, BAKITA katika kuimarisha Kiswahili kimataifa limeendelea na mradi wake wa kuunda kongoo ya Kiswahili ambapo kwa sasa kongoo hiyo ina jumla ya maneno 29,000,000 kati ya maneno 50,000,000 yanayotarajiwa, sawa na asilimia 58 ya malengo yake. Kongoo hili likikamilika litakuwa na manufaa makubwa katika uendelezaji wa lugha kiteknolojia na kuimarisha data ya uhifadhi wa lugha. Aidha, wataalamu na watu mbalimbali watakuwa na uwezo wa kulitumia kongoo hili kwa shughuli za uandishi wa kamusi, ujifunzaji wa Kiswahili na uandishi wa vitabu.

**40.** ***Mheshimiwa Spika,*** BAKITA lilitafsiri jumla ya kazi kubwa na ndogo 954. Pia, BAKITA lilithibitisha tafsiri 2,452 zilizofanywa na Mawakala wake. BAKITA lilitoa huduma ya tafsiri na ukalimani katika mikutano miwili ya Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu huko Banjul, Gambia. Aidha, BAKITA liliratibu huduma ya ukalimani katika mikutano mbalimbali ikiwemo; Mkutano wa Tatu wa Dharura wa Baraza la Mawaziri la *Afican Diamond Producers Association* (ADPA), ulioandaliwa na Chama cha Wazalishaji Almasi Afrika uliofanyika Arusha, Tanzania mwezi Oktoba, 2022; Mkutano wa Baraza la Utendaji na Uratibu wa nne (4) wa nusu mwaka wa Umoja wa Afrika (AU) na *Regional Economic Communities* (RECs) uliofanyika Lusaka, Zambia mwezi Julai, 2022; Mkutano wa Bunge la Afrika uliofanyika Midrand, Afrika Kusini mwezi Agosti, 2022; Mkutano wa 18 wa Chama cha Wazalisha Pamba Afrika 2022 ulioandaliwa na Chama cha Wazalishaji Pamba Afrika uliofanyika Jijini Mwanza, Tanzania mwezi Agosti, 2022; Mkutano wa 8 wa Kamati ya Uendeshaji ya *African Flight Procedure Programme* (AFPP), ulioandaliwa na International Civil Aviation uliofanyika Dar es Salaam, Tanzania mwezi Oktoba, 2022; Mkutano wa kwanza wa Bunge la Sita la *Pan African*

*Parliament* (PAP) uliofanyika Midrand Afrika Kusini mwezi Novemba, 2022; Mkutano wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika ya Haki za Binadamu na Watu uliofanyika Banjul, Gambia mwezi Oktoba, 2022; Mkutano wa Uanuwai wa Viwanda na Uchumi uliofanyika Desemba, 2022, Jijini Dar es Salaam; Mkutano wa Wataalamu wa Methodolojia ya Rushwa, ulioandaliwa na Bodi ya Ushauri dhidi ya Rushwa ya Umoja wa Afrika uliofanyika Zanzibar, Tanzania mwezi Julai, 2022; Mkutano wa Baraza la Michezo la Umoja wa Afrika Kanda ya IV uliofanyika Arusha tarehe 2-4 Mei, 2023, Kikao cha Kawaida cha 75 cha Kamisheni ya Haki za Binadamu na Watu uliofanyika Banjul, Gambia tarehe 3 -13 Mei, 2023 na Mkutano wa Umoja wa Afrika uliofanyika Addis Ababa Ethiopia mwezi Februari, 2023.




*Wakalimani wa Kiswahili - Kiingereza Bw. Petro Basil Mswahili na Amos Mjemah wakiwa katika chumba cha kutolea huduma ya Ukalimani wakati wa kikao cha Mkutano wa Feed The Future - USAID kilichofanyika Morena Hotel tarehe 11 Mei, 2023.*

**41.** ***Mheshimiwa Spika,*** BAKITA lilitambua Vituo vitatu (3) vya kufundisha Kiswahili kwa wageni vikiwemo Kituo cha KKKT Shule ya Lugha Morogoro; Kijiwe cha Kiswahili cha nchini Ujerumani; Kituo cha Kiswahili na Utamaduni kilichopo Bulawayo nchini Zimbabwe na hivyo kuwa na jumla ya vituo 31 ambapo kati ya vituo, vituo 10 vilianzishwa kupitia balozi za Korea Kusini, Nigeria, Ufaransa, Italia, Sudani, Mauritius, Uholanzi, Havana, Abu Dhabi na

Zimbabwe; na vituo 21 ni vituo vilivyo nje ya balozi ambavyo kati yake vituo 16 viko nchini na vitano (5) viko katika nchi za Afrika Kusini, Ethiopia, Italia, Zimbabwe na Ujerumani, (***Kiambatisho Na.1).*** Fauka ya hayo, BAKITA limefanya utafiti na kubaini jumla ya vituo na vyuo 150 vinavyofundisha Kiswahili nje ya nchi na Watanzania zaidi ya 95 wanafanya kazi kupitia Kiswahili na taaluma zake husianifu huko ughaibuni.



*Baadhi ya Wanafunzi wageni wakihudhuria mafunzo ya lugha ya Kiswahili katika darasa la Kiswahili katika Kituo cha lugha cha KKKT kilichopo mkoani Morogoro mwezi Februari, 2023.*

**42.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza jitihada za Serikali za kuongeza idadi ya wakalimani, BAKITA liliendesha mafunzo kwa Wakalimani wa lugha za Kiarabu, Kifaransa na Kiingereza. Aidha, kwa sasa kanzidata ya wakalimani ina wataalamu 118 wa fani hiyo ambapo 25 ni wakongwe katika tasnia na 93 ni wapya ambao walipatiwa mafunzo baada ya Serikali kununua vifaa vya kisasa vya ukalimani. Vilevile, BAKITA lilihariri na kutoa ithibati kwa vitabu 94 na Moduli saba (7) za ujifunzaji na ufundishaji kwa madarasa ya awali. Vitabu hivi viliwasilishwa na Taasisi ya Elimu Tanzania, Shirika la *Room to Read* na wachapishaji na waandishi binafsi.



*Baadhi ya Wakalimani wakifuatilia darasa la Msasa kwa vitendo katika Ukumbi wa kutolea Mafunzo hayo wenye vifaa vya kisasa uliopo BAKITA. Mafunzo hayo yalitolewa Mwezi Agosti, 2022.*

### 3.2.1.3 KITUO CHA URITHI WA UKOMBOZI WA BARA LA AFRIKA

**43.** ***Mheshimiwa Spika,*** heshima ya Taifa letu katika diplomasia, utu, uzalendo, umoja, maadili na utangamano chanzo chake kikubwa ni mchango wa Tanzania katika kuzikomboa nchi za Afrika hususan kusini mwa Bara la Afrika. Tanzania ni nchi pekee ya Afrika iliyoanza kupokea wapigania uhuru wa nchi mbalimbali za Afrika, licha ya vitisho na udhalimu wa kikoloni,

Tanzania ilisimama na Afrika. Hili linajidhihirisha katika wimbo wa Taifa la Tanzania na Mwenge wa Uhuru. Kutokana na jukumu kubwa tulilolibeba kwa miaka 31 (1963-1994), mnamo mwaka 2011, Umoja wa Afrika, uliridhia kuipa heshima Tanzania ya kuanzisha na kuwa Makao Makuu ya Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika, ambapo iliwekwa chini ya usimamizi wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo.

**44.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika kimetekeleza majukumu yafuatayo: kukarabati jengo la yaliyokuwa Makao Makuu ya Ofisi ya Kamati ya Ukombozi ya OAU ambapo ukarabati wa jengo hilo umefikia asilimia 95.




*Jengo lililokarabatiwa na Serikali lililopo Jijini Dar es Salaam ambalo lilitumiwa na Kamati ya Ukombozi ya OAU kuanzia mwaka 1963-1994.*

**45.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa maeneo yenye historia ya ukombozi wa Afrika yanahifadhiwa, kuenziwa na kutangazwa, Kituo cha urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika kwa kushirikiana na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kimeyatambua jumla ya maeneo 260 na kuweka mabango 80 ya kuyaelezea na kuyatangaza maeneo hayo katika Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Mbeya, Mtwara, Ruvuma, Pwani, Morogoro na Lindi kwa upande wa Tanzania Bara na Zanzibar ikiwa ni sehemu ya kuyarasimisha kuwa urithi wa Taifa ili kuyalinda kisheria. Aidha, Kituo cha Urithi wa Ukombozi kimefanikiwa kukusanya nyaraka mbalimbali zilizotumika wakati wa harakati za ukombozi zipatazo 22,770; maktaba hai walioshiriki au kushuhudia harakati za ukombozi 284 wamehojiwa na kurekodiwa; vifaa mbalimbali kama pikipiki, toi la moyo, mhuri, sufuria, taipureta, sanduku la huduma ya kwanza viti na meza vilivyotumika wakati wa harakati za ukombozi 42 vimekusanywa; na elimu kwa umma kuhusu masuala ya harakati za ukombozi imetolewa kwa zaidi ya watu 500,000.

**46.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuunga mkono jitihada za Serikali za kukuza utalii

nchini, Kituo cha Urithi wa Ukombozi kimeanzisha utalii wa maeneo ya kiukombozi yaliyotumiwa na wapigania uhuru wa nchi za Kusini mwa Afrika ambapo kwa mwaka 2022/23 zaidi ya watalii 60,152 walitembelea maeneo hayo. Kati ya watalii hao, watalii zaidi ya 152 walitoka nje ya nchi na zaidi ya watalii 60,000 walitoka ndani ya nchi na maeneo waliyotembelea ni pamoja na Mazimbu na Dakawa - Morogoro; Kongwa -Dodoma; Masonya - Ruvuma; Farm 17 – Lindi; na Kituo cha Ukombozi – Dar es salaam. Aidha, Kituo cha Urithi wa Ukombozi kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii kimeratibu hatua za kutangazwa katika Gazeti la Serikali maeneo ya Urithi wa Ukombozi 15 ambapo kwa sasa yapo katika hatua za mwisho za kutangazwa. Lengo ni maeneo hayo kuwa Urithi wa Taifa na ili yaweze kulindwa, kutunzwa na kuwa kivutio cha utalii. Baadhi ya maeneo yanayotarajiwa kutangazwa ni Kongwa, jengo lililotumiwa na Kamati ya Ukombozi ya OAU, Dakawa, Mazimbu, Masonya na Kaole.

**47.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika licha ya kupokea watalii mbalimbali kimekuwa pia kikitembelewa

na Viongozi mbalimbali waliohusika na mapambano ya ukombozi wa Bara la Afrika. Mfano mzuri tarehe 14 Aprili, 2023 Rais mstaafu wa Jamhuri ya Msumbiji wa Awamu ya Pili Mheshimiwa Joacquim Chissano alitembelea eneo la makumbusho hayo na kusimulia namna walivyokuwa wakipokea misaada na mikakati ya kujikomboa kupitia Kamati ya Ukombozi ya OAU iliyokuwa na Makao Makuu yake nchini Tanzania. Pia, alitoa heshima kwa Baba wa Taifa Mwl. Julius K. Nyerere kwa kukubali Kamati ya Ukombozi ya Afrika kutekeleza majukumu yake katika eneo hilo.



*Rais mstaafu wa Jamhuri ya Msumbiji wa Awamu ya Pili, Mhe. Joacquim Chissano (kulia) na Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Balozi Dkt. Pindi H. Chana (Mb.) wakiangalia kumbukumbu za historia ya ukombozi alipotembelea Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Afrika tarehe 14 Aprili, 2023 Jijini Dar es Salaam.*

**48.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha historia hii inarithishwa kwa kizazi kijacho, Wizara imeshirikiana na Wizara ya Elimu kupitia Taasisi ya Elimu kuhakikisha uhuishaji wa mitaala ya kufundishia wanafunzi unaingiza maudhui ya historia ya Tanzania katika ukombozi wa Bara la Afrika. Aidha, Kituo kwa kushirikiana na wadau kimeendelea na zoezi la kusambaza juzuu 9 za Hashim Mbita zinazoelezea Harakati za Ukombozi wa Bara la Afrika ikiwa ni utekelezaji wa maelekezo ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC). Tayari Wizara imetafsiri juzuu 2 kwa lugha ya Kiswahili na hatua iliyobaki ni kushirikiana na Wizara ya Elimu ili vitabu hivyo viwe sehemu ya vitabu vya ziada kwa wanafunzi.

### 3.2.1.4 MFUKO WA UTAMADUNI NA SANAA TANZANIA

**49.** ***Mheshimiwa Spika****,* Maendeleo ya Utamaduni na Sanaa ni hali ya kuwapo kwa ongezeko la ushiriki wa watu katika shughuli za Utamaduni na Sanaa pamoja na kuimarika kwa ubora wa kazi za sekta hizo. Faida au manufaa yatokanayo na shughuli hizo ni pamoja na kukua kwa uchumi wa wasanii binafsi na Taifa kwa ujumla sambamba na kuimarika kwa maadili ya

jamii. Aidha, maendeleo hayo yanajipambanua katika nyanja mbalimbali zikiwemo ongezeko la idadi au wingi wa watu wanaojitokeza kushiriki katika shughuli mbalimbali za Utamaduni na Sanaa, wingi wa makundi yanayojumuishwa katika shughuli za Utamaduni na Sanaa kwa kuzingatia hali zao kama vile watu wenye ulemavu, watoto, jinsia na umri, namna Serikali na wadau wengine wa utamaduni na sanaa wanavyowasaidia watu kupata fedha za mitaji na kujiendeleza ili kukuza uwezo wao na kufikia viwango vinavyokubalika kitaifa na kimataifa katika fani husika.

**50.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na umuhimu wa uzingatiaji wa maendeleo ya Utamaduni na Sanaa, Serikali imechukua jitihada za makusudi za kuhuisha Mfuko wa Utamaduni na Sanaa tarehe 30 Septemba, 2020 kwa lengo la kukuza na kuendeleza Sekta ya Utamaduni na Sanaa kupitia utoaji wa mitaji yenye masharti nafuu na mafunzo ili kuziwezesha kazi za wadau katika Sekta hizi kukidhi vigezo vya mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi. Mfuko huu unatoa huduma katika maeneo ya urithi wa utamaduni, matumizi ya lugha na fasihi, sanaa za maonesho, sanaa za

ufundi, utengenezaji wa filamu na makala, muziki, uandishi wa vitabu vya kukuza lugha ya Kiswahili, na miradi mingine ya kukuza Utamaduni, Sanaa na Maadili. Aidha, walengwa wa Mfuko ni watu binafsi, vikundi, vyama, mashirikisho, vituo vya elimu na mafunzo, asasi za kiraia na taasisi zinazojishughulisha na kazi za kukuza na kuendeleza kazi za Utamaduni na Sanaa.

**51.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Aprili, 2023, Mfuko ulipokea maombi ya mikopo yenye thamani ya Shilingi 9,262,096,578 kutoka kwa waombaji 219. Hadi kufikia tarehe Aprili, 2023 Mfuko umefanikiwa kutoa mikopo yenye thamani ya Shilingi 1,077,000,000 kwa miradi 45 kutoka katika maeneo mbalimbali ya Sekta ya Utamaduni na Sanaa. Kutolewa kwa mitaji kwa miradi michache kumetokana na sababu mbalimbali ikiwemo waombaji kutorasimisha miradi yao, kutokuwa na uelewa wa uandishi wa miradi, kutokuwa na kumbukumbu za mapato na matumizi, kutokuwa na elimu ya fedha, usimamizi mbovu wa miradi, kutokuwa na elimu ya uwekezaji, kutokuwa na uhakika wa masoko ya kazi walizoziombea mitaji n.k.

**52.** ***Mheshimiwa Spika***, katika miradi 45 iliyowezeshwa, maeneo ya sekta yaliyowezeshwa na idadi yake katika mabano pamoja na thamani ya fedha iliyotolewa ni Filamu (miradi 17) iliyowezeshwa Shilingi 475,000,000; Muziki (miradi 14) iliyowezeshwa Shilingi 287,000,000; Sanaa za Ufundi (miradi 5) iliyowezeshwa Shilingi 105,000,000; Sanaa za Maonesho (miradi 3) iliyowezeshwa shilingi 30,000,000; na Sanaa ya Uandishi (mradi 1) uliowezeshwa Shilingi 10,000,000. Miradi hii imetoka katika mikoa saba (7) ambayo ni Dar es Salaam, Dodoma, Mara, Iringa, Mwanza, Mtwara na Mbeya.

**53.** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia miradi 45 ya Utamaduni na Sanaa kwa kipindi kilichotajwa kumekuwa na mafanikio mbalimbali yaliyofikiwa. Miongoni mwa hayo ni uboreshaji wa Studio 21 zilizowezeshwa ikiwemo kununua vifaa vya kisasa vitakavyoweza kuzalisha kazi zenye ubora unaotakiwa. Kuwapo kwa Studio hizi umekuwa ni mkombozi kwa wasanii kwa kuwaondolea usumbufu na gharama za kusafiri nje ya nchi kwa ajili ya kutafuta sehemu za kuzalisha kazi zao. Mfuko umefanikisha ununuzi wa vitendea kazi kwa vyuo vitano (5) vinavyozalisha wadau wapya wa Utamaduni na Sanaa katika nyanja

mbalimbali hususan U-DJ, mapambo, uibuaji wa vipaji vya uimbaji, urembo, mitindo, mapambo, upishi wa vyakula vya asili n.k. Vyuo vilivyowezeshwa ni Simba Scratch Academy, Koshuma Training Institute and Co., Mwanamboka Ujuzi-HUB, Dage School of Dressing, na AM Fashion. Vyuo hivi vinazalisha wadau wapya 332 kwa mwezi mmoja wanaojishughulisha na kazi za Utamaduni na Sanaa. Aidha, Mfuko umewezesha uandishi wa miswada 12 ya filamu na tamthilia, uzalishaji wa filamu mbalimbali kama vile JERAHA, LOLITA, REHANI, KICHUGUU, ANU, ASILI YETU n.k. zinazorushwa na zinazotegemewa kurushwa katika vituo mbalimbali vya redio na luninga nchini.

**54.** ***Mheshimiwa Spika***, jumla ya ajira 21,579 zimetengenezwa na miongoni mwa ajira hizo, ajira za kudumu ni 733 na ajira za muda ni 20,846. Aidha, Mfuko umekuwa kichocheo kikubwa kwa wadau katika eneo la urasimishaji kwani umewahamasisha kurasimisha shughuli zao katika mamlaka mbalimbali kama vile Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Halmashauri pamoja na mamlaka nyingine za

udhibiti ili waweze kuendesha shughuli zao kibiashara.

**55.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa umuhimu wa mikopo hii na ili kupata njia iliyo rahisi ya kuwafikia wajasiriamali wengi wa sekta za Wizara hii, Wizara kupitia Mfuko wa Utamaduni na Sanaa ipo katika hatua za mwisho za kuingia mkataba wa utoaji wa mikopo kupitia benki ya NBC. Kwa kuwa benki hii ipo katika mikoa yote ya Tanzania Bara ni imani ya Serikali itasaidia kufikisha huduma hii kwa walengwa katika mikoa yote badala ya hivi sasa ambapo imetolewa kwa mikoa michache.

**56.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa wadau wa Utamaduni na Sanaa wanakidhi vigezo, kutumia mitaji katika madhumuni yaliyokusudiwa, wanasimamia miradi yao kitaalamu ili iweze kuwa na tija, hadi kufikia mwezi Aprili, 2023, Mfuko umetoa mafunzo kwa wadau wa tasnia 4,534 kati ya hao wanawake walikuwa 1,896 na wanaume 2,638. Mafunzo yaliyotolewa yalihusisha mada mbalimbali miongoni mwa hizo ni elimu ya fedha, utunzaji wa kumbukumbu, uandishi wa miradi, urasimishaji wa kazi za Sanaa, usimamizi na

uendeshaji wa miradi, uwekezaji, kuutambua mnyororo wa thamani wa kazi za Utamaduni na Sanaa na kujitambua. Mafunzo haya yamefanyika kwa awamu ya kwanza katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma na Pwani. Aidha, mipango ya kuwafikia wadau wengine katika mikoa yote ya Tanzania Bara inafanyika kwa lengo la kuwafikia wadau 6,000 kwa mwaka 2023/24.

### 3.2.2 SEKTA YA SANAA

#### 3.2.2.1 IDARA YA MAENDELEO YA SANAA

**57.** ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Maendeleo ya Sanaa ni eneo jingine muhimu katika maendeleo ya nchi yetu na inahusisha Idara ya Maendeleo ya Sanaa, Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), Bodi ya Filamu na Michezo ya Kuigiza (TFB), Taasisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA) na Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa).

**58.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha Sanaa inatumika ipasavyo kulitangaza Taifa kimataifa, Serikali kwa kushirikiana na BASATA, Kituo cha Sanaa na Utamaduni kwa Viziwi

Tanzania (KISUVITA) na *International Deaf Cultural Arts Inc. (IDCA)* yenye Makao Makuu yake Nevada, Marekani iliandaa na kuendesha kwa mafanikio makubwa Shindano la Kimataifa la Urembo na Utanashati kwa viziwi *(Miss and Mr. Deaf International – MMDI, 2022)* kuanzia tarehe 23 – 31 Oktoba, 2022. Ikiwa ni mara ya kwanza kabisa Barani Afrika, mashindano haya yalifanyika katika Ukumbi wa Selous katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Mwl. Julius Nyerere *(Julius Nyerere International Convention Centre - JNICC)* Jijini Dar es Salaam ambapo watu 147 kutoka nchi 43 duniani walishiriki na kwa taarifa za makusanyo ya kadi, watazamaji 1,478 walifika ukumbini kutoka ndani na nje ya nchi. Katika shindano hilo, Mtanzania Khadija Kanyama aliibuka binti ***mrembo*** zaidi kiziwi duniani na Mtanzania Russo Songoro aliibuka mwanamitindo bora zaidi wa kiume kiziwi duniani na Mtanzania mwingine Rajan Ally alishinda nafasi ya pili mwanaume mtanashati zaidi kiziwi duniani. Kupitia shindano hili, Tanzania ilitangazwa kimataifa kama nchi ya fursa kwa wote bila kujali changamoto za kimaumbile walizonazo wanadamu na tayari waandaaji wa mashindano haya wamewasilisha na kukubaliwa ombi la kufanyika tena kwa

mashindano haya kati ya tarehe 15 Novemba, na tarehe 3 Desemba, 2023 kutokana na mafanikio makubwa ya mwaka 2022 na heshima kubwa waliyopewa na nchi yetu. Kupitia mashindano hayo, washindi walipata fursa ya kutembelea Hifadhi ya Ngorongoro kama sehemu ya kuutangaza utalii wetu. Kwa mwaka 2023, Wizara inalenga kutangaza zaidi maeneo mengine muhimu na maandalizi yameanza.




*Bi Khadija Kanyama: Mtanzania binti mrembo zaidi kiziwi duniani aliyeshinda katika mashindano ya Miss and Mr. Deaf International yaliyofanyika Jijini Dar es Salaam nchini Tanzania tarehe 23 – 31 Oktoba, 2022.*

**59.** ***Mheshimiwa Spika***, jukumu kubwa la Serikali ni kuhakikisha vijana wote nchini

wanapata fursa ya ajira na kuonesha vipaji vyao. Serikali kwa kushirikiana na BASATA na Asasi ya *The Music in Africa Foundation* imeratibu kufanyika kwa mara ya kwanza nchini Mkutano mkubwa wa wadau wa Muziki wa Afrika ujulikanao kama The Music in Africa Conference for collaboration, Exchange and Show Case (ACCES) uliofanyika kati ya tarehe 24 na 26 Novemba, 2022. Mkutano huo ulizileta nchini kampuni zinazojishughulisha na uzalishaji, uelimishaji, usambazaji, utumiaji na uratibu wa Muziki wa Afrika kama vile Tune core, Siemens stiftung, Goethe Institute, Sauti za Busara, Womex , Smille, Media, Sound na *Africa Ari Lines Ziiki Media, Boomplay, Sportfy, The Orchard, Samcom, IOMMA, Sound Connect Fund, Action Music Academy,* COSOTA, BASATA, MaDJ, waandaaji wa matamasha, mapromota, mawakala wa muziki, Mameneja wa wasanii, Lebo za kurekodi muziki, Watangazaji, Waandishi wa Habari za Muziki, sound engineers, wenye shule za kufundisha muziki, wafanyabiashara wa kazi za muziki, wadau na wanamuziki wenyewe.

**60.** ***Mheshimiwa Spika***, mkutano huu ulikuwa ni wa awamu ya Tano baada ya ule wa Dakar, Senegal uliofanyika mwaka 2017, Nairobi,

Kenya mwaka 2018, Accra, Ghana mwaka 2019, na Johannesburg, Afrika Kusini mwaka 2021 ambapo Wasanii wa Tanzania Barnaba, Sinaubi Zawose, Sholo Mwamba na Vitalis Maembe walitumbuiza sambamba na wanamuziki wenye ushawishi mkubwa kama vile Sampa the Great (Zambia), Mr. Eazi (Nigeria), Thandiswa Mazwai (Afrika Kusini), Sarkodie (Ghana), Banky W (Nigeria), Mulatu Astatke (Ethiopia), Baaba Maal (Senegal), Ebo Taylor (Ghana), Eric Wainaina (Kenya), Samini (Ghana), Cheick Lô (Senegal), Blinky Bill (Kenya) na Efya (Ghana). Kwa mujibu wa majumuisho ya Asasi zilizotajwa, wadau wapatao 1,120 kutoka nchi 45 ulimwenguni walishiriki na wadau hao wameuthaminisha mkutano huu kuwa wa mafanikio ya hali ya juu. Mafanikio katika maandalizi ya mkutano huu yameifanya Tanzania kuteuliwa mara ya pili kuwa mwenyeji wa Kongamano hili litakalofanyika tena tarehe 9 – 11 Novemba, 2023 hapa Nchini jambo ambalo halikuwahi kutokea huko nyuma nchi moja kuandaa mkutano huo miaka miwili mfululizo.

**61.** ***Mheshimiwa Spika***, kupitia Mkutano huo, washiriki mashuhuri waliandaliwa ziara ya kiutalii ili wanapoondoka nchini wabaki na

kumbukumbu ya Tanzania isiyofutika akilini mwao *(Tanzania: The Unfortgotable)*. Aidha, kupitia matukio kama haya, Tanzania sasa imeanza kuaminiwa na Asasi za Kimataifa kwa kuifanya nchi yetu kuombwa kuwa mwenyeji wa matukio makubwa duniani hasa upande wa Tuzo na ujenzi wa Akademia za muziki na filamu. Serikali inaendelea na majadiliano nao hasa kuhusu uwezeshaji wa kifedha katika matukio hayo.

**62.** ***Mheshimiwa Spika*** katika kuhakikisha Sekta ya Sanaa inakuzwa kuanzia ngazi ya chini na kurithishwa kwa watoto na vijana, Wizara kwa kushirikiana na BASATA iliratibu Mashindano ya Sanaa za Maonesho na Muziki wakati wa mashindano ya UMITASHUMTA na UMISSETA yaliyofanyika Mkoani Tabora ambapo kwa upande wa UMITASHUMTA yalifanyika kuanzia tarehe 31 Julai hadi 06 Agosti, 2022, ambapo wanafunzi wa shule za Msingi kutoka mikoa yote ishirini na nane (28) Tanzania Bara na Zanzibar walishiriki. Mashindano haya yalihusisha kwaya, ngoma na Muziki wa kizazi Kipya. Aidha, mashindano upande wa UMISSETA yalifanyika tarehe 09 hadi 19 Agosti, 2022 ambapo wanafunzi wa shule za Sekondari kutoka mikoa

25 Tanzania Bara na Kusini Unguja na kufanya jumla ya mikoa 26 kushiriki. Lengo la mashindano hayo ni kuibua na kukuza vipaji na kuviunganisha vipaji hivyo kwenye soko la ajira. Kwa mfano, baadhi ya washindi wa ngoma katika mashindano hayo walishiriki Tamasha la JAMAFEST nchini Burundi kama sehemu ya motisha ya ushindi walioupata. Sambamba na mashindano hayo, Wizara iliratibu ushiriki wa wananchi wa Tabora na viunga vyake ili kujionea vipaji vya vijana hao huku Wasanii hasa wa muziki wa Kizazi Kipya wakipenyeza ujumbe wa umuhimu wa michezo katika kujenga afya na manufaa ya kujitokeza kushiriki Sensa iliyofanyika mwezi Agosti, 2022 ikiwa ni sehemu ya programu pana ya Sensabika.

**63.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na BASATA iliratibu ushiriki wa Tanzania katika Tamasha lijulikanalo kama "Jumuiya ya Afrika Mashariki Utamaduni Festival" (JAMAFEST). Tamasha hilo huandaliwa kwa mzunguko miongoni mwa nchi wanachama kila baada ya miaka miwili. Kwa mwaka 2022 tamasha hili liliandaliwa na nchi ya Burundi na lilikuwa ni onesho la Tano tangu kuanzishwa kwake baada ya Rwanda (2013), Kenya (2015),

Uganda (2017) na Tanzania (2019). Wizara kwa kushirikiana na wadau wake iliratibu ushiriki wa Tanzania katika Tamasha hilo lililofanyika katika Jiji la Bujumbura kuanzia tarehe 04 hadi 12 Septemba, 2022 lililoongozwa na kaulimbiu isemayo "Kutumia Rasilimali za Utamaduni kukabiliana na Athari za UVIKO-19 kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki". Katika maonesho hayo, Tanzania ilipeleka wajasiliamali 65 na vikundi vya sanaa 13 ambavyo vilionesha kazi zao na kujipatia kipato, ikiwa ndiyo nchi ya kwanza iliyopeleka washiriki wengi zaidi baada ya mwenyeji Burundi.

**64.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo inaendelea na uratibu wa maandalizi ya ujenzi wa Sanamu ya Mwl. Nyerere inayotarajiwa kusimikwa Jijini Addis Ababa Ethiopia katika Makao Makuu ya Umoja wa Afrika ambapo hadi Aprili, 2023 hatua iliyofikiwa ni kuanza kwa ujenzi wa Sanamu halisi baada ya Mkandarasi, Kampuni ya EPITOME ARCHITECTS LIMITED ya Tanzania kukamilisha ujenzi wa sampuli kifani ya pili na kuridhiwa na Kamati ya Kitaifa kwa mujibu wa Sheria ya kuwaenzi Waasisi wa Taifa Na. 18 ya mwaka 2004 na Kanuni zake za mwaka

2005. Chimbuko la Mradi huo ni mapendekezo ya Hayati Robert Mugabe la mwaka 2015 yaliyolenga kutambua mchango uliotukuka wa Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere katika ukombozi wa Bara la Afrika hasa Mataifa yaliyo Kusini mwa Bara hilo. Mradi huo wenye thamani ya Dola za Marekani 205,942 unajengwa chini ya usimamizi wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Sekretarieti ya SADC, Mameneja Mradi kwa kushirikiana na familia ya Mwalimu Nyerere na kwa mujibu wa Mkataba uliopo, inatarajiwa kukamilika Desemba, 2023. Usimamizi wa Tanzania unalenga haswa kutimiza matakwa ya Kanuni ya 17 na 18 ya Kanuni za 2005 za Sheria ya Kuwaenzi Waasisi wa Taifa Na. 18 ya mwaka 2004 zinazoelekeza Sanamu inayojengwa kumuenzi mmoja wa Waasisi kufanana pasi na shaka na anayeenziwa.

**65.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara pia iliandaa Tamasha la kimataifa la Muziki wa Taarabu lililofanyika katika ufukwe wa Bahari ya Hindi (Coco Beach) tarehe 3 Julai, 2022. Tamasha hili lilijumuisha vikundi tisa (9) vya muziki wa Taarabu kutoka ndani ya nchi, wasanii binafsi

watano (5) na kikundi kimoja cha Taarabu kutoka nchini Burundi. Lengo la Tamasha hili lilikuwa kubainisha mchango wa muziki wa Taarabu katika kueneza lugha ya Kiswahili kuelekea Siku ya lugha hiyo duniani tarehe 7 Julai ya kila mwaka.




*Kikundi cha Taarabu kutoka nchini Burundi ambacho ni moja ya kikundi kilichotumbuiza katika Tamasha la Taarabu lililofanyika tarehe 03 Julai, 2022 katika ufukwe wa Bahari ya Hindi.*

**66.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea na mpango wake wa kuwapa fursa Wasanii wa Tanzania kuonesha vipaji vyao kupitia Tamasha la Serengeti Music Festival, ambalo kwa sasa linakwenda kufanyika Kimataifa. Tofauti na

miaka iliyopita, kwa mwaka 2022/23, Tamasha hili limeendeshwa kwa mtindo tofauti kwa kupeleka makundi ya Sanaa na Wasanii mmoja mmoja nje ya nchi kushiriki shughuli za Sanaa katika matukio makubwa yenye hadhi ya kimataifa. Kwa mfano, Kikundi cha *Safi Theatre* kimeshiriki Maadhimisho ya Miaka 60 ya Umoja wa Afrika katika eneo la Cradle of Humankind, Johannesburg wakati kikundi cha Singeli cha Sholo Mwamba kikishiriki Tamasha la African Music Days ukumbi wa Muffathalle, Munich katika maadhimisho ya miaka 60 ya Umoja wa Afrika kati ya tarehe 24 - 25 Mei, 2023. Kikundi hicho hicho pia kimeshiriki Tamasha linaloandaliwa kila mwaka na *Asasi ya The Africa We Want e.V* la *German Pan-African Expo* nchini Ujerumani lililofanyika tarehe 1 - 4 Juni, 2023 mjini Tübingen. Katika matamasha hayo, Singeli imeonekana kukonga nyoyo za wazungu wengi na imetia fora kwa kufuatiliwa kwa kiasi kikubwa ndani na nje ya nchi. Vilevile, Msanii wa Vichekesho Mujuni Sylivery Bajwauka (Mpoki) ameshiriki kama MC katika matukio ya Siku ya Tanzania na Siku ya Kiswahili yaliyoandaliwa na Ubalozi wa Tanzania nchini Uingereza na kufanyika tarehe 3 Juni, 2023 Jijini London.

### 3.2.2.2 BARAZA LA SANAA LA TAIFA (BASATA)

**67.** ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu ya Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) ni pamoja na kukuza na kuendeleza sanaa nchini; kufanya tafiti za fursa za masoko na masuala mbalimbali yanayohusu sanaa; kuandaa Kanuni za kusimamia ubora wa kazi za Sanaa; na kuandaa na kuendesha maonesho, mashindano, matamasha na biashara za sanaa.

**68.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia BASATA imeendelea kukuza ubunifu na utengenezaji wa sanaa bora kwa lengo la kuwawezesha wasanii kuwa wabunifu na kubuni kazi za sanaa zilizo bora. BASATA liliendelea na mageuzi ya kiutendaji na kitaasisi ili kuwa mwezeshaji zaidi wa shughuli za sanaa badala ya kudhibiti. Hivyo, BASATA limeshiriki kuratibu kutatua migogoro ya wasanii kuhusu mikataba waliyoingia ambapo katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Aprili, 2023 zaidi ya migogoro mikubwa mitano (5) imetatuliwa. Pia, BASATA limekuwa likiwaita wasanii siyo tu pale kwenye upungufu bali hata pale wanapofanya vizuri na kuwapongeza. Sambamba na hatua hii, BASATA

limeendelea kutokimbilia kuwafungia wasanii kama ilivyokuwa awali bali kunapotokea changamoto zilizokithiri za kimaadili, kama alivyoagiza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa Tamasha la Usiku wa Msanii Joseph Mbilinyi.

**69.** ***Mheshimiwa Spika,*** BASATA limeendelea kuleta mageuzi ya kuboresha muziki wa kizazi kipya kwa kutengeneza Kivunge cha Mtozi yaani ***Producers' Kit*** chenye zaidi ya vionjo 400 vyenye ladha ya asili ya kitanzania. Vionjo hivi vilirekodiwa kutoka kwenye ngoma za makabila mbalimbali ya Tanzania. Matokeo ya Kivunge cha Mtozi ni kuchochea mageuzi ya kuwa na muziki wa kitanzania wenye midundo ya Taifa la Tanzania. Nawapongeza sana wanakamati.

**70.** ***Mheshimiwa Spika,*** BASATA limeendelea kuwawezesha wasanii nchini kwa kuwasajili na kutoa vibali kwa wasanii binafsi 1,188; vikundi 201; kumbi za sherehe, starehe na burudani 261; kampuni 94 na vibali vya matukio 24. Aidha, BASATA limetoa vibali 307 vya wasanii wa Tanzania kwenda nje ya nchi kufanya shughuli za sanaa pamoja na vibali 52 vya

wasanii wasiokuwa watanzania kuingia nchini kwa ajili ya kufanya shughuli za Sanaa. Aidha, BASATA limetoa vibali 64 kwa Taasisi vikiwemo vyama, mashirikisho Asasi zisizo za Kiserikali na Taasisi binafsi kujishughulisha na Sanaa. Hatua hii inasaidia BASATA kutambua wadau wake pamoja na shughuli wanazofanya na kuwasaidia kutambulika na kusaidiwa zaidi na mamlaka nyingine za ndani na nje ya nchi.

**71.** ***Mheshimiwa Spika,*** BASATA liliendesha warsha ya kuwajengea uwezo wasanii wa Tanzania katika kutumia fursa za kiteknolojia kupitia jukwaa la *Access Music*. Kwa kushirikiana na Shirika lisilo la Kiserikali la *Music in Africa* kutoka Afrika Kusini, liliwajengea uwezo wasanii 89 wa Tanzania katika kuziona fursa za kibiashara katika muziki ikiwemo matumizi ya fursa za kiteknolojia katika mitandao ya kijamii kuendesha kazi zao. Aidha, kwa kushirikiana na Kituo cha Sanaa cha Chamwino (Chamwino Art Center), limetoa mafunzo ya kuwajengea uwezo wasanii 38 kutoka katika vikundi 38 vya Sanaa wilayani Chamwino mkoani Dodoma. Mafunzo haya yalijikita katika masuala ya ubunifu katika kazi za Sanaa, Mikataba na masuala ya Hakimiliki, pamoja na

masuala ya usajili. Katika mafunzo hayo BASATA lilishiriki katika kutoa mada zilizotajwa hapo juu kwa kushirikiana na walimu 3 wa shule za msingi na Sekondari pamoja na wataalamu 2 kutoka Kituo cha Sanaa cha Chamwino.




*Wataalamu wa Music in Africa kutoka Afrika Kusini wakiendesha warsha kwa Wasanii wa Tanzania wa Muziki jijini Dar es Salaam tarehe 24 – 26 Novemba, 2022.*

**72.** ***Mheshimiwa Spika,*** ikiwa ni juhudi za kukuza na kuongeza ubora wa kazi za sanaa, Serikali kupitia Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) na TaSUBa limetoa mafunzo ya sanaa kwa wasanii 37 ambao vipaji vyao viliibuliwa kwenye mashindano mbalimbali ikiwemo *Bongo Star Search* (BSS 2021) – washiriki 5, *Taifa Challenge Cup and Music* - washiriki 26 pamoja na washindi 6 wa ***Miss and Mr. Deaf Africa.*** Mafunzo yalifanyika katika Chuo cha Sanaa na

Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) kuanzia tarehe 06 Agosti, 2022 hadi tarehe 03 Septemba, 2022. Mafunzo haya yalilenga kuwajengea uwezo katika fani ya uimbaji, utunzi na matumizi ya jukwaa.

**73.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha ushiriki wa BASATA na wasanii katika maonesho mbalimbali nchini, BASATA limeshiriki na kuratibu ushiriki wa Wasanii wa Sanaa za Ufundi katika Maonesho ya Sabasaba ya mwaka 2022 yaliyofanyika Dar es Salaam kuanzia tarehe 30 Juni hadi 13 Julai, 2022. Katika maonesho hayo, wasanii 24 wa Sanaa za Ufundi waliwezeshwa kuonesha bidhaa zao kupitia banda lililoandaliwa na BASATA. Vilevile, wasanii 364 walihamasishwa kushiriki maonesho ya Sabasaba katika mikoa ya Morogoro, Manyara, Tanga na Njombe. Aidha, BASATA lilihamasisha wasanii katika mikoa mingine kushiriki maonesho hayo ambapo jumla ya wasanii 364 walifanikiwa kuonesha bidhaa zao katika mikoa mbalimbali.

**74.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia BASATA imeendelea kuhamasisha jamii kushiriki katika shughuli za Sanaa. Katika kipindi cha

Julai, 2022 hadi Aprili, 2023 Baraza limewezesha kuanzishwa kwa Programu inayotambulika kwa jina la ***'Sanaa Mtaa kwa Mtaa'***. Lengo la programu hii ni kushirikisha na kuhamasisha jamii katika maeneo mbalimbali kuendesha shughuli za kukuza, kufufua na kuendeleza sanaa nchini na utekelezaji wake umefanyika katika Mkoa wa Pwani, Wilaya ya Rufiji tarehe 16 Oktoba, 2022. Jumla ya wasanii na wadau wa Sanaa zaidi ya 452 walishiriki na jumla ya mitaa 16 ilipitiwa. Na pia imefanyika katika Mkoa wa Arusha mjini tarehe 09 na Wilaya ya Karatu tarehe 10 Disemba, 2022 kwa kushirikiana na uongozi wa Jiji la Arusha na Wilaya ya Karatu ambapo jumla ya wasanii na wadau wa Sanaa 497 walishiriki.

**75.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia BASATA imekuwa ikiimarisha shughuli za Sanaa kupitia Taasisi mbalimbali za elimu ikiwemo Shule za Msingi na Sekondari. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Aprili, 2023 BASATA kwa kushirikiana na Taasisi ya *Kukaye Moto Cultural Center* lilitoa mafunzo ya Sanaa kwa watoto 120 kutoka shule 6 za Msingi za mikoa ya Dar es Salaam na Pwani. Mafunzo hayo yalihitimishwa kwa tamasha la watoto katika fani za ngoma,

utambaji wa hadithi, Maigizo, Sarakasi na Muziki. Aidha, kupitia mashindano ya UMISSETA na UMITASHUMTA 2022, BASATA limetoa mafunzo ya sanaa kwa wanafunzi ambapo mafunzo hayo yalijikita katika kufundisha namna bora ya kuendesha Sanaa za Maonesho hususan katika maeneo ya fani za maigizo, muziki na ngoma za asili. Jumla ya walimu 26 wa shule za Msingi na 26 wa Shule za Sekondari na wanafunzi 580 walipatiwa mafunzo hayo.

**76.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha utoaji wa taarifa na ushawishi kwa umma kuhusu masuala ya sanaa, BASATA limefanya ziara 21 katika Vituo vya Habari pamoja na kufanya Vikao 19 na waandishi wa Habari. Vile vile, BASATA limeendelea kutumia kurasa zake za mtandaoni za *Instagram* (basata.tanzania) na *Twitter* (Basata_Tanzania) kutoa elimu na taarifa mbalimbali kwa jamii kuhusiana na masuala ya sanaa. Katika kuhakikisha jamii inahabarishwa na kushauriwa katika masuala yahusuyo Sanaa, BASATA limeendesha midahalo minne (4) ya Sanaa mkoani Arusha na Kagera, lengo likiwa ni kuimarisha utendaji wa wasanii na wadau wa sanaa nchini. Katika midahalo hii, Jumla ya wasanii na wadau wa sanaa 302 walishiriki.



*Moja ya vikao vya Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) na Waandishi wa Habari kilichohusu kuimarisha utoaji wa taarifa na ushawishi kwa umma kuhusu masuala ya Sanaa kilichofanyika mkoani Dar es Salaam.*

**77.** ***Mheshimiwa Spika,*** BASATA limetoa ushauri kwa wasanii na wadau wa Sanaa wapatao 2,759 kutoka maeneo mbalimbali nchini. Ushauri huu ulitolewa katika maeneo ya masoko ya kazi za sanaa, uendeshaji wa matukio, utafutaji fedha kwa vikundi na Taasisi pamoja na masuala ya usajili na vibali. Ushauri huu ulitolewa kupitia vikao vya wadau, mawasiliano ya simu na mazungumzo ya wadau wanaotembelea Ofisi za BASATA.

**78.** ***Mheshimiwa Spika,*** BASATA liliendesha Kikao Kazi cha Maafisa Utamaduni kutoka Mikoa

26 ya Tanzania Bara, chenye lengo la kushirikisha jamii. Katika kuimarisha ushiriki wa mamlaka za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa katika kufufua, kukuza na kuendeleza sanaa nchini, BASATA limeendesha kikao kazi cha siku mbili cha Maafisa Utamaduni wa mikoa na Wilaya. Kikao kazi hiki kilifanyika mkoani Dodoma katika ukumbi wa African Dreams tarehe 26 na 27 Januari, 2023. Jumla ya Maafisa Utamaduni 143 walishiriki. Katika kikao kazi hicho mada mbalimbali zilijadiliwa ikiwa ni pamoja na; Mwongozo wa Uendeshaji wa Kamati za Sanaa za Mikoa na Wilaya, Mwongozo wa Uendeshaji wa Programu ya Sanaa ya Mtaa kwa Mtaa, Mwongozo wa Usimamizi wa Maadili katika Sekta ya Sanaa, Mapitio ya Kanuni za BASATA, matumizi ya Mfumo wa Kielektroniki wa Usajili (AMIS) pamoja na mada zingine kutoka katika Taasisi za COSOTA, Bodi ya Filamu, na Mfuko wa Fidia kwa Watumishi.

**79.** ***Mheshimiwa Spika,*** BASATA kwa kushirikiana na Taasisi ya Afrofest (Shirika lisilo la Kiserikali kutoka Kanada linalojishughulisha na kukuza Muziki wa Afrika nchini Kanada) waliwezesha mafunzo ya wasanii 4 kutoka Kanada na kundi la Mjomba Bendi inayoongozwa

na Mrisho Mpoto ambapo wasanii 8 walishiriki kwenye mafunzo hayo na kufanya maonesho ya pamoja katika Tamasha la Kimataifa la Utamaduni na Sanaa Bagamoyo mwezi Novemba, 2022. Kutokana na zoezi la kufanya maonesho kwa pamoja wasanii kutoka kundi la Mjomba Bendi chini ya uongozi wa Mrisho Mpoto na wasanii kutoka Kanada kila mmoja alijifunza kutoka kwa mwenzake na mwisho wa siku kila mmoja alijifunza.

**80.** ***Mheshimiwa Spika,*** ikiwa ni hatua ya kuhamasisha jamii kushiriki kikamilifu zoezi la Sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022, BASATA liliratibu tamasha kubwa lililotambulika kwa jina la Tamasha la SENSABIKA lililofanyika tarehe 21 Agosti, 2022 jijini Dar es Salam katika viwanja vya Leaders Club. Tamasha lilihusisha michezo mbalimbali na maonesho ya Sanaa za Maonesho, Ngoma, Muziki, Sanaa za Ufundi, na Filamu. Katika tamasha hili wasanii waliandaa kazi 107 zilizotumika kutoa elimu juu ya ushiriki wa wananchi katika zoezi la Sensa ya Watu na Makazi. Aidha, wasanii wapatao 442 walishiriki katika tamasha hilo.

**81.** ***Mheshimiwa Spika,*** BASATA limeendelea kutoa Tuzo za Muziki wa Tanzania

(TMA) kwa mara ya pili mfululizo. Tamasha la utoaji wa Tuzo hizi lilifanyika Dar es Salaam katika ukumbi wa Super Dome, Masaki Tarehe 29 Aprili, 2023. Utuoji wa Tuzo ulihusisha utoaji wa Tuzo maalumu zilizotolewa kwa Taasisi Nne (4) ambazo ni: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo cha Sanaa na Utamaduni Bagamoyo, Clouds Media Group na Sauti za Busara, Zanzibar. Lengo lilikuwa ni kutambua mchango wao wa kukuza tasnia ya muziki Tanzania. Tuzo ya Heshima ilitolewa kwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Awamu ya Nne (4). Aidha, Tuzo 52 zilitolewa kwa wasanii mbalimbali. Vilevile tukio la utoaji wa Tuzo hizi lilihudhuriwa na waalikwa wapatao 1,500. Fauka ya hayo jumla ya vyombo vya habari 46 vilishiriki usiku wa Tuzo hizo na kufanya matangazo mubashara ikiwemo Azam TV; Clouds TV na Digital; Global online TV; Mwananchi Digital; TVE na vyombo vingine vya habari na mitandao ya kijamii, ambapo inakadiriwa jumla ya watu 19,865,064 walifuatilia matangazo ya usiku wa Tuzo mubashara ndani na nje ya nchi.

**82.** ***Mheshimiwa Spika,*** BASATA likiwa kama msimamizi wa Sekta ya Sanaa nchini,

lilishiriki katika utoaji wa Tuzo za AFRIMMA nchini Marekani ambapo Watanzania 19 walishiriki na watano kati yao kushinda Tuzo hizo. Wasanii walioshinda Tuzo ni pamoja na Diamond Platnumz (Best Live Act), Rayvanny (Best Male East Africa), Zuchu (Best Female East Africa), Mrisho Mpoto (Best Traditional Artist) na Joel Lwaga (Best Gospel). Pamoja na malengo mengine, ushiriki huo ulilenga kujifunza na kupata uzoefu katika maandalizi na uendeshaji wa Tuzo za Sanaa kutoka katika mataifa mengine. Aidha, kupitia ushiriki huo, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alipewa Tuzo ya Heshima kama kiongozi mwenye kuleta mabadiliko na mapinduzi (Transformational Leader) katika kuendeleza Sekta ya Sanaa nchini Tanzania. Aidha, Baraza kwa kushirikiana na Taasisi ya Uni Media limeendesha shughuli ya utoaji wa Tuzo kwa wanafunzi wa Vyuo Vikuu nchini. Tuzo hizo zilitolewa tarehe 04 Desemba, 2022 jijini Dar es Salaam ambapo jumla ya Tuzo 31 zilitolewa kwa washindi waliopatikana. Katika kutoa Tuzo hizi Baraza lilidhamini kwa lengo la kukuza vipaji vyuoni na kuwapatia vijana mafunzo ya namna ya kuanzisha na kuratibu utoaji wa Tuzo.

**83.** ***Mheshimiwa Spika,*** BASATA limeanza kutumia mfumo wa Kielektroniki wa usajili na kutoa vibali kwa wasanii na wadau wa sanaa, lengo likiwa ni kuongeza makusanyo ya rasilimali fedha na kudhibiti mianya ya upotevu wa maduhuli ya Serikali pamoja na kuongeza ufanisi katika kuwahudumia wasanii na wadau wa sanaa nchini. Mfumo huu unafanya kazi sanjari na mifumo mingine ya Serikali. Katika kuhakikisha mfumo huu mpya wa kielektroniki wa usajili na vibali - AMIS unatambulika na kuweza kutumiwa na wasanii, BASATA limeendelea kutoa elimu na kuwajengea uwezo wasanii na wadau wa sanaa kuhusu matumizi ya Mfumo huu unaopatikana kwa kiungo cha https://sanaa.go.tz/.

**84.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, BASATA limeendelea kurejesha uhusiano baina yake na Taasisi zingine na Vituo vya Utamaduni vya Nchi za Umoja wa Ulaya na Marekani (Culture Development Partners) kwa kufanya vikao vya kuendeleza tasnia za Sanaa nchini. Aidha, BASATA limefanikiwa kuhuisha uanachama wake katika Shirikisho la Kimataifa la Mabaraza ya Sanaa na Utamaduni Duniani (IFACCA) ambapo kwa sasa Katibu Mtendaji wa BASATA

anakuwa Mjumbe na aliiwakilisha Tanzania katika Mkutano wa Shirikisho la Mabaraza hayo uliofanyika Mjini Stockholm Sweden kuanzia tarehe 1 hadi 5 Mei, 2023 ambapo ulihudhuriwa na zaidi ya viongozi 400 kutoka kila kona ya Dunia. Ajenda kubwa ya Mkutano huo ilikuwa ni kuimarisha uhusiano wa wasanii katika ubunifu wa kazi za Sanaa.




*Mkutano wa Shirikisho la Kimataifa la Mabaraza ya Sanaa na Utamaduni Duniani (IFACCA) ambao Katibu Mtendaji wa Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) ni Mjumbe na aliiwakilisha Tanzania katika Mkutano huo uliofanyika Mjini Stockholm Sweden tarehe 1 - 5 Mei, 2023.*

### 3.2.2.3 BODI YA FILAMU TANZANIA (TFB)

**85.** ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu ya Bodi ya Filamu ni pamoja na kusimamia na kuratibu

kazi za filamu ikiwemo kuhakiki na kuzipanga katika madaraja; kutoa vibali vya usambazaji, maonesho ya filamu, michezo ya kuigiza, kampuni za usambazaji wa filamu, kumbi za maonesho ya filamu, maktaba za picha za filamu, studio za uandaaji wa filamu; pamoja na kujenga uwezo wa wadau waliojiajiri/kuajiriwa katika tasnia ya filamu.

**86.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Bodi ya Filamu iliratibu uendeshaji wa Tamasha la Tuzo za Filamu na kutoa Tuzo kwa wadau waliofanya vizuri katika fani mbalimbali kwenye Tasnia ya Filamu ambapo kilele chake kilikuwa tarehe 17 Desemba, 2022 Jijini Arusha. Kupitia Tamasha hili, jumla ya Tuzo 45 zilitolewa kwa wadau wa filamu. Kati ya hizo, Tuzo 32 zilitolewa kwa washindi kwenye vipengele mbalimbali vilivyoshindaniwa, Tuzo 10 zilitolewa kwa wasanii/wadau wa filamu wakongwe, na Tuzo 3 zilitolewa kwa viongozi wa Serikali akiwemo Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutambua mchango wake katika kuilea na kuikuza Sekta ya Filamu nchini ikiwemo kufanikisha Tuzo hizo.



*Mshindi wa Tuzo ya kipengele cha Mwigizaji Bora wa Kike, Bi. Tunu Mwinyimbegu akikabidhiwa Tuzo hiyo na Mkurugenzi wa Maendeleo ya Filamu kutoka Bodi ya Filamu Tanzania, Bw. Emmanuel Ndumukwa katika kilele cha Tuzo za Filamu Tanzania za mwaka 2022 tarehe 17 Desemba, 2022 Jijini Arusha.*

**87.** ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi imeendelea kuratibu utoaji mafunzo ya kuwajengea uwezo wadau wa filamu kupitia pragramu zake mbalimbali za mafunzo. Kwa mfano, katika kipindi hiki, kumefanyika mafunzo yaliyotolewa kwa mtindo wa uchambuzi wa filamu ijulikanayo kama ***Film Screening and Criticism***, ambapo kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Aprili, 2023, wadau 297 wamenufaika kupitia uchambuzi wa jumla ya filamu 19. Aidha, kupitia Programu ya kuwaendeleza wasanii chipukizi ijulikanayo kama ***The Coming Film Star*** iliwajengea uwezo

wasanii chipukizi 60 katika masuala ya weledi, utawala wa fedha, pamoja na uwajibikaji. Pia, waandaaji wa filamu 16 walitembelewa katika maeneo yao ya kazi na kupata mafunzo kuhusu uboreshaji wa kazi za filamu. Vilevile, Bodi kwa kushirikiana na Chama cha Waigizaji Mkoa wa Morogoro iliandaa mafunzo yaliyotolewa kwa waigizaji 65 mkoani humo kupitia programu yake ya ***Taylor-made Training*** na kuwajengea uwezo katika fani ya uigizaji.

**88.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, katika kuendelea kuimarisha uwezo wa tasnia ya filamu katika uzalishaji wa filamu Bodi ya filamu imeingia makubaliano na Asasi ya Busan Foundation for International Cooporation (BFIC) ya nchini Korea Kusini yenye lengo la kuanzisha shule ya filamu (Film Academy) nchini itakayotoa mafunzo kwa wasanii na wadau wetu ili kuwawezesha kuandaa filamu zenye ubora na shindani kimataifa. Aidha, jopo la wataalamu watano lilikuja nchini kutoka Korea Kusini kwa lengo la kufanya upembuzi yakinifu na kujua mahitaji halisi ya uanzishwaji wa shule hiyo.

**89.** ***Mheshimiwa Spika,*** programu iitwayo *Mapping the Film Locations* yenye lengo la

kutangaza mandhari za kipekee za upigaji picha za filamu zipatikanazo hapa nchini kama vile mbuga za wanyama, hifadhi, milima pamoja na miundombinu ya kisasa ya nchi, imeendelea kutekelezwa ili kuvutia wacheza filamu kutoka nje ya nchi kuja kutengeneza filamu zao hapa nchini. Maeneo hayo yanatangazwa kupitia makala fupi ya filamu iliyowekwa kwa lugha za Kiswahili, Kiingereza, Kifaransa na Kihispania ili kuongeza wigo wa uelewa, na imesambazwa katika balozi 34 za Tanzania zilizopo katika nchi mbalimbali Duniani. Aidha, njia nyingine iliyotumika ni kupitia Taasisi mbalimbali, ikiwemo Kamisheni ya Filamu Nchini Namibia *(Namibia Film Commission)*, Kituo cha Utamaduni cha Irani *(Culture Center of Islamic Republic of Iran*), Chama cha Waendeshaji wa Biashara ya Utalii Tanzania *(Tanzania Association of Tour Operators),* Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) kupitia Safari Chaneli pamoja na mitandao ya kijamii ya Bodi.

**90.** ***Mheshimiwa Spika,*** kongamano (Symposium) la Wadau wa Filamu lililofanyika mwezi Desemba, 2022 Jijini Arusha liliandaliwa ikiwa ni mwendelezo wa jitihada za kuweka mazingira ya wadau wa filamu kujadili masuala

muhimu yanayohusu maendeleo ya Tasnia ya Filamu. Kongamano hilo lilihudhuriwa na wadau wa filamu takribani 200 na lilihusisha mijadala ya masuala mbalimbali ya tasnia ikiwemo fedha, mitaji na weledi katika uandaaji wa filamu. Aidha, vikao 2 vilivyoshirikisha viongozi wa Shirikisho la Filamu Tanzania (TAFF) vilifanyika, ambapo masuala mbalimbali yanayohusu uongozi na mipango ya kuendeleza Tasnia ya Filamu kupitia vyama vinavyounda Shirikisho hilo yalijadiliwa. Vilevile, Bodi iliwezesha maandalizi na kufanyika kwa Tuzo za Filamu kwa wanafunzi wa Vyuo Vikuu mbalimbali zijulikanazo kama UNI-AWARDS zilizotolewa tarehe 4 Desemba, 2022 jijini Dar es Salaam, ambapo jumla ya Tuzo 30 zilitolewa kwa wanafunzi hao.

**91.** ***Mheshimiwa Spika,*** mkakati maalumu wa kurudisha utamaduni wa kuonesha na kutazama filamu kwenye kumbi za sinema ikiwa ni hatua ya kuongeza na kuwezesha masoko ya filamu za Kitanzania na kuboresha mapato ya kazi za filamu umeendelea kufanyika. Kwa kutumia utaratibu huo filamu ya **The Green Tanzanite** ilizinduliwa na kuoneshwa katika ukumbi wa Mlimani City tarehe 21 Aprili, 2023

na Mheshimiwa. Balozi Dkt. Pindi H. Chana (Mb.), Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo ambapo watazamaji 222 walihudhuria. Vilevile, filamu nyingine zilizozinduliwa na kuoneshwa kupitia mkakati huu ni pamoja na filamu ya **Ugonjwa wa Kifo** iliyooneshwa eneo la wazi Tabata jijini Dar es salaam na filamu ya jina la **Dodoma** ambayo ilioneshwa katika ukumbi wa Mlimani City.

**92.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki Bodi imeweza kutoa leseni za uendeshaji wa shughuli za biashara za filamu na michezo ya kuigiza 180, ambayo ni sawa na asilimia 300 ya lengo la kutoa leseni 60 katika kipindi hicho. Leseni hizo zilitolewa ikiwa ni hatua za urasimishaji wa shughuli na biashara ya filamu nchini. Aidha, Vitambulisho 271 ambayo ni sawa na asilimia 22.6 ya lengo la vitambulisho 1,200 vilitolewa kwa wadau wanaojihusisha na shughuli za Filamu na Michezo ya Kuigiza.

**93.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki pekee jumla ya miswada na maombi 286 ya vibali vya kutayarisha filamu yamepokelewa na kuchambuliwa, ambapo kati yake, maombi 69 yalikuwa ya watayarishaji kutoka nje ya nchi, na

maombi 217 ni ya watayarishaji kutoka ndani ya nchi (Watanzania). Aidha, jumla ya filamu 1,109 zilihakikiwa na kupangiwa madaraja, sawa na asilimia 73.9 ya lengo la filamu 1,500 kwa mwaka mzima. Kati ya filamu hizo, filamu za ndani ya nchi zilikuwa 1,097 na za nje ya nchi zilikuwa 12.

**94.** ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi ya Filamu Tanzania iliendesha Operesheni 35 kati ya 36 sawa na asilimia 97.2 ya oparesheni zilizopangwa kufanyika kwa mwaka mzima katika maeneo mbalimbali ya jiji la Dar es Salaam na mikoa ya Tabora na Mwanza pamoja na mji wa Kahama mkoani Shinyanga. Operesheni hizo zilihusu ufuatiliaji wa vibali vya Bodi ya Filamu katika filamu zinazozalishwa na kusambazwa pamoja na kuwapo kwa ithibati za uendeshaji wa biashara za filamu zinazotolewa na Bodi ya Filamu. Aidha, hatua mbalimbali zimechukuliwa dhidi ya baadhi ya wadau wanaokiuka Sheria ikiwa ni pamoja na kuwaita wahusika ili watoe maelezo kuhusiana na uvunjifu wa Sheria pamoja na kuwaelimisha mambo ya kuzingatia wanapojihusisha na uzalishaji, usambazaji pamoja na biashara nyingine zinazohusisha kazi za filamu. Faida ya zoezi hili ni pamoja na kulinda haki za wamiliki

na walaji wa mazao ya filamu pamoja na kuongeza makusanyo ya mapato ya Serikali.

**95.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kupitia programu ya Sanaa Mtaa kwa Mtaa katika Tasnia ya Filamu, Bodi iliandaa mikutano na mafunzo kwa vitendo yaliyotolewa kwa wadau wa filamu na michezo ya kuigiza ambapo jumla ya wadau 750 waliweza kufikiwa na kupewa elimu kuhusu masuala yanayohusu filamu na michezo ya kuigiza katika mikoa 25 ya Tanzania Bara.

### 3.2.2.4 TAASISI YA HAKIMILIKI TANZANIA (COSOTA)

**96.** ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu ya Ofisi ya COSOTA ni pamoja na kukuza na kulinda maslahi ya watunzi, waandishi, wasanii, wafasiri, watayarishaji wa kurekodi sauti, watangazaji, na wachapishaji, kukusanya na kugawa mirabaha au ujira unaotolewa kulingana na haki zao zilizofafanuliwa katika Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Na. 7 ya Mwaka 1999. Ukusanyaji na ugawaji mirabaha ni kwa kipindi ambacho Kampuni Binafsi za Wasanii na wamiliki wa hakimiliki na hakishiriki hazijaanza kazi. Aidha, COSOTA pia ina majukumu ya kutunza rejesta za kazi za ubunifu, usanii na vyama vya watunzi,

wasanii, wafasiri, watayarishaji wa sauti zilizorekodiwa, watangazaji na wachapishaji, kutoa elimu katika masuala ya hakimiliki, kusimamia uanzishwaji na uendeshwaji wa kampuni za kukusanya na kugawa mirabaha ya wasanii na wamiliki wa hakimiliki na hakishiriki, kushughulikia migogoro ya hakimiliki ili kubainisha umiliki na kukuza ushirikiano na mashirika na ofisi za kimataifa zinazohusiana na masuala ya hakimiliki na miliki bunifu kwa ujumla.

**97.** ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya shilingi 1,350,000,000 zilipangwa kupatikana kutokana na vyanzo mbalimbali vikiwemo mirabaha kutoka kwa watumiaji wa kazi za Sanaa; leseni 419; Mirabaha toka kwa watumiaji wa kazi za sanaa; Ada ya Wanachama na usajili wa Hakimiliki; na Mapato ya Uendeshaji. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Mei 17, 2023 jumla ya shilingi 302,760,823, sawa na wastani wa asilimia 22.43 ya lengo zilikusanywa. Mapato mengine yalitegemewa kukusanywa kutokana na chanzo kipya cha mapato kutoka kwenye vibebeo vya kazi za ubunifu yaani *blanktape devices* ambapo hadi sasa taarifa ya utekelezaji wake kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) bado

haijapokelewa.

**98.** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi imeendelea na usajili wa kazi na wasanii, waandishi na wabunifu wanaomiliki kazi za ubunifu. Kwa sasa usajili huo hufanyika kwa njia ya mtandao kupitia kiunganishi cha *www.hakimiliki.go.tz.*

Ili kuboresha usimamizi wa kazi za hakimiliki, COSOTA imepandisha kazi hizo katika mfumo wa kidigiti kwa utambuzi ili kujulikana zinapotumika kwenye mitandao mbalimbali. Inatarajiwa fedha kutokana na matumizi mbalimbali ya kazi hizo kuwasilishwa COSOTA kutoka katika Kampuni ya *Composers, Authors and Publishers Association* (CAPASSO) ya Afrika Kusini kwa ajili ya kupewa wasanii na wadau wa kazi husika. Jumla ya kazi 22,203 za muziki zilipandishwa kwenye mfumo baada ya kuhakikiwa na kusajiliwa katika mfumo wa WIPOCOS ili wasanii wanufaike na mgao wa kazi zao kwa njia ya kidigitali. Taarifa hizo zitawezesha Ofisi ya Hakimiliki kuweza kupokea fedha ya mirabaha kutokana na haki za matumizi ya Kidijitali (Digital Mechanical Rights) zinazosimamiwa na Taasisi hiyo iliyoko nchini Afrika Kusini.

**99.** ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusiana na usajili na matumizi ya kazi nje ya nchi, COSOTA imeendelea na kufuatilia ushirikiano na Vyama dada kwenye mataifa mbalimbali. Ofisi imefanya mawasiliano na Ofisi za Hakimiliki katika nchi tatu (3) ambazo ni DR Congo *(Bureau Congolais du Droit dÁuteur - BCDA),* Liberia *(Copyright Society of Liberia - COSOL)* na Gambia *(Copyright Society of Gambia - COSOG)* ili kuboresha ushirikiano wa usimamizi wa Hakimiliki. Kutokana na mabadiliko ya sheria kuanza kutambua kampuni za ukusanyaji na ugawaji mirabaha, COSOTA inatarajia kusaidia Kampuni husika kusaini mikataba na kampuni kama hizo kwa nchi mbalimbali ili kuwezesha ukusanyaji na ugawaji mirabaha. Katika kipindi hiki, COSOTA pia imekuwa na ushirikiano ambao umeendelea kupitia Shirika la Miliki Ubunifu Duniani (World Intellectual Property Organization -WIPO) na Shirika la Miliki Ubunifu Afrika (African Regional Intellectual Property Organization - ARIPO) na Shirikisho la Watunzi na Waandishi Duniani (Confederation of Authors and Composers Societues - CISAC), Shirikisho la Waandaaji wa kazi (International Federation of Phonograms Industries - IFPI) na Shirikisho linalohusika na uchapishaji (International Federation for

Reprographic Rights Organizations -IFRRO).

**100.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Mei, 2023 Ofisi ilipokea Migogoro 29 kwa ajili ya kufanyiwa usuluhishi na kati ya migogoro iliyopokelewa, iliyotatuliwa na kuhitimishwa ni migogoro 23 na 6 iliyobaki inaendelea na utaratibu wa utatuzi. Aidha, elimu ya hakimiliki ilitolewa kwa wateja 476 ambapo wateja 425 walitoka Dar es Salaam na wateja 51 walitoka Arusha. Kutokana na mageuzi ya taasisi (Institutional Reform) inayotokana na Marekebisho ya Sheria ya Hakimiliki Na 7/1999 yaliyofanyika Julai, 2022 kupitia Sheria ya Fedha ya Mwaka 2022, COSOTA pia imetoa elimu kwa wadau mbalimbali ikiwemo Semina kwa Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo tarehe 20 Septemba, 2022 na tarehe 18 Mei 2023. Vilevile, tarehe 30 Mei, 2023 COSOTA ilifanya semina kwa Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu ulinzi wa Hakimiliki za Kazi za Ubunifu.

**101.** ***Mheshimiwa Spika***, elimu pia imetolewa kwa Shirikisho la Sanaa za Maonesho, Shirikisho la Muziki Tanzania, Shirikisho la Filamu na

Chama cha Wachapishaji Tanzania. Elimu kwa umma imefanyika kwa kushirikiana na wadau kama Benki ya NBC, Ziiki Media na Wasafi Media, Kampuni ya Multichoice Tanzania, Kampuni ya Azam Media, Taasisi za WUSM, Viwanja vya Sabasaba (Tanzania Trade Development Authority - TANTRADE), ABC Initiative na *ABC Attorneys, Tanzania Music Foundation, Bongo Star Search* na *Tanzania Cosmetology Association* na Kadogoo *Club*.

**102.** ***Mheshimiwa Spika***, COSOTA pia imeshirikiana na Kamati ya Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo iliyoundwa kwa ajili ya kukusanya maoni ya wadau kuhusu namna bora zaidi ya usimamizi wa hakimiliki nchini. Maoni na elimu kuhusu hakimiliki ilitolewa kwa Kanda sita (6) ambazo ni Kanda ya Kati (Dodoma), Kanda ya Kusini (Mtwara), Kanda ya Ziwa (Mwanza), Kanda ya Kaskazini (Arusha), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (Mbeya) na Kanda ya Mashariki (Dar es Salaam). Matokeo ya kazi ya Kamati hiyo ni marekebisho ya Kanuni, kutolewa elimu kwa wadau, na mabadiliko ya muundo wa COSOTA. Mabadiliko ya Kanuni yamepelekea kuwapo na nafasi ya kuundwa kwa kampuni binafsi za wasanii (Collective

Management Organizations – CMOs) ambazo zitahusika na ukusanyaji na ugawaji wa mirabaha kwa wasanii. CMOs hizi zitaundwa na wasanii wenyewe.

**103.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na kuwa Kanuni za kuanzishwa kwa CMOs hizo zimepitishwa mwezi Mei, 2023, kwa sasa COSOTA ipo katika harakati za kuhamasisha na kutoa elimu kwa wadau wanaohusika kujiunga na kuunda CMOs zao. Aidha, naomba nitumie fursa hii kuwahimiza na kuwahamasisha wadau wote wanaohusika na hakimiliki kujiunga na kuunda CMOs zao kwa maslahi yao.

**104.** ***Mheshimiwa Spika***, kutokana na marekebisho ya kanuni ya leseni iliyoingizwa katika mfumo wa Government electronic Payment Gateway (GePG), COSOTA kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango imefanya maboresho ya mfumo wa usajili na utoaji wa leseni unaopatikana *www.hakimiliki.co.tz* kwa lengo la kuwezesha mfumo kutumika kwa urahisi zaidi. Marekebisho hayo ni pamoja na uwekaji wa viwango vipya vya leseni (Tariffs). Matokeo ya marekebisho hayo ya mfumo ni pamoja na kuongezeka kwa usajili wa wanachama 576;

kusajiliwa kwa kazi 1,074 na leseni 6.

**105.** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi imehuisha Muundo wa Taasisi (Organisation Structure) baada ya marekebisho ya Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki. Marekebisho hayo yalifanyika kwenye majukumu ya Idara ya Leseni na Uharamia, Idara ya Kumbukumbu pamoja na kuanzishwa kwa Kurugenzi ya Sheria na Vitengo vyake ambapo hapo awali kilikua Kitengo kimoja. Rasimu ya Muundo huo imewasilishwa Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa hatua zaidi za utekelezaji.

**106.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha utekelezaji, COSOTA imefanya ukaguzi dhidi ya warusha maudhui kwa njia ya waya wasio na leseni na kutumia maudhui ya wazalishaji/wamiliki kinyume na Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Na.7/1999. Ukaguzi huo ulifanyika kwa kushirikiana na wadau yaani Kampuni ya Multichoice Tanzania; Kampuni ya Azam Media; na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) katika mikoa ya Arusha, Geita, Tabora, Katavi, Rukwa, Songwe, Mtwara na Pwani. Kutokana na ukaguzi huo, kesi tano (5) zilifunguliwa na mmiliki mmoja wa *cable* mkoani Katavi alipewa barua ya onyo kwa kuzuia maafisa

ukaguzi kutekeleza majukumu yao. Vilevile, ukaguzi umefanyika kwa wanaogoma kulipia leseni kwa mikoa ya Dodoma, Dar es Salaam na Arusha. Ukaguzi kama huo utaendelea kufanyika katika mikoa mingine ya Tanzania Bara iliyobaki, hadi mikoa yote itakapofikiwa.

#### 3.2.2.5 TAASISI YA SANAA NA UTAMADUNI BAGAMOYO (TaSUBa)

**107.** ***Mheshimiwa Spika,*** hatuwezi kuendeleza sanaa bila kuwekeza katika utaalamu na utafiti; TaSUBa ni Taasisi inayotoa mafunzo ya aina mbalimbali kuhusiana na masuala ya Sanaa na Utamaduni nchini. TaSUBa ni Taasisi ambayo inatoa kozi mbalimbali za masuala ya Sanaa na Utamaduni, miongoni mwa kozi hizo ni pamoja na Filamu na Uzalishaji wa Vipindi vya Televisheni (Film and TV Production); Uzalishaji wa Muziki na Sauti (Music and Sound Production); na Sanaa za Maonesho na Ufundi (Performing and Visual Arts). Aidha, Taasisi inatarajia kuanza kutoa mafunzo ya kozi mpya ambazo ni Usimamizi wa Sanaa na Masoko katika Sanaa (Arts Management and Marketing); Urithi wa Utamaduni na Utalii (Cultural Heritage and Tourism); na Muziki (Music). Mafunzo ya kozi hizo yataanza mara tu baada ya kukamilisha

mahitaji ya NACTVET ambayo yako katika hatua za mwisho kukamilishwa. Kazi zote zitatolewa katika ngazi ya Astashahada na Stashahada (Certificate and Diploma).

**108.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Aprili, 2023 TaSUBa imefanikiwa kuvuka lengo kwa kudahili wanachuo 684 wa kozi ndefu sawa na ongezeko la asilimia 14 ya lengo la wanachuo 600. Ongezeko hilo linatokana na uhamasishaji mkubwa uliofanywa na Taasisi. Kwa wanafunzi waliodahiliwa kozi fupi kwa kipindi hicho ni 222, sawa na asilimia 148 ya lengo la kudahili wanafunzi 150. Aidha, Taasisi imefanikiwa kuendesha semina mbili (3), warsha tatu (5) na kongamano moja (1). Kongamano lilifanyika wakati wa Tamasha la Kimataifa la 41 la Sanaa na Utamaduni Bagamoyo ambapo washiriki walitoka nje na ndani ya nchi, hivyo lilifanyika kwa mafanikio makubwa kutokana na mahudhurio ya washiriki na mada zilizojadiliwa katika kongamano hilo.

**109.** **Mheshimiwa *Spika*,** pia Taasisi imefanikiwa kuandaa Mitaala na kuiwasilisha kwenye Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na

Mafunzo ya Ufundi Stadi (The National Council for Technical and Vocational Eduction and Training - NACTVET) kwa ajili ya kupata Ithibati. Mitaala hiyo ni: Urithi wa Utamaduni na Utalii - Cultural Heritage and Tourism; Muziki – Music; na Usimamizi wa Sanaa na Masoko - Art Management and Marketing.

**110.** ***Mheshimiwa Spika***, Taasisi iliendesha Tamasha la 41 la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni la Bagamoyo ambapo Taasisi hii ni muanzilishi na mwenyeji wa Tamasha hilo lililofanyika tarehe 10 - 12 Novemba, 2022, ambalo hufanyika kila mwaka mara moja. Mgeni rasmi siku ya ufunguzi alikuwa Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tamasha lilihudhuriwa na watazamaji wa ndani na nje wanaokadiriwa kufikia 30,000. Aidha, vikundi mbalimbali vya sanaa kutoka ndani na nje ya nchi vipatavyo 46 vilishiriki. Kati ya hivyo, vikundi vya ndani vilikuwa 40 na vya nje 6 kutoka nchi za Zambia (vikundi 4); Canada (kikundi 1); na Visiwa vya Mayotte – Ufaransa (kikundi 1).




*Onesho la Sanaa la Wakufunzi na Wanachuo katika Tamasha la 41 la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni Bagamoyo lililofanyika tarehe 10 Novemba, 2022 Bagamoyo, Pwani.*

**111.** ***Mheshimiwa Spika***, TaSUBa imeendelea Kuimarisha Mtandao (Networks) kati ya Taasisi na Wadau wa Sanaa Nje na Ndani ya Nchi kwa kushirikiana na wadau wa ndani wafuatao ambao tayari makubaliano ya ushirikiano (MoU) yamesainiwa. Miongoni mwa wadau wa ndani ni pamoja na *Good Neighbours Tanzania;* Chuo cha Taaluma ya Urekebishaji Tanzania *(Tanzania Correction Training Academy -TCTA); Tanzania House of Talent (THT);* na *Naweza Foundation.* Wadau wa nje ambao Taasisi inashirikiana nao na makubaliano ya ushirikiano (MoU) yamesainiwa ni pamoja na *Bagamoyo Friendship*

*Society* (Ujerumani); *Musicians for a Better Life* (Ujerumani); na *Volkshochschule Ahlen* (VHS Ahlen - Ujeremani). Taasisi inaendelea na mazungumzo na taratibu za kusaini ushirikiano na *Pedagogical Studies & Arts Teacher's Pedagogical Studies - University of the Arts Helsinki* Finland; *Teaching Artist Institute - TAI* (Marekani); na *Media for Development International Inc.* (Marekani).

### 3.2.3 SEKTA YA MICHEZO

#### 3.2.3.1 IDARA YA MAENDELEO YA MICHEZO

**112.** ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Maendeleo ya Michezo hapa nchini ina jukumu la kuhakikisha inaweka mazingira bora na kuwezesha Maendeleo ya Michezo hususan kuzalisha ajira, kuimarisha afya za wananchi pamoja na kuwaletea furaha Watanzania. Sekta hii kwa sasa inatekeleza majukumu yake kwa kufuata Sera ya Maendeleo ya Michezo ya Mwaka 1995 ambayo imetengenezewa mkakati wa Utekelezaji wa mwaka 2022. Sekta hii ni miongoni mwa mihimili inayotoa ajira na kuchangia katika uchumi wa mtu mmoja mmoja na kwa Taifa kwa ujumla. Aidha, sekta hii

inahusisha Idara ya Maendeleo ya Michezo, Baraza la Michezo la Taifa (BMT), na Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya. Katika kutekeleza majukumu yake Wizara kupitia Sekta hii imetekeleza majukumu ifuatavyo:

**113.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeratibu mashindano ya Jumuiya ya Madola yaliyofanyika mwezi Julai hadi Agosti, 2022 nchini Uingereza katika mji wa Birmingham. Timu mbalimbali kutoka Tanzania zilishiriki zikiwemo timu za michezo ya Riadha, Ngumi, Judo, Kuogelea na Kunyanyua Vitu Vizito (Powerlifting). Kwa mara ya kwanza baada ya miaka mingi Tanzania ilifanikiwa kupata medali tatu (3), ambapo moja (1) ni ya fedha kutoka kwa mwanariadha Alphonce Simbu aliyoipata katika mbio za Marathon na mbili (2) za shaba kutoka kwa mabondia Yusuph Changarawe aliyemchapa bila huruma kwa *knockout* bondia Arthur Langlier wa St. Lucia na Kassim Mbundwike aliyepata medali hiyo baada ya kumuadhibu kwa *knockout* bondia Marion Faustino Ah Tong kutoka visiwa vya Samoa.

**114.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuratibu mashindano ya Taifa Cup, Ili

kuhakikisha Mashindano hayo yanakuwa na hadhi ya Taifa, Serikali kupitia Wizara imeelekeza mashindano hayo kuanzia katika ngazi ya chini kabisa ya Mtaa. Dhana hii ndiyo inayofahamika kama Mashindano ya Taifa Cup Mtaa kwa Mtaa. Mashindano haya yaliyozinduliwa katika Wilaya ya Rufiji Mkoa wa Pwani tarehe 16 Oktoba, 2022 na baadaye Jijini Arusha tarehe 9 Desemba, 2022 ambapo pia yalizinduliwa katika Wilaya ya Karatu tarehe 10 Desemba, 2022 na aliyekuwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo Mheshimiwa Mohamed O. Mchengerwa (Mb.). Mashindano haya yanaanzia ngazi ya Mtaa na kuendelea hadi ngazi ya Taifa. Lengo la mashindano hayo ni kuibua vipaji vya michezo na sanaa kuanzia ngazi ya mtaa. Kutokana na mpango huo Serikali imefanikiwa kupata vifaa vya michezo vitakavyotumika katika mashindano hayo, kutoka kwa wafadhili nchini China ambavyo vitagawiwa kwa Halmashauri ikiwa ni hatua ya kuyawezesha mashindano hayo kuwa na hamasa na kuvutia washiriki wengi zaidi katika ngazi zote.

**115.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ina dhamira ya kweli ya kuinua michezo, ambapo imeendelea kuziwezesha Timu za Taifa kwa kadri

bajeti inavyopatikana. Katika kipindi cha mwaka 2022/23 Timu ya Taifa ya Wanawake (Serengeti Girls) iliwezeshwa kukaa kambi ya maandalizi ya wiki mbili nchini Uingereza katika jiji la Southampton kabla ya kushiriki fainali za kombe la dunia nchini India. Aidha, Serikali iligharamia kambi ya maandalizi ya miezi sita iliyofanyika ndani ya nchi na wiki mbili nchini Uturuki Timu ya Wanaume ya mpira wa miguu ya Watu Wenye Ulemavu (Tembo Warriors) kushiriki mashindano ya fainali za Kombe la Dunia yaliyofanyika nchini Uturuki. Aidha, Serikali iliisaidia Timu ya *Fountain Gate* ya Mpira wa Miguu iliyopo Jijini Dodoma kushiriki mashindano yaliyoandaliwa na CAF kwa shule za Sekondari ya Bara la Afrika kwa Wasichana yaliyofanyika Durban Afrika Kusini mwezi Aprili, 2023 na Timu hiyo ilitwaa Ubingwa wa Bara la Afrika.

**116.** ***Mheshimiwa Spika***, Tanzania imeendelea kuwa mwenyeji wa mikutano ya Kimataifa ambapo tarehe 10 Agosti, 2022 ilikuwa mwenyeji wa Mkutano Mkuu wa 44 wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF) ambao ulifanyika Jijini Arusha na Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Duniani (FIFA) Bw. Giani Infantino pamoja

na viongozi wengine kutoka sehemu mbalimbali Afrika na Duniani walishiriki mkutano huo. Aidha, tarehe 24 Mei, 2023 Wizara imewasilisha Taarifa ya Tanzania kwa kushirikiana na nchi ya Kenya na Uganda kuhusu kuwa mwenyeji wa Mashindano ya Mpira wa Miguu barani Afrika (AFCON 2027). Taarifa ya kuomba zabuni ya kuwa mwenyeji wa mashindano hayo imeshawasilishwa CAF na kura ya uamuzi wa nani ameshinda zabuni hiyo itapigwa mwezi Julai, 2023. Fauka ya hayo, nchi zinazoshindania uenyeji wa mashindano hayo ni pamoja na Botswana, Misri, na Algeria.

**117.** ***Mheshimiwa Spika***, tarehe 2 - 4 Mei, 2023 nchi yetu ilikuwa mwenyeji wa Mkutano wa Mawaziri wa Michezo wa Baraza la Michezo la Afrika Kanda ya IV uliofanyika Jijini Arusha ambapo Viongozi kutoka Nchi 9 kati ya 14 wanachama wa Baraza hilo walishiriki. Katika Mkutano huo, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alituma salamu, naomba ninukuu. "*Huu ni mkutano wa kwanza wa kihistoria wa Kanda ya IV kufanyika katika ardhi ya Tanzania. Tunawakaribisha Wajumbe wote wa Baraza la Michezo la Umoja wa Afrika Kanda ya IV hapa*

*nchini kwetu ambayo ni Nchi ya amani na ukarimu ikiwa na vivutio vingi vya Utalii Bora Duniani".* Mwisho wa kunukuu.

**118.** ***Mheshimiwa Spika***, mgeni rasmi katika mkutano huo alikuwa Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kati ya mambo aliyoyasema, miongoni ni pamoja na, naomba ninukuu *"kuwekeza kwenye kujenga uwezo wa kitalaamu ili kuzalisha wanamichezo wanaoweza kuleta mageuzi kwenye Sekta ya Maendeleo ya Michezo na Maendeleo kupitia Michezo. Tusikubali kushika mkia kila siku na wala tusikubali kurudi nyuma. Lengo la kila taifa ni kuona timu yake inashinda makombe ya Kimataifa hasa Kombe la Dunia. Tukiamua kuwekeza kwenye miundombinu ya michezo na ujuzi pamoja na kushirikiana tunaweza kufikia malengo makubwa kwenye sekta ya michezo".* Mwisho wa kunukuu.



*Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipohutubia Mkutano wa Mawaziri wa Michezo wa Baraza la Michezo la Umoja wa Afrika Kanda ya IV uliofanyika Jijini Arusha tarehe 2 - 4 Mei, 2023.*

**119.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa kutumia Mkutano huo, Tanzania ilitumia fursa hiyo vizuri kwa kuomba nafasi ya kuwa Makao Makuu ya Kanda ya IV ambapo ilikidhi vigezo vyote ambavyo Baraza la Michezo la Umoja wa Afrika Kanda ya IV vilitakiwa na hivyo kuifanya Tanzania kuchaguliwa kuwa Makao Makuu ya Sekretarieti ya Baraza hilo. Baraza la Michezo la Umoja wa Afrika Kanda ya IV linahusisha nchi za Comoros, Djibouti, Eritrea, Ethiopia, Kenya, Madagascar, Mauritius, Rwanda, Sychelles,

Somalia, Sudan, Sudani Kusini, Uganda na Tanzania. Kwa kuwa Ofisi za Makao Makuu ya Baraza la Michezo la Umoja wa Afrika Kanda ya IV imepitishwa kuwa Tanzania, itasaidia kudumisha uhusiano na mataifa wanachama na itatoa ajira kwa vijana wa Kitanzania hususan katika sekta ya michezo lakini pia itasaidia kuhamasisha upatikanaji wa wataalamu zaidi wa michezo.

**120.** ***Mheshimiwa Spika***, kutokana na mafanikio kadhaa yaliyopatikana katika kipindi ambacho Serikali ilitia mkono wake katika kuziunga mkono Timu za Taifa zinapokwenda kwenye mashindano ya Kimataifa, Serikali itaendelea kuziunga mkono Timu zote za Taifa zitakazofuzu kushiriki mashindano ya Kimataifa. Ili kuhakikisha hilo linatekelezwa, Serikali itaendelea kutenga bajeti ya kuhudumia Timu za Taifa kujiandaa na kushiriki Mashindano ya Kimataifa. Mfano, mwaka 2019/20 Serikali ilitenga Sh. 270,000,000; mwaka 2020/21 ilitenga Sh. 431,000,000; mwaka 2021/22 ilitenga Sh. 1,320,000,000; mwaka 2022/23 ilitenga Sh. 1,446,900,000; na mwaka 2023/24 Serikali imetenga Sh. 1,066,895,000.

**121.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea na lengo la kuiwezesha Tanzania kuwa na miundombinu ya michezo bora katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati. Kwa sasa, Wizara inaendelea na taratibu mbalimbali za Ujenzi wa Viwanja vya Mazoezi na Kupumzika Wananchi (Recreational and Sports Centres) katika mikoa ya Dar es Salaam na Dodoma ambapo mikataba ya ujenzi imesainiwa kwa maeneo ya Dar es Salaam na Dodoma. Mkandarasi amekabidhiwa maeneo na ameanza hatua za awali za ujenzi (mobilization stage). Ujenzi wa maeneo hayo unatarajiwa kugharimu zaidi ya shilingi bilioni 54.6 na ujenzi utafanyika katika kipindi cha miezi 36. Serikali pia inaendelea na taratibu za ujenzi wa uwanja mkubwa wa michezo katika Mkoa wa Dodoma katika eneo la Nzuguni ambapo zabuni kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa uwanja huo imetangazwa. Sambamba na ujenzi wa Uwanja wa Michezo Dodoma, pia Serikali inajiandaa kujenga Uwanja kama huo katika jiji la Arusha kwa ajili ya kujiandaa na michezo ya AFCON 2027 endapo nchi za Afrika Mashariki zitashinda zabuni ya kuandaa michezo hiyo.



*Muonekano wa Kituo cha Mazoezi na Kupumzikia Wananchi kitakavyokuwa mara baada ya kukamilika kujengwa katika jiji la Dodoma eneo la Nanenane Nzuguni.*

**122.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeanza kukarabati miundombinu ya Michezo katika shule Teule za Michezo Nchini. Shule hizi 56 za Sekondari zinahusisha shule mbili kwa kila Mkoa, kutoka mikoa yote ya Tanzania Bara ikiwa na lengo la kuendeleza vipaji vya michezo mbalimbali vinavyoibuliwa kutoka katika ngazi ya shule za msingi. Miundombinu ya Michezo kwenye shule zilizoteuliwa inahitaji ukarabati na ujenzi. Utekelezaji wa mpango wa kuboresha miundombinu hiyo utafanyika kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha ambapo kwa awamu ya kwanza, imefanyika tathmini ya

miundombinu ya michezo katika shule saba (7) kutoka katika mikoa ya Tabora, Tanga, Dodoma, Manyara, Pwani na Mtwara. Mshauri mwelekezi kwa ajili ya kusimamia mradi huu amepatikana ambaye ni Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) na kwa sasa kwa kushirikiana na Wizara anaendelea na zoezi la kukamilisha nyaraka za zabuni kwa ajili ya kumpata mkandarasi wa kutekeleza mradi huo.

**123.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali Mitaa (OR-TAMISEMI) na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia iliandaa Mwongozo kwa ajili ya maandalizi na uendeshaji wa Michezo ya Umoja wa Michezo ya Shule za Sekondari Tanzania (UMISSETA) na Umoja wa Michezo na Taaluma kwa Shule za Msingi Tanzania (UMITASHUMTA) Kitaifa. Mwongozo unabainisha masuala mbalimbali ikiwemo utaratibu wa uteuzi wa Kamati ya Kitaifa ya uratibu, Udhamini, mgawanyo wa bajeti na ugharamiaji wa mashindano hayo. Kwa mwaka 2022/23 mashindano hayo yaliyofanyika mkoani Tabora kuanzia tarehe 29 Julai, 2022 hadi 19 Agosti, 2022 jumla ya wachezaji na viongozi 3,920 wa shule za msingi walishiriki, na wachezaji na

viongozi 4,200 wa shule za Sekondari kutoka mikoa yote ya Tanzania Bara na Visiwani walishiriki. Mashindano haya yamekuwa na manufaa makubwa kwa kuwaunganisha wanafunzi na ni njia mojawapo ya kuibuwa vipaji kwa ajili ya timu zetu za Taifa na vilabu mbalimbali nchini.

**124.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwongozo wa uendeshaji wa mashindano ya UMISSETA, UMITASHUMTA na *Federation of East Africa Secondary School Sports Associations* (FEASSSA) umekamilika na umesambazwa katika Sekretarieti za mikoa na Wizara zenye dhamana na Elimu, Michezo na OR-TAMISEMI. Aidha, mwongozo huo umezinduliwa wakati wa uzinduzi wa michezo UMISSETA na UMITASHUMTA ya tarehe 04 Agosti, 2022. Aidha, mashindano hayo kwa mwaka 2023 yamezinduliwa tarehe 03 Juni, 2023 na yanafanyikia mkoani Tabora, ambapo mashindano ya FEASSSA yatafanyika mwezi Agosti, 2023 nchini Rwanda, baada ya kumalizika kwa mashindano ya UMISSETA na UMITASHUMTA.



*Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (kulia) akizindua Mwongozo wa Michezo ya UMISSETA, UMITASHUMTA na FEASSSA tarehe 04 Agosti, 2022.*

**125.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kupambana na mbinu haramu za matumizi ya dawa za kuongeza na kusisimua misuli michezoni, Serikali kupitia Wizara ilipokea fedha dola za Marekani 21,025.06 mwezi Septemba, 2022 kutoka Shirika la Elimu, Sayansi na Utamaduni la Umoja wa Mataifa (UNESCO) kwa ajili ya kuwezesha mafunzo ya kukabiliana na matumizi ya dawa na mbinu haramu michezoni. Kutokana na fedha hizo masuala yaliyofanyika ni pamoja

na wajumbe 2 kutoka Tanzania walihudhuria Mkutano wa Kanda ya Tano wa *Antidoping* nchini Uganda mwezi Oktoba, 2022; kuwezesha kuendesha mafunzo ya Wakufunzi (ToT) kwa Maafisa 30 kutoka Wizarani, BMT, Vyama vya Michezo na Maafisa Michezo wa Wilaya za Mkoa wa Dar es Salaam; mafunzo ya uelewa kuhusu *antidoping* kwa viongozi 180 wa vyama vya kitaifa vya Michezo; mafunzo kwa wadau na waendeshaji wa mashindano ya michezo 100 kuhusu umuhimu wa kuwapo kwa Sheria ya *antidoping*; na mafunzo kwa Maafisa Michezo 38 wa mikoa, BMT na Wizara yaliyofanyika Jijini Dodoma tarehe 31 Novemba hadi 1 Desemba, 2022.

**126.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imekuwa ikiimarisha na kuwashirikisha watu wenye mahitaji maalumu katika michezo. Kwa mwaka 2022/23 katika michezo ya UMISSETA na UMITASHIMTA kwa mara ya kwanza watoto wenye mahitaji maalumu walishiriki michezo hiyo iliyofanyika katika mkoa wa Tabora. Aidha, kupitia Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Timu ya Taifa ya Mchezo wa Tennis (Wheel Chair Tennis) imewezeshwa kupata eneo la kujenga Miundombinu ya michezo jijini Dar es Salaam

katika Wilaya ya Kigamboni; Timu ya Wanawake ya Basketball (Wheel Chair Basketball) ilishirikishwa katika Tamasha la Wanawake lijulikanalo kwa jina la *Tanzanite International Women Sports Festival* lililofanyika tarehe 20 hadi 22 Oktoba, 2022 Jijini Dar es Salaam; na Timu ya Taifa ya Walemavu wanaocheza mpira wa miguu (Tembo Warriors) waliwezeshwa kifedha na kiutaalamu hadi kufika robo fainali ya mashindano ya Kombe la Dunia kwa mchezo huo yaliyofanyika nchini Uturuki kuanzia tarehe 30 Septemba hadi 10 Oktoba, 2022.

### 3.2.3.2 BARAZA LA MICHEZO LA TAIFA (BMT)

**127.** ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu ya Baraza la Michezo la Taifa (BMT) ni pamoja na kuendeleza, kustawisha na kusimamia aina zote za michezo ya ridhaa na kulipwa kwa kushirikiana na Vyama na Mashirikisho ya Michezo; kusajili Vyama vya Michezo; kutoa Tuzo kwa Wanamichezo wanaofanya vizuri katika mashindano ya Kitaifa na kimataifa; na kuamsha ari ya wananchi kupenda aina zote za michezo.

**128.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia BMT limewezesha kuzigharamia Timu za Taifa

kushiriki katika mashindano mbalimbali ya kimataifa. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2022 hadi Aprili, 2023 Serikali kupitia BMT, imewezesha jumla ya timu 15 kushiriki katika mashindano ya kimataifa ambapo kiasi cha shilingi 3,636,512,694.90 kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwemo Mfuko wa Maendeleo ya Michezo, udhamini na harambee zimetumika. Timu hizo ni pamoja na Timu za michezo ya Riadha, Ngumi, Judo, Kuogelea na Parapowerlifting ziliwezeshwa kushiriki mashindano ya Jumuiya ya Madola yaliyofanyika Birmingham nchini Uingereza. Katika mashindano hayo Tanzania ilipata jumla ya medali tatu katika mchezo wa Riadha na Ngumi; Timu ya Taifa ya vijana ya Mpira wa Miguu kwa Wanawake (Serengeti Girls) iliwezeshwa kushiriki mashindano ya Kombe la Dunia yaliyofanyika nchini India kuanzia tarehe 11 hadi 30 Oktoba, 2022 ambapo timu hiyo ilifanikiwa kufika hatua ya robo fainali. Hii iliwezekana baada ya timu yetu kuichapa timu ya Taifa ya Ufaransa mabao (2-1) na kutoka sare dhidi ya Kanada (1-1).

**129.** ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio mengine ni Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu kwa watu wenye ulemavu (Tembo Warriors) iliwezeshwa

kushiriki mashindano ya Kombe la Dunia yaliyofanyika nchini Uturuki kuanzia tarehe 30 Septemba hadi 10 Oktoba, 2022 ambapo timu hiyo ilifanikiwa kufika hatua ya robo fainali na kushika nafasi ya saba (7) duniani. Pia, Timu hiyo ilifanikiwa kuziadhibu nchi kubwa duniani kama Japan (3-1) na Uzbekistan (3-0) na kutoka sare na nchi ya Uhispania (0-0). Aidha, baada ya mashindano hayo, timu hiyo ilifanikiwa kuuza wachezaji 10 katika vilabu vya nchini humo. Wachezaji waliobahatika kupata ajira katika Timu za nchini Uturuki ni pamoja na Alfan Kyanga, Juma Kidevu, Habibu Likoike na Shedrack Hebron waliosajiliwa kwenye klabu ya Sisli Yeditepe. Wengine ni Abdulkarim Amiri na Salimu Bakari waliosajiliwa na klabu ya Keysari, Ramadhan Chomelo aliyejiunga na klabu ya Konya na Frank Ngailo klabu ya Izmir BBSK na Mudrick Azzan na Richard Swai kwenye klabu ya Mersin.

**130.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/23 Tanzania imeendelea kufanya vizuri katika mashindano mbalimbali ya Kimataifa ikiwemo mpira wa miguu ambapo hivi karibuni timu zetu za Simba na Yanga zimeweza kufika katika hatua nzuri katika michezo ya Klabu

Bingwa na Kombe la Shirikisho Barani Afrika. Timu ya Yanga kwa mara ya kwanza katika historia ya michezo ya Shirikisho imekuwa ya kwanza kufuzu kucheza fainali baada ya kuiondoa timu ya Marumo Gallants ya Afrika Kusini kwa mabao 4-1 katika hatua ya nusu fainali. Aidha timu ya Simba ilifanikiwa kuingia robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika baada ya kuibuka mshindi wa mabao 7-0 dhidi ya timu ya Horoya ya Guinea.

**131.** ***Mheshimiwa Spika***, mafanikio hayo yamechochewa na maono ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye alichangia kwa kuziongezea morali timu zetu kwa kununua magoli ya ushindi, ambapo alianza na Sh. 5,000,000 katika hatua ya makundi na robo fainali; Sh. 10,000,000 katika hatua ya nusu fainali; na Sh. 20,000,000 na kutoa usafiri wa ndege katika hatua ya fainali. Kutokana na hamasa hiyo ya Mheshimiwa Rais, Timu ya Simba imeweza kupata jumla ya magoli 11 katika hatua ya makundi na robo fainali na kujikusanyia jumla ya Sh. 55,000,000 wakati Timu ya Yanga imeweza kupata magoli 16 katika hatua ya makundi, robo, nusu fainali na fainali

na kujikusanyia jumla ya Sh. 115,000,000. Mafanikio hayo ni makubwa na ya kihistoria kwa nchi yetu kwa kuwa inaimarisha ubora wa ligi yetu na kuitangaza Tanzania nje ya mipaka yetu.

**132.** ***Mheshimiwa Spika***, kadhalika wanamichezo wa Tanzania wameendelea kufanya vizuri katika mashindano ya Kimataifa na kuipeperusha vema bendera ya Tanzania. Wachezaji hao ni pamoja na Gabriel Gerald Geay aliyeshika nafasi ya pili katika Mbio kubwa Duniani za Boston Marathon na Valencia Marathon, mwanariadha Alphonce Felix Simbu aliyeshika nafasi ya Tatu katika mbio za Osaka Marathon na Yangzhou Jianzhen Half Marathon. Aidha, Timu ya Taifa ya Mchezo wa kuogelea ilishiriki Mashindano ya kualikwa nchini Afrika ya Kusini yaliyoshirikisha nchi 10 na kunyakua jumla ya medali 74 na kushika nafasi ya pili. Katika Nyanja za masumbwi, mabondia wa Kitanzania wameendelea kufanya vizuri katika mashindano mbalimbali ya Kimataifa. Mabondia waliofanya vizuri katika kipindi hiki ni pamoja na;

(i) Twaha Kiduku ambaye alimcharaza bondi Lago Kiziria kutoka nchini Georgia katika pambano lililofanyika mkoani Morogoro

tarehe 22 Aprili, 2023;

(ii) Hassan Mwakinyo ambaye alimbamiza bondia Murdochee Kuvesa Katembo kutoka nchini Congo DRC katika pambano lililofanyika jijini Dodoma tarehe 23 Aprili, 2023;

(iii) Ibrahim Class ambaye alimchakaza bondia Gustavo Pina Melger kutoka nchini Mexico katika pambano lililofanyika jijini Dar es Salaam tarehe 30 Septemba, 2022;

(iv) Mwanadada Fatuma Yazidu alimcharanga bondia Consolata Musanga kutoka nchini Kenya katika pambano lililofanyika Nairobi Kenya tarehe 25 Machi, 2023; na

(v) Bondia machachari Karim Mandonga alimchanachana bondia Kenneth Lukyamuzi kutoka nchini Uganda katika pambano lililofanyika Nairobi Kenya tarehe 25 Machi, 2023.

**133.** ***Mheshimiwa Spika,*** Timu ya Taifa ya Netiboli iliwezeshwa kushiriki mashindano ya Afrika ya kufuzu kushiriki Kombe la Dunia yaliyofanyika nchini Afrika Kusini mwezi Agosti, 2022. Vilevile Timu ya Taifa ya Wanawake ya Gofu iliwezeshwa kushiriki mashindano ya Afrika ya *All Africa Challenge Trophy* yaliyofanyika

mwezi Septemba, 2022 ambapo Tanzania ilikuwa mwenyeji wa mashindano hayo na kuibuka mshindi wa jumla wa tatu. Mafanikio mengine ni pamoja na Shirikisho la Michezo Vyuo Vikuu Tanzania kushiriki Kambi ya wanavyuo vya Afrika Mashariki; na Timu ya Taifa ya Kuogelea iliwezeshwa kushiriki mashindano ya ubingwa wa Kanda ya tatu, ambapo Tanzania ilikuwa mwenyeji wa mashindano hayo na timu ya Tanzania iliibuka mshindi wa kwanza kati ya nchi 12 zilizoshiriki.

**134.** ***Mheshimiwa Spika,*** kadhalika, mashindano ya Afrika Kanda ya Tano ya mpira wa mikono (handball) ambayo yalifanyika tarehe 25 hadi 30 Aprili, 2023 jijini Dar es Salaam na kushirikisha nchi 9 ambazo ni Tanzania, Kenya, Uganda, Burundi, Rwanda, Somalia, Ethiopia, Sudan Kusini na Djibouti yamewezeshwa. Vilevile, mashindano ya Judo ya Kanda ya Tano Afrika Mashariki ambayo yalifanyika kuanzia tarehe 29 hadi 30 Aprili, 2023 jijini Dar es Salaam na kushirikisha nchi za Tanzania Bara, Zanzibar, Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Somalia na Congo DRC yamewezeshwa. Pia, mashindano ya kimataifa ya Mpira wa Kikapu kwa Watu wenye Ulemavu (wheelchair basketball)

yaliyofanyika tarehe 5 – 7 Mei, 2023 jijini Dar es Salaam na kushirikisha nchi za Tanzania, Kenya, Uganda na Ethiopia yaliwezeshwa. Aidha, Baraza liliwezesha mashabiki wa klabu ya Yanga kwenda nchini Afrika Kusini kushuhudia mechi ya nusu fainali ya kombe la Shirikisho baina ya Yanga na Klabu ya Marumo Gallants.

**135.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na mazingira na amani iliyopo katika nchi yetu, imekuwa ni kuvutio kwa nchi za Afrika na dunia kwa ujumla kutaka kuendesha mashindano ya michezo mbalimbali katika nchi hii. Hivi karibuni tumepokea maombi kutoka Chama cha Kriketi Tanzania (TCA) la kuwa mwenyeji wa mashindano ya Kriketi ya kufuzu Kombe la Dunia kwa timu za vijana waliochini ya umri wa miaka 19 kwa nchi za Afrika. Mashindano hayo yatafanyika tarehe 21 - 30 Julai, 2023 jijini Dar es Salaam. Tunavikaribisha vyama vingine vya michezo kutoka duniani kote kuja Tanzania kufanya michezo yao, kwani ni sehemu sahihi wala hawatajutia maamuzi watakayokuwa wameyafanya ya kuichagua Tanzania.

**136.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Mei, 2023 Serikali kupitia BMT

imefanikiwa kusajili Vyama 5, Vilabu 109, Akademi 8, Vituo 10, Mawakala 4 na Wakuzaji 17. Aidha, mapitio ya Katiba ya Shirikisho ya Karate Tanzania (Tanzania Sports Karate – Do Federation), Chama cha Mchezo wa Gofu (Tanzania Golf Union) na Chama cha Mpira wa Miguu kwa Wanawake Tanzania yamefanyika. Pia, marekebisho ya Katiba ya Chama cha Morogoro Region Basketball Association na Katiba za Vilabu vinne (4) ambavyo ni Tanganyika Kigoma Football Club, Copco Football Club, Ceassia Queens Football Club, na Rock Solution Football Club yamefanyika.

**137.** ***Mheshimiwa Spika,*** BMT limefanikiwa kujenga Mfumo wa Usajili wa kidigitali (Online Registration) wenye lengo la kurahisisha utaratibu wa usajili kwa watendaji na wadau wa michezo. Mfumo huu utasaidia shughuli za usajili kufanyika kidigitali. Mfumo huu utawarahisishia wadau wa michezo kufanya usajili mahali popote walipo na kuwezesha kufanya malipo kwa kupata namba ya kumbukumbu ya malipo (control number). Kadhalika, mfumo huu utasaidia kuongezeka kwa ukusanyaji wa maduhuli. Kwa sasa mfumo upo kwenye hatua ya majaribio.

**138.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha kuwapo kwa wataalamu wa kutosha wa Michezo, BMT liliendesha mafunzo mbalimbali ya kuwajengea uwezo wanamichezo. Mafunzo hayo yalitolewa kwa michezo na viwango tofauti ambavyo ni BMT kwa kushirikiana na Kamisheni ya Ngumi za Kulipwa liliratibu na kusimamia mafunzo kwa wataalamu wa Ngumi za Kulipwa wakiwemo Makocha, Waamuzi na Wakuzaji wa Ngumi za Kulipwa nchini. Jumla ya wataalamu 100 walipata mafunzo hayo. Lengo ni kuwajengea uwezo wataalamu wa Ngumi kutekeleza majukumu yao kitaalamu kuendana na wakati. Aidha, kwa kushirikiana na Vyama vya Mchezo wa Riadha, Mpira wa Miguu na Netiboli Baraza liliratibu mafunzo kwa Walimu wa Shule teule 56 za Michezo za Sekondari kutoka mikoa yote ya Tanzania Bara. Jumla ya walimu 57 walipata mafunzo ya Mpira wa Miguu, Netiboli na Riadha. Lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea walimu uwezo wa kwenda kuibua na kuendeleza vipaji vya vijana kupitia shule hizo.

**139.** ***Mheshimiwa Spika,*** BMT liliendesha mafunzo kwa walimu wa Shule za Sekondari wapatao 48 kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Mafinga mkoani Iringa. Lengo la mafunzo hayo ni

kuwajengea uwezo walimu kuibua na kuendeleza vipaji vya watoto katika shule. BMT pia limesimamia Utawala Bora kwa Vyama vya Michezo. Katika kuendeleza dhana ya utawala bora kwa vyama, BMT limeweka mikakati mbalimbali ikiwemo kuandaa Katiba za mfano kwa vyama, vituo, wakuzaji, mawakala wa michezo, kufanya chaguzi za vyama mbalimbali vya michezo. Vyama vilivyofanya chaguzi ni pamoja na Tanzania Baseball & Soft Ball Association (TaBSA); Tanzania Rugby Union (TRU); Tanzania Table Tennis Association (TTTA); Tanzania Hockey Association (THA); Tanzania Golf Union (TGU), Tanzania Ladies Golf Union (TLGU), Chama cha Kuogelea Tanzania (TSA), Chama cha Baiskeli Tanzania (CHABATA)na Athletics Tanzania (AT).

**140.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia BMT iliratibu vikao kazi vya kamati za utendaji za Vyama na Mashirikisho ya Michezo ili kuwashauri na kuwajengea uwezo wa kiutawala na uongozi ambapo katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Aprili, 2023 vikao vya vyama 15 vimefanyika kama ifuatavyo: Shirikisho la Mpira wa Miguu kwa Watu Wenye Ulemavu (TAFF); Shirikisho la Ngumi za Wazi Tanzania (OBFT);

Chama cha Baseball & Softball Tanzania (TaBSA); Chama cha Kabaddi Tanzania; Chama cha Netiboli Tanzania (CHANETA); CHANETA NA CHANEZA; Riadha Tanzania (RT); Umoja wa wachezaji wa Soka wa Zamani (UMSOTA); PAN AFRICA; SIMBA SC; TFF & DRFA; Special Olympics; Chama cha Kriketi Tanzania (TCA); Chama cha WUSHU Tanzania; na Chama cha Tenisi Tanzania (TTA).

**141.** ***Mheshimiwa Spika,*** BMT lilifuatilia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa shughuli za michezo katika mikoa 26, Wilaya 52, Vyama vya Michezo 54 na Taasisi za Michezo 15. Katika kutekeleza jukumu hilo, Baraza liliendesha kikao kazi cha ufuatiliaji na tathmini kilichohusisha Makatibu wa Kamati zote za Michezo Tanzania Bara. Kikao hicho kilihudhuriwa na Makatibu kutoka mikoa 24 ya Tanzania Bara. Vilevile, Baraza lilifanya vikao kama hivyo na Vyama 28 na Taasisi tatu (3) za Michezo. Katika vikao hivyo ilisisitizwa kuendelea kusimamia kwa karibu utekelezaji wa shughuli za michezo katika ngazi za mikoa na Wilaya ikiwemo kuhamasisha ushiriki wa jamii katika michezo, kusimamia uendelezaji wa viwanja na miundombinu ya Michezo, kuibua vipaji, na kusimamia vyama na

Vilabu vya Michezo katika ngazi za mikoa na Wilaya.

**142.** ***Mheshimiwa Spika,*** BMT lilifanya ufuatiliaji wa mashindano mbalimbali ya Kitaifa yanayoandaliwa na Vyama na Mashirikisho ya Michezo ikiwemo SHIMMUTA – Tanga, SHIMIWI – Tanga, SHIMISEMITA – Morogoro, UMISSETA na UMMITASHUMTA – Tabora. Riadha – Arusha, Dodoma na Dar es Salaam, CHANETA – Morogoro na Dar es Salaam na kubaini kuwa mashindano hayo yanaleta hamasa kubwa na kusaidia ukuzaji na uendelezaji wa vipaji pamoja na kupunguza maradhi yasiyoambukiza. Pia yanahamasisha mshikamano, uzalendo na umoja miongoni mwa washiriki.

**143.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuendelea kuhamasisha ushiriki wa wanawake katika Michezo, katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Mei, 2023, Baraza liliratibu Tamasha la Kimataifa la Michezo la Wanawake (Tanzanite International Women Sports Festival) likihusisha Kongamano na Mashindano ya Michezo mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi. Jumla ya wanamichezo 712 kutoka vyama vya michezo 13 ikiwemo Mpira wa Miguu wanawake, Mpira wa Kikapu kawaida,

Mpira wa Kikapu kwa Watu wenye Ulemavu, Mpira wa Wavu, Netiboli, Ngumi za Ridhaa, Ngumi za Kulipwa, Michezo ya Jadi, Riadha, Karate, Kabaddi, Mpira wa Mikono na Power Arts kutoka nchi za Tanzania, Kenya, Uganda na Zambia walishiriki. Aidha, wananchi na wadau mbalimbali wa michezo wapatao 3,000 walihudhuria Tamasha hilo.

**144.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia BMT kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Japan (JICA) na Shirikisho la Riadha Tanzania waliandaa mashindano ya mchezo wa riadha kwa wanawake (*ladies First*) kutoka mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar. Lengo la mashindano hayo ni kuendelea kuhamasisha ushiriki wa wanawake katika michezo. Kutokana na matamasha na mashindano hayo kumeshuhudiwa kuhamasika kwa hali ya juu kwa wanawake kushiriki katika michezo mbalimbali.

**145.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa lengo la kuendelea kutambua vipaji vya wanamichezo na vilabu mahiri na wanaofanya vizuri katika mashindano mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa, BMT liliandaa tukio la utoaji Tuzo kwa

wanamichezo na vilabu ambapo tuzo hizo zilitolewa tarehe 17, Machi, 2023 ambapo wanamichezo na vilabu mbalimbali vilipewa tuzo mbalimbali kulingana na sifa ya mhusika.



*Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana (Mb.) akikabidhi Tuzo ya Wimbo Bora wa Mwaka 2022 kwa mwakilishi wa mwanamuziki Jay Melod kwenye Usiku wa Tuzo za Muziki Tanzania zilizofanyika tarehe 29 Aprili, 2023 Jijini Dar es Salaam.*

**146. *Mheshimiwa Spika,*** kwa upande mwingine, Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) kwa kushirikiana na Serikali wamejiunga na programu maalumu ya Mpira wa Miguu kwa Shule “Football for Schools(F4S)”

inayodhaminiwa na Shirikisho la Mpira wa Miguu la Dunia (FIFA) ambapo Tanzania itapokea mipira takriban elfu sitini na nne (64,000) kwa ajili ya programu hiyo. Mipira hiyo itapelekwa katika shule za Msingi zilizopo Tanzania Bara na Zanzibar ambapo kila Mkoa utapokea mipira takriban elfu mbili (2,000). Aidha, programu hiyo itahusisha pia utoaji wa mafunzo kwa walimu na makocha wa ngazi za chini "grassroot level" kutoka kwa wataalamu wa FIFA, hii ikiwa ni pamoja na kupata mbinu za kufundishia kupitia mfumo maalumu wa kidigitali ambao utatumiwa na walimu hao mara baada ya kupata mafunzo hayo. Programu hii itasaidia sana katika kuibua na kuendeleza vipaji kwa kuwa inahusisha upatikanaji wa mipira, mbinu za kufundishia na wataalamu wa kutosha.

#### 3.2.3.3 CHUO CHA MAENDELEO YA MICHEZO MALYA

**147.** ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya ni chuo pekee kinachotoa mafunzo ya michezo kwa wataalamu wa michezo nchini. Chuo hiki kipo mkoani Mwanza katika Wilaya ya Kwimba. Jukumu kuu la chuo hiki ni kufundisha taaluma ya michezo, kutafiti na kutoa ushauri kuhusu masuala ya

maendeleo ya michezo.

**148.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya imeendelea kudahili wanachuo katika masomo ya Michezo. Katika juhudi hizo, Chuo kimefanikiwa kuongeza idadi ya wanachuo ambapo katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Aprili, 2023 kilifanya usajili wa wanachuo 154 kwa mwaka wa kwanza ambapo Wanaume ni 108 na Wanawake ni 46 ukilinganisha na usajili wa wanachuo 130 katika mwaka 2021/22, sawa na ongezeko la asilimia 18. Kwa upande wa mwaka wa pili Chuo kina wanachuo 107, Wanaume 83 na Wanawake 24. Hivyo jumla ya wanachuo waliosajiliwa katika Chuo kwa mwaka 2022/23 ni 261 ikilinganishwa na jumla ya wanachuo 221 waliosajiliwa mwaka 2021/22.

**149.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2022/23 Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya kimetoa mafunzo ya muda mfupi katika vituo viwili vya Dar es Salaam na Chuoni Malya ambapo aina ya mafunzo yaliyotolewa ni kuhusu Mpira wa Mikono, Lishe, Tiba na Kinga, uandaaji na uratibu wa matukio mbalimbali ya michezo *(sports event management)*, utafutaji wa masoko

katika michezo *(sports marketing)*, Mpira wa Miguu, Mpira wa wavu, Netiboli na Mpira wa Kikapu kwa kushirikiana na Vyama vya Michezo/Mashirikisho nchini, jumla ya washiriki 538 wameshiriki na kuhitimu mafunzo hayo, hii ni sawa na ongezeko la asilimia 79.3 ya lengo la washiriki 300 lililowekwa.

**150.** ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya kimehuisha mitaala ya ufundishaji wa kozi ndefu na kuboresha mbinu za ufundishaji *(teaching pedagogy)* ili kukidhi haja ya ualimu wa michezo kwa lengo la kuongeza weledi wa ufundishaji michezo katika shule za msingi na sekondari nchini. Aidha, Chuo kwa kushirikiana na Idara ya Michezo ya Chuo Kikuu cha Dar es salaam kinaendelea na utafiti kuhusu kutofanya vizuri kwa Timu za Taifa katika mashindano ya kimataifa *(An Assessment of "Critical Success Factors Influencing Performance of the Tanzanian National Teams in the International Sporting Competitions")*. Kufanyika kwa utafiti huo kutasaidia kupata suluhu ya kufanya vizuri kwa Timu za Taifa katika mashindano mbalimbali ya Kimataifa.

**151.** ***Mheshimiwa Spika,*** Sambamba na utoaji wa mafunzo kwa wanachuo, Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya kimeendelea kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia kwa kuendelea na ujenzi wa hosteli za wanachuo. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Aprili, 2023, shughuli mbalimbali zimefanyika kwa upande wa ujenzi wa hosteli za wanafunzi, shughuli hizo ni pamoja na ujenzi wa msingi katika hatua ya sakafu; ujenzi wa nguzo na ngazi kuelekea ghorofa ya kwanza; ujenzi wa sakafu ya ghorofa ya kwanza; ujenzi wa nguzo kuelekea ghorofa ya pili; ujenzi wa sakafu ya ghorofa ya pili na ujenzi wa nguzo kuelekea ghorofa ya tatu.



*Muonekano wa Ujenzi wa Hosteli za Wanafunzi unaoendelea katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya. Hosteli hiyo itakuwa na jumla ya ghorofa nne (4) itakapokamilika.*

**152.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa ujenzi wa Akademia ya Michezo (National Sports Academy) katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo (Mshauri Elekezi *(*Consultant*)* amelipwa kwa mujibu wa Mkataba. Mradi huu unatarajiwa kuwa Kituo pekee katika Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati kwa kuwa na viwanja vya michezo, hosteli, bwawa la kuogelea, madarasa, jengo la utawala, multipurpose *hall,* gymnasia na uwanja wa riadha, ambapo viwanja vyote hivi vinajengwa kukidhi viwango vya Olimpiki. Hadi kufikia Aprili, 2023 kazi zilizokamilika ni pamoja na maandalizi ya eneo la ujenzi wa kituo; kuhuisha mipaka ya eneo kwa ajili ya kulitambua; kuchora michoro ya mradi; na kutangazwa kwa zabuni ya ujenzi. Mradi huu utakapokamilika unakadiriwa kugharimu shilingi bilioni 33 za Kitanzania.

### 3.2.4 KUIMARISHA UTENDAJI WA WIZARA NA RASILIMALI WATU

**153.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Aprili, 2023 Wizara iliratibu na kuwezesha uendeshaji wa shughuli mbalimbali za ofisi ikiwepo matengenezo ya magari; ununuzi wa mafuta ya magari kwa ajili ya shughuli

mbalimbali za uendeshaji wa ofisi; kuwezesha utoaji wa huduma za usafi na ulinzi wa ofisi, Viwanja vya Benjamin Mkapa na Uhuru na kwenye makazi ya viongozi; kulipa pango la Ofisi katika jengo la PSSSF Jijini Dodoma; kulipa umeme katika Ofisi za Mtumba, PSSSF, Ofisi za Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika na Viwanja vya Benjamin Mkapa na Uhuru. Aidha, imewezesha upatikanaji wa shajala na vitendea kazi vingine vya ofisi ikiwemo samani, magari na kompyuta.

**154.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilisimamia upatikanaji wa stahili mbalimbali za viongozi na watumishi ikiwemo malipo ya nauli za likizo, posho za kujikimu, na vibali vya likizo. Pia, imeendelea kuratibu safari za viongozi na watumishi za ndani na nje ya nchi. Aidha, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara ilipokea kibali cha ajira cha watumishi 17 wa kada mbalimbali wakiwemo Maafisa Utamaduni, Michezo, Ugavi, Wachumi na Watakwimu. Mchakato wa kuwapata maafisa hao unaendelea ambapo Wizara imewasilisha kibali hicho katika Ofisi ya Sekretarieti ya Ajira kwa ajili ya kukamilisha suala hilo.

## 4.0 CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA NA HATUA ZILIZOCHUKULIWA KUKABILIANA NAZO

**155.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na mafanikio yaliyopatikana mwaka 2022/23, changamoto katika utekelezaji wa majukumu hazikosekani. Changamoto hizo na hatua zilizochukuliwa na Serikali ni kama ifuatavyo:

(i) Mtiririko wa mahitaji ya fedha kutoendana na mahitaji ya Wizara hususan kwa miradi ya maendeleo. Aidha, ukomo mdogo wa bajeti ya Wizara ikilinganishwa na maelekezo makubwa ya kutekeleza shughuli za kutangaza Taifa, Kikanda na Kimataifa.

Wizara iliendelea kuwasiliana na Wizara ya Fedha na Mipango kuhusu upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kutekeleza majukumu na maelekezo mbalimbali yaliyotolewa kwa Wizara ambayo awali hayakupangiwa bajeti. Aidha, Wizara imeendelea kufanya mazungumzo na Balozi mbalimbali nchini zikiwemo za Saudi Arabia, China, Qatar, Uswizi, Ujerumani, Ufaransa, Uhispania, Falme za Kiarabu (UAE) na Uturuki ili kushirikiana katika maeneo mahsusi.

(ii) Kukosekana kwa mifumo thabiti ya kiteknolojia ya kufuatilia matumizi na mapato ya watumiaji wa kazi za sanaa na ubunifu zinazosimamiwa na Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Namba 7 ya mwaka 1999.

Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kufanyika kwa marekebisho ya sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki, Sura 218 na kutokana na maandalizi ya Kanuni za uanzishwaji wa kampuni za ukusanyaji na ugawaji mirabaha (CMOs) zitakazoanzisha mifumo ya upatikanaji wa taarifa za mapato na matumizi ya kazi za muziki zitakazotumika katika kukusanya na kugawa mirabaha. Aidha, COSOTA ipo katika hatua ya kuwa na mfumo unaojitegemea utakaosaidia katika kuhakiki taarifa za kampuni wakati wa kugawa mirabaha;

(iii) Upungufu wa vitendea kazi vikiwemo magari kwa upande wa Wizara pamoja na Taasisi zake.

Wizara imeendelea kuandaa maandiko ya miradi kwa ajili ya kuwasilishwa kwa Wadau

na Washirika wa Maendeleo kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya Wizara ikiwemo ununuzi wa vitendea kazi;

(iv) Uelewa mdogo wa jamii hususan vijana kuhusu umuhimu wa kuhifadhi na kuenzi urithi wa ukombozi wa Bara la Afrika na nafasi ya Tanzania kama kitovu cha harakati za Ukombozi wa Bara la Afrika.

Wizara kupitia Kituo cha Programu ya Urithi wa Ukombozi imeendelea kutoa elimu kupitia makongamano, mitandao ya kijamii na kufanya maonesho mbalimbali ya kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa kulinda urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika.

(v) Upungufu wa watumishi katika kada mbalimbali za michezo na utamaduni hususan katika Halmashauri nchini. Pamoja na kufanikiwa kuanzishwa kwa Vitengo vya utamaduni na Michezo katika Halmashauri, kumekuwa na changamoto ya Vitengo hivyo kukosa wataalamu wanaostahili. Pia Vitengo kutokupewa kipaumbele katika Halmashauri na kutokupangiwa bajeti ya kutekeleza majukumu yao ya kibajeti.

Katika kutatua changamoto hizo, Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya kimeongeza mtaala wa elimu ya cheti na vituo vya mafunzo ili kuongeza idadi ya wataalamu mbalimbali wa michezo, na Chuo cha Sanaa na Utamaduni Bagamoyo pia kimeongeza kiwango cha udahili ili kuongeza idadi ya Maafisa Utamaduni nchini. Aidha, Wizara inaendelea kuwasiliana na Ofisi ya Rais TAMISEMI ili kujaza nafasi ambazo hazina wataalamu sahihi na pia Wizara inaendelea kuwasiliana na OR – TAMISEMI kuzielekeza Halmashauri kuviwezesha Vitengo kwa kuvitengea bajeti.

**156.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nilifahamishe Bunge lako tukufu kuwa Vitengo hivi ni muhimu sana katika jamii yetu kwa sababu vina kazi kubwa ya kuihimiza na kuielimisha jamii yetu kuzingatia na kufuata maadili ya Kitanzania. Kwa sasa kumekuwa na kasi kubwa sana ya jamii yetu kuvamiwa na utamaduni wa kimagharibi ambayo ni hatari sana kwa jamii yetu kupoteza utamaduni na maadili yetu. Niwaombe Wakurugenzi wa Halmashauri zote nchini kuvitengea Vitengo hivi bajeti na majukumu yanayostahili.

**157.** ***Mheshimiwa Spika,*** Utamaduni ni utambulisho, kielelezo cha uhai na utashi wa watu katika Taifa. naomba niwakumbushe kauli ya Baba wa Taifa hili Hayati Mwl. Julius Kambarage Nyerere aliyoitoa wakati alipokuwa akifungua kwa mara ya kwanza Wizara ya Utamaduni mwaka 1962 alisema, nanukuu "***Nchi inayokosa utamaduni wake ni sawa na mkusanyiko wa watu usiokuwa na roho na hivyo kukosa sifa ya kuitwa Taifa kamili***". Mwisho wa kunukuu. Kwa nukuu hiyo ni dhahiri kuwa Sekta ya Utamaduni ni muhimu sana kuliko kitu chochote tunachokifanya na ndiyo maana kwa kutambua hilo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizipa umuhimu wa kipekee Sekta hizi ikiwa ni pamoja na kuzitenga na Idara ya Habari-MAELEZO ili ziweze kutambulika kwa wananchi na kujipambanua katika majukumu yanayotekelezwa na Sekta hizi. Hivyo, Watanzania kwa pamoja tuungane kulinda maadili na utamaduni wetu.

## 5.0 MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24

**158.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha wa 2023/24 Wizara na Taasisi zake kwa kushirikiana na wadau itatekeleza majukumu mbalimbali kwa kuzingatia maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) (2020-2025); Ahadi na Maelekezo mbalimbali ya Viongozi wa Kitaifa; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26); na Mpango Mkakati wa Wizara wa Mwaka 2021/22 - 2025/26. Aidha, utekelezaji wa majukumu utazingatia pia malengo ya Umoja wa Mataifa kuhusu Maendeleo Endelevu ya Mwaka 2030 katika maeneo yanayohitaji kuchukuliwa hatua na Wizara, pia utazingatia Mwongozo wa Bajeti wa mwaka 2023/24. Majukumu yatakayotekelezwa yanaainishwa kama ifuatavyo kwa kila Sekta.

### 5.1 SEKTA YA UTAMADUNI

#### 5.1.1 IDARA YA MAENDELEO YA UTAMADUNI

**159.** ***Mheshimiwa Spika***, malengo yaliyopangwa kutekelezwa ni kuratibu na kuendesha vipindi vya Redio na Televisheni,

makongamano na midahalo kuhusu namna ya kukabiliana na mmomonyoko wa maadili nchini; kufanya Tamasha la Kitaifa la Utamaduni pamoja na kuratibu Matamasha ya Kiutamaduni katika Kanda saba (7) za Utamaduni ili kusherehekea Uanuai wa Urithi wa Utamaduni; kuratibu vikao vitatu (3) vya wadau wa Sekta ya Utamaduni vya kukamilisha uhuishaji wa Sera ya Taifa ya Utamaduni ya mwaka 1997 pamoja na kuandaa Mkakati wa Utekelezaji wake; na kukamilisha zoezi la upatikanaji wa Vazi la Taifa. Majukumu mengine ni pamoja na kutafiti, kukusanya na kuhifadhi elementi za Urithi wa Utamaduni Usioshikika na kuandaa ripoti ya miaka minne ya utekelezaji wa Mkataba wa UNESCO wa mwaka 2003 unaohusu Kulinda Urithi wa Utamaduni Usioshikika; kuratibu na kushiriki katika mikutano, makongamano, maadhimisho na matamasha ya kiutamaduni ya kitaifa, kikanda, na kimataifa; kuandaa mkutano wa wadau kuhusu kuanzisha mchakato wa Sheria ya Taifa ya Kulinda Urithi wa Utamaduni Usioshikika; kufanya Vikao Kazi viwili (2) vya Maafisa Utamaduni nchini; kusimamia na kuratibu utekelezaji wa shughuli za Baraza la Kiswahili la Taifa; Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika; na kuratibu shughuli za Mfuko wa

Utamaduni na Sanaa Tanzania.

### 5.1.2 BARAZA LA KISWAHILI LA TAIFA (BAKITA)

**160.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2023/24 majukumu yaliyopangwa kutekelezwa ni pamoja na kuratibu maadhimisho ya pili ya Siku ya Kiswahili Duniani; kutekeleza *Mkakati wa Taifa wa Kubidhaisha Kiswahili* wa mwaka 2022 – 2032 kwa kutoa mafunzo ya stadi za kufundisha Kiswahili kama lugha ya kigeni kwa diaspora 150, kuchapisha vitabu 2 vya kufundishia na kujifunzia Kiswahili; kuimarisha Kiswahili nchini na kukitangaza kimataifa; kutoa elimu ya matumizi sanifu na fasaha ya lugha ya Kiswahili kwa kuandaa na kurusha hewani jumla ya vipindi 700 kupitia redio na televisheni. Pia, makala 30 zitachapishwa katika magazeti na maudhui mbalimbali kuhusu Kiswahili yatatolewa kupitia mitandao ya kijamii ambayo ni YouTube, Facebook na Twitter; kutoa mafunzo ya kuimarisha stadi za kufundisha Kiswahili kwa wageni kwa wataalamu 250 kutoka katika mikoa mbalimbali ya Tanzania; na kutoa semina kuhusu matumizi bora ya Kiswahili kwa waandishi na watangazaji kutoka vyombo vya habari duniani. Majukumu mengine ni kutoa

ithibati kwa miswada 85 ya vitabu vya kiada na ziada; kuendesha mafunzo kwa wakalimani 30 wa lugha mbalimbali; kutoa huduma ya tafsiri kwa nyaraka 700 na kuthibitisha tafsiri 3,000 zinazofanywa na wakala wake; kutambua na kusajili jumla ya wataalamu 400 katika kanzidata ya wataalamu wa Kiswahili; na kutambua na kutoa ithibati ya vituo 3 vya kufundisha Kiswahili kwa wageni.

### 5.1.3 MFUKO WA UTAMADUNI NA SANAA TANZANIA

**161.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2023/24 Mfuko wa Utamaduni na Sanaa umepanga kutoa huduma zake kwa kuzingatia makundi maalum, mgawanyiko kisekta na mikoa ya Tanzania Bara. Aidha, Mfuko utawezesha miradi ya Utamaduni na Sanaa 650 kiasi cha Shilingi bilioni 9.5 kwa wastani wa miradi 25 kwa kila Mkoa. Kipaumbele kitawekwa kwa miradi inayomilikiwa na makundi maalumu yaani wanawake, vijana na wenye ulemavu ili waweze kujikwamua kiuchumi na kuchangia katika Pato la Taifa. Mfuko umepanga kutoa mafunzo kwa wadau 6,000 nchini. Aidha, mkazo utawekwa katika eneo la usimamizi wa miradi, utunzaji wa kumbukumbu, utamaduni wa kujiwekea akiba,

uwekezaji, urasimishaji na maadili. Aidha, Mfuko umekwisha andaa mpango wa kuzishirikisha taasisi za fedha katika utoaji wa huduma ambapo mpango huu utasaidia kusogeza huduma katika maeneo ambapo wananchi wanaishi. Jumla ya Ajira 59,150 zinatarajiwa kuzalishwa kupitia miradi 650 itakayowezeshwa ambapo ajira za kudumu zinatarajiwa kuwa 19,700 na ajira za muda 39,450.

## 5.2 SEKTA YA SANAA

### 5.2.1 IDARA YA MAENDELEO YA SANAA

**162.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2023/24, Serikali kupitia Wizara itaendelea na Maandalizi ya Sera ya Maendeleo ya Sanaa; kusimamia maboresho ya Sheria na Kanuni za sekta; kusimamia Ujenzi wa Sanamu ya Mwalimu Nyerere katika Jiji la Addis Ababa nchini Ethiopia; kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Wadau wa Muziki wa Afrika (Music in Africa Conference (ACCES); kuratibu Mashindano ya Kimataifa ya Urembo na Utanashati kwa Viziwi na Tamasha la Sanaa na Utamaduni kwa Viziwi Duniani; na kuratibu matumizi ya Sanaa kutangaza utekelezaji wa Serikali wa shughuli za maendeleo. Aidha, Serikali itaendelea kuratibu kutangaza

vipaji vya Wasanii wa Tanzania kitaifa na kimataifa kupitia Tamasha la Serengeti Music Festival; kuratibu shughuli za Burudani katika Maadhimisho ya Siku za Uhuru na Muungano; kuratibu mashindano ya Sanaa kwa vijana kupitia UMMISETA, UMITASHUMTA, Taifa Cup na mashindano mengine; na kuratibu Tamasha la Sauti za Busara, Masai Festival, Usiku wa Taarabu, kuratibu kutumia sanaa kuhamasisha vijana kushiriki kilimo, na shughuli nyingine za Kitaifa na Kimataifa kwa kushirikiana na wadau.

### 5.2.2 BODI YA FILAMU TANZANIA

**163.** ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu yatakayotekelezwa ni kusimamia maudhui ya filamu nchini kwa kuhakiki na kupanga katika madaraja filamu 1,500; kurasimisha shughuli/biashara za filamu na kutoa leseni 200 za uendeshaji wa shughuli/biashara hizo; kushughulikia maombi na kutoa vibali 1,300 vya uandaaji wa filamu nchini; kuwatambua wadau wa filamu na Michezo ya Kuigiza kwa kutoa vitambulisho 1,200 kwa wadau hao; kuendesha Tamasha la Kitaifa la utoaji wa Tuzo za Filamu; kuendesha programu/mafunzo kwa lengo la kuwajengea uwezo wadau wa filamu; kuendelea na mkakati wa kuyabaini na kuyatangaza

maeneo ya upigaji picha za filamu nchini; na kuendelea kuwawezesha wadau kutumia huduma za Bodi kupitia mfumo wa Utambuzi wa wadau (Arts Management Information System-AMIS) pamoja na kuwasajili.

### 5.2.3 BARAZA LA SANAA LA TAIFA (BASATA)

**164.** ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu yatakayotekelezwa ni kuimarisha ubunifu na utengenezaji wa sanaa bora; kuimarisha mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU/UKIMWI; kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa mahala pa kazi; kuimarisha Utawala bora katika kutekeleza shughuli za Baraza na uendeshaji wa Sekta ya Sanaa; kuimarisha na kuongeza mapato ya Baraza; kukarabati na kujenga vituo vya sanaa na Ofisi za Baraza; kuimarisha utoaji habari, mawasiliano ya Umma na ushawishi; kusimamia maslahi ya wasanii yasiyo ya hakimiliki au hakishiriki; kuendesha elimu na shughuli za sanaa katika shule za Msingi na Sekondari; kusimamia matumizi ya sanaa za jadi; na kuimarisha ushiriki wa jamii katika shughuli za Sanaa.

### 5.2.4 OFISI YA HAKIMILIKI TANZANIA (COSOTA)

**165.** ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu yatakayotekelezwa ni kusimamia Makampuni ya Wasanii wenyewe yaliyoidhinishwa kukusanya na kugawa miraba; kutoa leseni/kukusanya mirabaha kwa watumiaji wa kazi za ubunifu katika maeneo ambayo hayatakuwa chini ya CMOs; kukusanya mapato kutoka katika vibebeo tupu (blanktape devices); kusajili kazi za ubunifu na wasanii, waandishi na wabunifu; kukagua uharamia wa kazi za wabunifu; kutatua migogoro na utaoji msaada wa kisheria; na kufanya kampeni kubwa kwa kutoa Elimu kwa Umma kuhusu hakimiliki na hakishirikishi.

### 5.2.5 TAASISI YA SANAA NA UTAMADUNI BAGAMOYO (TaSUBa)

**166.** ***Mheshimiwa Spika,*** TaSUBa katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Juni, 2024 imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo; Kudahili wanachuo wapatao 750 kwa kozi ndefu na 250 kwa kozi fupi; kuendesha semina 4, warsha 4 na kongamano 1; kuendelea na ukarabati wa ukumbi mkuu wa maonesho, ukumbi wa "flexible", Jukwaa la Mwembeni, nyumba ya Mkuu wa Chuo, kununua vifaa vya

kufundishia na kujifunzia, kununua vifaa vya jukwaa la kuendeshea Tamasha, kuimarisha miundombinu ya TEHAMA na Kununua Samani za Ofisi; kupata ithibati kwa mitaala mipya mitatu (3); kununua na kusimika mitambo ili kuanza kurusha matangazo katika Kituo cha Redio na TV; kuanza mchakato wa kupata eneo la kuanzisha kampasi ya mafunzo Dodoma; kuendesha Tamasha la 42 la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni la Bagamoyo; kuimarisha mtandao (Networks) kati ya Taasisi na wadau wa sanaa nje na ndani ya nchi; na kuandaa Mpango Mkakati wa Kutangaza Taasisi (Communication Strategy).

## 5.3 SEKTA YA MAENDELEO YA MICHEZO

### 5.3.1 IDARA YA MICHEZO

**167.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Juni, 2024, Serikali kupitia Wizara itatekeleza majukumu mbalimbali, miongoni mwa majukumu hayo ni pamoja na kujenga na kukarabati miundombinu ya michezo; kuandaa kongamano la wadau wa Sekta ya michezo; kuratibu ushiriki wa Tanzania katika mashindano ya Kimataifa ikiwa ni pamoja na Mashindano ya Afrika (AAG) na michezo ya Afrika

Mashariki; kusambaza na kutoa elimu kuhusu Mkakati wa Maendeleo ya Michezo kwa wadau wa Sekta; kupambana na dawa na mbinu haramu katika michezo; na kuratibu kikao kazi cha mwaka cha maafisa michezo. Majukumu mengine ni pamoja na kuratibu mashindano ya Kitaifa ya UMITASHUMTA na UMISSETA kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; kuratibu mashindano ya *Tanzanite International Women Sports Festival* na Taifa Cup mtaa kwa mtaa kwa kushirikiana na BMT; kuratibu matunzo na matumizi ya eneo changamani la michezo la Taifa (viwanja vya Benjamin Mkapa na Uhuru); kutoa huduma ya kinga na tiba kwa wanamichezo; kuratibu ushiriki wa Tanzania katika mikutano ya Kimataifa inayohusu sekta ya michezo; na kuratibu mashindano ya Fainali ya Mpira wa Miguu Bara la Afrika (AFCON 2027) kwa kushirikiana na nchi ya Kenya na Uganda.

### 5.3.2 BARAZA LA MICHEZO LA TAIFA (BMT)

**168.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24 majukumu yaliyotekelezwa ni pamoja na kuendelea kuwezesha na kuzigharamia Timu za Taifa 15 kushiriki mashindano mbalimbali ya

Kimataifa; kuendelea kutoa mafunzo ya utaalamu wa michezo na usimamizi kwa wataalamu 150 ili kupata wataalamu wa michezo nchini; kuendelea kusajili Vyama/Mashirikisho na vilabu vya michezo vipatavyo 200; kuratibu matamasha mawili ya Michezo ya Wanawake (Tanzanite); kuendelea kuhamasisha Utawala Bora katika vyama na mashirikisho ya michezo 48; kuratibu na Kusimamia Mfumo wa Usajili wa kidijitali (Online Registration); kuidhinisha vibali 180 vya matukio mbalimbali ya michezo; na kuendelea kutoa tuzo kwa wanamichezo bora kwa michezo yote inayochezwa Tanzania, kuendelea kufanya ufuatiliaji wa Kamati za Michezo ngazi za mikoa na Wilaya ili kusimamia kikamilifu programu za kuinua na kuendeleza vipaji katika ngazi za chini.

## 5.4 MIRADI YA MAENDELEO

**169.** ***Mheshimiwa Spika,*** Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika, katika mwaka wa fedha 2023/24 umetengewa jumla ya shilingi 450,000,000 na shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na kukamilisha ukarabati wa jengo lililotumiwa na Kamati ya Ukombozi ya O.A.U pamoja na kufanya ukarabati wa makaburi na mahandaki yenye urithi wa ukombozi wa Afrika;

kutambua na kukusanya kumbukumbu na taarifa za Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika unaoshikika na usioshikika ndani na nje ya Nchi; kutayarisha na kuchapisha vitabu vya mashujaa wa ukombozi wa Afrika; R.M. Kawawa, S.A. Salim, J.S. Warioba, na Br. Gen. H. Mbita; kuratibu maadhimisho ya Siku ya Ukombozi wa nchi za Kusini mwa Afrika (Machi 23) na Siku ya Afrika (Mei 25), kwa ajili ya kutoa elimu kuhusu historia ya ukombozi wa Afrika; na kufanya ziara kwenye Matawi ya Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Afrika katika Nchi za Kusini mwa Afrika kwa ajili ya kutoa mwongozo wa uendeshaji wake.

**170.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania, katika mwaka wa fedha 2023/24 umepangiwa jumla ya shilingi 1,600,000,000 na shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na kuendelea na utoaji wa mikopo, ruzuku na mafunzo kwa wadau wa sekta ya utamaduni na Sanaa; kuunda Mfumo wa Kielektroniki wa kanda ili kuweza kutoa huduma kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa kazi na kuwafikia walengwa wengi kwa urahisi.

**171.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24 Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) kupitia Mradi wa Kuimarisha BAKITA na Kukibidhaisha Kiswahili umetengewa jumla ya shilingi 300,000,000 kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya kuanzisha vituo 8 vya kufundisha Kiswahili kupitia balozi za Tanzania nje ya nchi na kutoa mafunzo ya kuimarisha stadi za kufundisha Kiswahili kwa wageni kwa diaspora na wenyeji katika nchi husika na kuandaa Kongamano la Kiswahili nje ya nchi.

**172.** ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusiana na mradi wa ujenzi wa Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya, katika mwaka 2023/24 umetengewa jumla ya Shilingi 610,000,000 na shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na kuendelea na ujenzi wa Hosteli za wanafunzi; na kukarabati madarasa matatu (3).

**173.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa ujenzi wa Akademia ya Michezo Malya kwa mwaka 2023/24 umetengewa jumla ya Shilingi 470,000,000 na shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na kuanza awamu ya kwanza ya ujenzi wa Akademia utakaohusisha miundombinu ya msingi ya viwanja vya michezo, vyumba vya

kubadilishia nguo na hosteli.

**174.** ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusiana na Ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo Dodoma, katika mwaka wa fedha 2023/24 umetengewa Shilingi 60,000,000 na shughuli zitakazotekelezwa ni kupata Mshauri Elekezi na kuhuisha upembuzi yakinifu wa mradi utakaohusisha uhuishaji wa michoro, gharama za ujenzi, utafiti wa athari za mazingira na andiko la biashara (business plan). Aidha, pamoja na kujenga uwanja mpya jijini Dodoma, Serikali itajenga uwanja mwingine wa kisasa jijini Arusha, ambao unatarajiwa kutumika katika mashindano ya AFCON 2027 endapo nchi za Afrika Mashiriki zitashinda zabuni ya kuandaa mashindano hayo.

**175.** ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusiana na Ujenzi wa Vituo vya Mazoezi na Kupumzika Wananchi (Recreational Centre) katika mwaka 2023/24 umetengewa Shilingi 4,760,000,000 na shughuli zitakazotekelezwa ni kukamilisha awamu ya kwanza ya vituo vya mazoezi na kupumzika wananchi katika majiji ya Dar es Salaam na Dodoma. Awamu hiyo itahusisha ujenzi wa hosteli zenye uwezo wa kuchukua watu 50; viwanja vya michezo ikiwemo uwanja wa

mpira wa miguu wa nyasi halisi na nyasi bandia; ujenzi wa viwanja vya mpira wa kikapu, pete, na wavu.

**176.** ***Mheshimiwa Spika***, mradi wa Ujenzi wa *Sports and Arts Arena* katika mwaka 2023/24 umetengewa jumla Shilingi 130,000,000 shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na kupata Mshauri Elekezi na kufanya upembuzi yakinifu wa mradi utakaohusisha michoro, gharama za ujenzi, utafiti wa athari za mazingira na andiko la biashara (*business plan*).

**177.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mfuko wa Maendeleo ya Michezo ni mradi ambao utatekelezwa katika mwaka 2023/24 na umetengewa jumla ya Shilingi 101,160,000 majukumu yaliyopangwa kutekelezwa ni kuendelea kugharamia timu za Taifa ikijumuisha makocha; kutoa mafunzo kwa wataalamu wa michezo nchini; kuratibu mashindano ya Kitaifa na kimataifa; kutekeleza programu za kuendeleza michezo kwa wanawake; na kuendelea kuboresha na kukarabati miundombinu ya michezo.

**178.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo Dar es Salaam katika

mwaka 2023/24 umepangiwa jumla ya Shilingi 1,120,000,000 na shughuli zitakazotekelezwa ni kuendelea kufanya ukarabati mkubwa wa uwanja wa Benjamin Mkapa katika eneo la kuchezea (pitch), mfumo wa umeme, mfumo wa zimamoto, mfumo wa maji, kubadilisha maeneo ya mashabiki, na majukwaa ya watu mashuhuri; kuendelea kufanya ukarabati mkubwa wa uwanja wa Uhuru katika maeneo ya kuweka viti vya watazamaji, kuweka *Score Board (Big Screen)*, kuweka mfumo wa sauti (*Sound system*) katika uwanja, kuboresha na kujenga vyumba vya kubadilishia nguo, kubadilisha paa la Uwanja kwa kuweka mabati mapya katika mzunguko, kuboresha Mfumo wa Maji Taka, na kuweka mfumo wa Ulinzi wa CCTV na kukarabati viwanja vitano (5) vya majiji ya Mwanza, Arusha, Dodoma, Tanga na Mbeya.

**179.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi wa Ujenzi na Uimarishaji wa Miundombinu ya Michezo katika Shule Maalumu za Michezo kwa mwaka 2023/24 umepangiwa Shilingi 1,360,000,000 shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na kuendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya michezo katika shule teule 56 za michezo.

**180.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ukarabati wa Chuo cha Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa), katika mwaka 2023/24 umetengewa Shilingi 570,000,000 na shughuli zitakazotekelezwa ni kuendelea na ukarabati wa ukumbi mkuu wa maonesho, ukumbi wa "flexible", Jukwaa la Mwembeni, nyumba ya Mkuu wa Chuo, kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia, kuimarisha miundombinu ya TEHAMA na Kununua Samani za Ofisi; kununua na kusimika mitambo ili kuanza kurusha matangazo katika Kituo cha Redio na TV; na kuendesha na kuimarisha miundombinu ya Tamasha la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni la Bagamoyo.

**181.** ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa Jumba Changamani la Filamu ni mradi utakaotekelezwa katika mwaka 2023/24 ambapo umetengewa Shilingi 100,000,000 na shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na kuanza maandalizi ya mradi kwa kufanya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina wa mradi na kuandaa andiko la kibiashara (*business plan*); na kuanza hatua za maandalizi ya ujenzi.

**182.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ujenzi wa Ukumbi wa Wazi wa Sanaa katika mwaka 2023/24 umepangiwa Shilingi 200,000,000 na shughuli zitakazotekelezwa ni kukamilisha ujenzi wa ukumbi wa wazi wa Sanaa katika eneo la Ilala Shariff Shamba Jijini Dar es Salaam; na kununua vifaa vya sauti na taa kwa ajili ya ukumbi.

## 5.5 KUIMARISHA UTENDAJI WA WIZARA NA RASILIMALI WATU

**183.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kuratibu na kuwezesha uendeshaji wa shughuli za ofisi. Kwa mwaka 2023/24 shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na kuratibu na kuwezesha uendeshaji wa shughuli za ofisi ikiwemo matengenezo na mafuta ya magari, huduma za usafi na ulinzi, kulipa pango la ofisi, umeme na simu pamoja na ununuzi wa vitendea kazi mbalimbali na samani za ofisi. Aidha, Wizara itaendelea na uratibu na kuwezesha mazoezi ya wafanyakazi wote wa Wizara kila wiki mara moja; kuwezesha upatikanaji wa stahili mbalimbali za wafanyakazi ikiwemo uhamisho, likizo, safari za kikazi n.k. na kuendesha vikao viwili vya Baraza la Wafanyakazi. Pia Wizara itaendelea na kuratibu ushiriki wa Wizara katika sherehe za

Mei Mosi, Siku ya Wanawake Duniani, Wiki ya Utumishi wa Umma na Michezo ya SHIMIWI; na kuratibu mafunzo, ajira na upandishwaji vyeo kwa watumishi.

## 6.0 MAKADIRIO YA BAJETI KWA MWAKA 2023/24

### 6.1 MAPATO

**184.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwaka 2023/24 Wizara inatarajia kukusanya jumla ya shilingi Bilioni Moja (Shilingi 1,000,000,000) kupitia Idara ya Maendeleo ya Michezo. Vyanzo vya mapato hayo ni pamoja na viingilio katika matukio ya michezo yanayofanyika katika viwanja vya Benjamin Mkapa na Uhuru, kukodisha kumbi na *gym* zilizopo katika Uwanja wa Benjamin Mkapa na ada za mafunzo na mitihani ya Kitaifa kutoka Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya. Aidha, kwa upande wa Taasisi sita (6) zilizo chini ya Wizara kiasi kinachotarajiwa kukusanywa ni shilingi Bilioni Tano, Milioni Mia Tisa Sabini, Mia Nne Ishirini na Nane Elfu (Shilingi 5,970,428,000). ***Kiambatisho Na. 2*** ni mchanganuo wa mapato yanayotarajiwa kukusanywa na Wizara na Taasisi zake kwa mwaka 2023/24.

## 6.2 MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO

**185.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwaka 2023/24 Wizara imetengewa bajeti ya **shilingi Bilioni Thelathini na Tano, Milioni Mia Nne Arobaini na Tano, na Arobaini na Moja Elfu** (Shilingi 35,445,041,000). Kati ya fedha hizo Mishahara ni **shilingi Bilioni Tisa, Milioni Mia Sita Hamsini na Moja, Mia Mbili Themanini na Tano Elfu** (Shilingi 9,651,285,000), Matumizi Mengineyo ni **shilingi Bilioni Kumi na Tatu, Milioni Mia Tisa Sitini na Mbili, Mia Tano Tisini na Sita Elfu** (Shilingi 13,962,596,000) na Miradi ya Maendeleo ni **shilingi Bilioni Kumi na Moja, Milioni Mia Nane Thelathini na Moja, Mia Moja Sitini Elfu** (Shilingi 11,831,160,000). ***Kiambatisho Na. 3*** kinaonesha mgawanyo wa Bajeti ya Wizara kwa Idara na Vitengo, Taasisi zilizo chini ya Wizara na Miradi ya Maendeleo.

## 7.0 MAOMBI YA FEDHA KWA AJILI YA KUTEKELEZA MPANGO WA MWAKA 2022/23

**186.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kutekeleza majukumu ya Wizara katika mwaka 2023/24 naomba sasa niliombe Bunge lako Tukufu liridhie na kuidhinisha Bajeti ya Wizara ya Utamaduni,

Sanaa na Michezo kwa mwaka 2023/24 yenye jumla ya **shilingi Bilioni Thelathini na Tano, Milioni Mia Nne Arobaini na Tano, na Arobaini na Moja Elfu** (Shilingi 35,445,041,000). Kati ya fedha hizo Mishahara ni **shilingi Bilioni Tisa, Milioni Mia Sita Hamsini na Moja, Mia Mbili Themanini na Tano Elfu** (Shilingi 9,651,285,000), Matumizi Mengineyo ni **shilingi Bilioni Kumi na Tatu, Milioni Mia Nane Thelathini na Moja, Mia Moja na Sitini Elfu** (Shilingi 13,831,160,000) na Miradi ya Maendeleo **ni shilingi Bilioni Kumi na Moja, Milioni Mia Nane Thelathini na Moja, Mia Moja Sitini Elfu** (Shilingi 11,831,160,000).

## 8.0 MWISHO NA SHUKURANI

**187.** ***Mheshimiwa Spika**,* kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, naomba kutumia fursa hii kuwashukuru wale wote waliochangia kwa namna moja au nyingine katika kuiwezesha Wizara kufanikisha majukumu yake. Mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2022/23 yametokana na ushirikiano na misaada ya kifedha na kiufundi kutoka kwa nchi wahisani, mashirika mbalimbali, taasisi za fedha, taasisi za hiari zisizokuwa za kiserikali na mashirika ya kidini bila kusahau hamasa na ushiriki wa

wananchi wakiongozwa na Waheshimiwa Wabunge.

**188.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa wadau siyo rahisi kuwataja wote kwa majina, nitawataja wachache nikianza na wadau wa ndani, ambao ni Kampuni za Azam Media; Multichoice Tanzania; Airtel Tanzania; Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF); Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) na Benki ya NMB. Wengine ni Tanzania National Park (TANAPA); Mamlaka ya Hifadhi ya Bonde la Ngorongoro (NCA); Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA); Benki ya CRDB; Tanzania House of Talent (THT); Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC); na Makumbusho ya Taifa. Aidha, wadau wengine ni pamoja na Shirika la Bima la Taifa (NIC); Programu ya kudhibiti UKIMWI (NACP); Wakala wa Serikali Mtandao (eGA); Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha (AICC); Shirika la Culture and Development East Africa (CDEA); Wakala wa usajili wa Biashara na Leseni (BRELA); Kampuni ya Startimes; Hotel ya Onomo Dar es Salaam; Kampuni ya Wanene Entertaiment; Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS); Kituo cha Televisheni cha DSTV; na Vituo vya Redio vya CLOUDS Media group, EFM na Wasafi.

**189.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa wadau wa nje, naomba nianze na Balozi zote za Tanzania katika mataifa mbalimbali, Serikali ya Mji wa Busan nchini Korea ya Kusini; Bagamoyo Friendship Society (Ujerumani); Musicians for a Better Life (Ujerumani); Alwaleed Philanthropies kutoka Saudi Arabia; Jamhuri ya Watu wa China; na Umoja wa Ulaya.

**190.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kumalizia hotuba yangu kwa kumshukuru tena Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maelekezo mahsusi kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara pamoja na Serikali kwa ujumla. Aidha, nawashukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maelekezo na ushauri katika kuimarisha usimamizi wa shughuli za Sekta ya Utamadui, Sanaa na Michezo. Vilevile, namshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miongozo na maelekezo ya mara kwa mara yaliyowezesha kuboresha utendaji wa Wizara.

**191.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kuhitimisha hotuba yangu kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Aidha, hotuba hii inapatikana kwenye tovuti ya Wizara ambayo ni *www.michezo.go.tz*.

**192.** ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa hoja.

# VIAMBATISHO

*Kiambatisho Na.1*

## VITUO VILIYOTAMBULIWA NA BAKITA VYA KUFUNDISHA KISWAHILI KWA WAGENI

| NA | JINA LA KITUO | MWEZI/ MWAKA | MAWASILIANO | NCHI AU MKOA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | SWAHILI DAR LANGUAGE SCHOOL | 11/2018 | S.L.P. 105025, Dar es Salaam, 0 753 073 780 / 0757 093 959 swahilidar@sdl.ac.tz | DAR ES SALAAM |
| 2. | LEAM SWAHILI | 01/2019 | 0755013111 josephinemmbando@gmail.com | DAR ES SALAAM |
| 3. | PEACE CORPS TANZANIA | 04/2019 | 0682866816 swahiliculture@gmail.com embilu@peacecorps.gov | DAR ES SALAAM |
| 4. | MS TCDC | 04/2019 | 0754693260 mgangay@mstcdc.or.tz | ARUSHA |
| 5. | SOUTH AFRICA FELLOWSHIP OF CHURCHES | 05/2019 | 0679285828 | AFRIKA KUSINI |
| 6. | ISIDERS LANGUAGES CENTER (NA YA USAJILI 452 497) | 08/2019 | | DAR ES SALAAM |
| 7. | LILINGA SWAHILI SCHOOL | 08/2019 | 0754389956 lilingaswahili@gmail.com | IRINGA |
| 8. | KISWAHILI NA UTAMADUNI | 10/2019 | 0754271263 info@swahilicourses.co.tz | DAR ES SALAAM |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | (KIU) | | | |
| 9. | SWAHILI HUB | 11/2019 | 0712127912 gsolomon@tz.nationmedia.com/ss.gadner@gmail.com | DAR ES SALAAM |
| 10. | ITALY SWAHILI LANGUAGE SCHOOL | 08/2019 | +3937117643550 | ITALIA |
| 11. | MODERN LINGUISTICS AND AFRICAN CULTURAL PROMOTION CENTRE (MOLAC) | O6/2020 | 0717498666<br><br>barheba@gmail.com paschalmulikuza@gmail.com | ARUSHA |
| 12. | NURU CALTURAL AND SWAHILI TRAINING SOLUTION | 08/2020 | 0784767170 S.L.P swahiliculture@gmail.com | DAR ES SALAAM KARIAKOO |
| 13. | UPI INNOVATIONS AND DEVELEPMENT | 15/01/2021 | 0745 203020 | DAR ES SALAAM |
| 14. | KITUO CHA KUFUNDISHA KISWAHILI WAGENI TANGA | 02/04/2021 | 0715235503 | TANGA |
| 15. | SWAHILI COMMUNITY CENTRE | 24/03/2021 | - | DAR ES SALAAM |
| 16. | RAS SIMBA LANGUAGES AND COMPUTER STUDIES | 2021 | 0674400400 | DAR ES SALAAM |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 17. | ETHOPIAN SWAHILI COMMUNITY | 5/2/2022 | +251 927483357 | ETHIOPIA |
| 18. | KIJIWE CHA KISWHILI UJERUMANI | Julai 2022 | +4915778913393 | UJERUMANI |
| 19. | KKKT SHULE YA LUGHA MOROGORO | 2022 | 0755802575 | MOROGORO |
| 20. | MOHAMEDINISM PHILOSPPHY TRAINING CENTRE | Aprili 2022 | 0745531101 | KIBAHA |
| 21. | KITUO CHA UTAMADUNI TANZANIA, SEOUL | Kilianza 2018 lakini usajili umefanywa 2022 | +8210-3334-3835 | KOREA KUSINI |
| 22. | KITUO CHA UBALOZI CHA UFARANSA | 2007 | 0715371853 | UFARANSA |
| 23. | KITUO CHA UBALOZI WA ITALIA 2023 | 2023 | +393509444514 | ITALIA |
| 24. | KITUO CHA UBALOZI CHA UHOLANZI 2023 | 2023 | +255713462601 | UHOLANZI |
| 25. | KITUO CHA UBALOZI WA ZIMBABWE | 2023 | +0713 238952 | ZIMBABWE |
| 26. | KITUO CHA UBALOZI WA HAVANA | 2023 | 0745563626 | CUBA |
| 27. | KITUO CHA UBALOZI WA | 2023 | 0777969606 | SUDAN |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | SUDAN | | | |
| 28. | KITUO CHA UBALOZI WA MAURITIUS | 2022 | | MAURITI US |
| 29. | KITUO CHA UBALOZI WA NIGERIA | 2021 | 0767047477 | NIGERIA |
| 30. | KITUO CHA UBALOZI WA ABU DHABI | 2023 | +971505137884 | FALME ZA KIARABU |
| 31. | KITUO CHA KISWAHILI NA UTAMADUNI BULAWAYO | 2023 | +263772406869 | ZIMBABWE |

*Kiambatisho Na. 2*

# MADUHULI YANAYOTARAJIWA KUKUSANYWA NA WIZARA NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA 2023/24

## a) Maduhuli Yatakayokusanywa na Wizara

### Idara ya Maendeleo ya Michezo

| Kijifungu | Maelezo | Makadirio ya Mapato | |
|---|---|---|---|
| | | Mwaka 2022/23 (sh.) | Mwaka 2023/24 (sh.) |
| 14220133 | Mapato ya Viwanja vya Michezo (Uhuru na Benjamin Mkapa) | 640,000,000 | 907,696,000 |
| 14220143 | Ada za Mafunzo | 259,998,000 | 92,302,000 |
| 14220161 | Mapato kutoka vyanzo mbalimbali | 1,000 | 1,000 |
| 14220211 | Marejesho ya fedha za Umma | 1,000 | 1,000 |
| **Jumla Ndogo** | | **900,000,000** | **1,000,000,000** |
| **JUMLA KUU** | | **900,000,000** | **1,000,000,000** |

## b) Mapato Yatakayokusanywa na Taasisi Zilizo Chini ya Wizara

| Na. | Jina la Taasisi | Makadirio ya Mapato 2022/23 (Sh.) | Makadirio ya Mapato 2023/24 (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1. | Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) | 416,750,000 | 480,228,000 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 2. | Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) | 720,000,000 | 800,000,000 |
| 3. | Bodi ya Filamu Tanzania | 1,359,642,000 | 1,460,000,000 |
| 4. | Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) | 865,063,000 | 950,200,000 |
| 5. | Baraza la Michezo la Taifa (BMT) | 685,000,000 | 920,000,000 |
| 6. | Ofisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA) | 1,350,000,000 | 1,360,000,000 |
| 7. | **JUMLA** | **5,396,455,000** | **5,970,428,000** |

*Kiambatisho Na.3*

# MGAWANYO WA BAJETI YA WIZARA YA MWAKA 2023/24 KWA IDARA NA VITENGO, TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA NA MIRADI YA MAENDELEO

## a) Mgawanyo wa Bajeti ya Wizara kwa Idara na Vitengo

| Kifungu | Idara/ Kitengo | Makisio ya Bajeti Mwaka 2023/24 | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Mishahara (PE) (Sh.) | Matumizi Mengineyo (Sh.) | Jumla (Sh.) |
| 1001 | Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu | 772,854,000 | 5,907,955,000 | 6,680,809,000 |
| 1002 | Fedha na Uhasibu | 274,596,000 | 203,431,000 | 478,027,000 |
| 1003 | Sera na Mipango | 202,704,000 | 362,744,000 | 565,448,000 |
| 1004 | Mawasiliano Serikalini | 176,445,000 | 165,071,000 | 341,516,000 |
| 1005 | Ununuzi na Ugavi | 184,584,000 | 127,794,000 | 312,378,000 |
| 1006 | Ukaguzi wa Ndani | 88,560,000 | 95,834,000 | 184,394,000 |
| 1007 | TEHAMA | 141,468,000 | 243,811,000 | 385,279,000 |
| 1008 | Huduma za Sheria | 61,330,000 | 73,802,000 | 135,132,000 |
| 6001 | Maendeleo ya Utamaduni | 371,714,000 | 566,668,000 | 938,382,000 |
| 6004 | Maendeleo ya Michezo | 808,405,000 | 1,847,805,000 | 2,656,210,000 |
| 6005 | Maendeleo ya Sanaa | 273,756,000 | 794,514,000 | 1,068,270,000 |
| **JUMLA** | | **3,356,416,000** | **10,389,429,000** | **13,745,845,000** |

## b) Mgawanyo wa Bajeti kwa Taasisi Zilizo Chini ya Wizara

| Jina la Taasisi | Makisio ya Bajeti Mwaka 2023/24 | | |
|---|---|---|---|
| | Mishahara (PE) (Sh.) | Matumizi Mengineyo (Sh.) | Jumla (Sh.) |
| **6001 - 26311266** Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) | 942,337,000 | 304,404,000 | 1,246,741,000 |
| **6001 – 26311231** Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania | - | 61,660,000 | 61,660,000 |
| **6005-26311352** Bodi ya Filamu Tanzania | 1,084,355,000 | 308,300,000 | 1,392,655,000 |
| **6005 - 26311267** Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) | 1,147,325,000 | 295,700,000 | 1,443,025,000 |
| **6005 - 26311234** Ofisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA) | 805,364,000 | 1,575,000,000 | 2,380,364,000 |
| **6005 – 26311130** Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) | 1,329,248,000 | 264,200,000 | 1,593,448,000 |
| **6004 – 26311273** Baraza la Michezo la Taifa (BMT) | 986,240,000 | 443,403,000 | 1,429,643,000 |
| **6004 – 6311346** Chuo cha Maendeleo ya Michezo-Malya | - | 320,500,000 | 320,500,000 |
| **Jumla** | **6,294,869,000** | **3,573,167,000** | **9,868,036,000** |
| **JUMLA KUU** | **9,651,285,000** | **13,962,596,000** | **23,613,881,000** |

## c) Mgawanyo wa Bajeti ya Miradi ya Maendeleo

| Na. | Jina la Mradi | Makisio ya Bajeti 2023/24 |
|---|---|---|
| **Idara ya Maendeleo ya Utamaduni** | | |
| 1 | 6293 – Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika | 450,000,000 |
| 2 | 6502 – Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania | 1,600,000,000 |
| 3 | 6521 – Kuimarisha BAKITA na Kubidhaisha Kiswahili | 300,000,000 |
| **Jumla ya Idara** | | **2,350,000,000** |
| **Idara ya Maendeleo ya Michezo** | | |
| 4 | 6385 – Ujenzi wa Chuo cha Michezo Malya | 610,000,000 |
| 5 | 6395 - Ujenzi wa Akademia ya Michezo | 470,000,000 |
| 6 | 6397 - Ujenzi wa Sports Arena (Dar es Salaam na Dodoma) | 130,000,000 |
| 7 | 6398 – Mfuko wa Maendeleo ya Michezo | 101,160,000 |
| 8 | 6503 – Ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo Dodoma | 60,000,000 |
| 9 | 6504 – Ujenzi wa Vituo vya Mazoezi na Kupumzika Wananchi | 4.760,000,000 |
| 10 | 6523 – Ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo Dar es Salaam | 1,120,000,000 |
| 11 | 6527 – Ujenzi na Uimarishaji wa Miundombinu ya Michezo katika Shule za Michezo | 1,360,000,000 |
| **Jumla ya Idara** | | **8,611,160,000** |
| **Idara ya Maendeleo ya Sanaa** | | |
| 12 | 4353 – Ukarabati wa Chuo cha Sanaa Bagamoyo | 570,000,000 |
| 13 | 6355 – Ujenzi wa Ukumbi wa Wazi BASATA | 200,000,000 |
| 14 | 6396 – Ujenzi wa Jumba Changamani la Filamu | 100,000,000 |
| **Jumla ya Idara** | | **870,000,000** |
| **JUMLA KUU YA DEV.** | | **11,831,160,000** |
| **JUMLA KUU YA FUNGU 96 (PE+OC+DEV)** | | **35,445,041,000** |



*Viongozi Wakuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo wakiwa katika picha ya pamoja.*